**5 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Arobaini – Tarehe 5 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja Kikao cha Arobaini tunaanza na Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, karibu.

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini, aulize swali lake.

Na. 516

**Kuipandisha hadhi barabara ya Irambo – Nsonyanga kuwa ya Mkoa**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Irambo - Nsonyanga ambayo inaunganisha barabara ya Isyonje – Makete hadi Njombe na TANZAM itapandishwa hadhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 09 Januari, 2023, kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Njombe kilifanyika ambapo moja ya barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi ni Barabara ya Irambo – Nsonyanga yenye urefu wa kilometa 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara Katika Hadhi Stahiki *(NRCC)* ilifika Mkoani Mbeya tarehe 24 Februari, 2023 na kutembelea barabara zilizoombwa kupandishwa hadhi ikiwemo barabara ya Irambo – Nsonyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati yamewasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na yanachambuliwa na uchambuzi ukikamilika taarifa itatolewa. Endapo barabara hiyo itakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi, itakuwa barabara ya Mkoa na itahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naishukuru Serikali Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alisharidhia kupandisha hadhi hiyo barabara kuwa ya Mkoa. Kwa vile hii barabara iko kwenye hali mbaya sana.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa hii barabara ili ianze kupitika?

Swali la pili, katika hali hiyo hiyo kuna barabara ya Ilembo - Isonso ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe. Je, ni lini hii barabara nayo itapandishwa hadhi kuwa ya Mkoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza kwanza lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii ambayo tayari imeshapandishwa hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, barabara ikiwa imeshakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi na ikapandishwa hadhi na kuwa inahudumiwa na *TANROADS* basi ni wajibu wa *TANROADS* kutenga bajeti hiyo kuweza kutengeneza barabara. Tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi na kuona wao wamejipanga vipi kwa ajili ya kutengeneza barabara hii ambayo ni muhimu sana kule Jimboni kwa Mheshimiwa Njeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la barabara ya Ilembo-Isonso ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe lakini hasa katika Wilaya ya Ileje. Barabara hii itapandishwa hadhi pale ambapo watafuata vile vigezo vya kisheria kama ambavyo barabara nyingine zinafanya. Waanze vikao vyao katika *DCC* waende kwenye *RCC* na baadaye Bodi ya Barabara ya Mkoa na kisha kumwandikia Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi mwenye dhamana ya barabara hizi za Mkoa, ili timu iweze kutumwa kwenda kwenye barabara hii ya Ilembo - Isonso, kufanya tathmini na kisha kumshauri Waziri wa Ujenzi kuhusu barabara hii kupandishwa hadhi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi Mbunge wa Moshi Vijijini.

Na. 517

**Barabara ya Getifonga – Mabogini – Kahe**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa Kiwango cha lami barabara ya Getifonga – Mabogini – Kahe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 kuijenga kwa kiwango cha lami ambapo hadi sasa *TARURA* – Mkoa wa Kilimanjaro wamekamilisha usanifu kwa kiwango cha lami na inahitaji shilingi bilioni 28.59 ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 *TARURA* imetenga shilingi milioni 158.85 kwa ajili ya

matengenezo ya kawaida kwa urefu wa kilomita 12 katika barabara hiyo na kazi imekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa urefu wa kilometa 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri yenye matumaini kutoka Serikalini na nina hakika wananchi wangu wa Mabogini na Kahe watakuwa wamepata faraja kubwa sana. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza tunaishukuru Serikali ilitenga shilingi milioni 475 kutengeneza barabara ya *TPC*, Samanga hadi Chemchem lakini tamanio la wananchi hawa ilikuwa ni kutengeneza daraja kwenye mto Ronga unaounganisha vijiji vya Samanga na Chemchem.

Je, Serikali ina mpango gani kutengeneza daraja hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili barabara ya *International School* Kibosho *KNCU* hadi kwa Raphael haijakamilika kwa kiwango cha lami.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa barabara hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Profesa Ndakidemi, kwanza ni hii barabara ya Samanga – Chemchem kuhitaji daraja katika mto unakopita.

Kwanza kama alivyosema yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge Serikali ilitenga shilingi milioni 475 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii na tutaangalia katika bajeti tunayoenda kuanza hii ya *TARURA* ya mwaka 2023/2024, kuona imetengewa kiasi gani kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili na tutamwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro kuweza kuelekeza fedha mara moja kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili hili la *International School* hadi Kibosho barabara hii. Serikali itaendeleza ujenzi wa barabara hii kadri ya upatikanaji wake wa fedha na tutaangalia Mheshimiwa Mbunge katika bajeti hii inayokuja kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukatenga fedha kwa ajili ya kwenda kuanza ukarabati wa kiwango cha lami kwenye barabara hii.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 518

**Ujenzi wa Bwalo la Shule ya Sekondari Igwachanya – Njombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwalo la Shule ya Sekondari Igwachanya Njombe?

**MWENYEKITI:** majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ikiwemo ujenzi wa

Mabwalo katika Shule za Sekondari nchini. Hata hivyo, natoa rai kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kuanza kutenga fedha kupitia Mapato ya Ndani kwa ajili ya ujenzi wa bwalo katika Shule ya Sekondari Igwachanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema William Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni lini Serikali itakarabati na kujenga upya majengo ya shule chakavu Wilaya ya Njombe, Ludewa, Wanging'ombe na Makete ndani ya Mkoa wa Njombe?

Swali la pili, ni lini Serikali itatua tatizo la upungufu wa Walimu wa Sayansi ndani ya Mkoa wa Njombe? ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgaya, swali lake la kwanza kuhusu ni lini Serikali itakarabati shule hizi kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Daktari Samia Suluhu Hassan ilikwisha karabati shule 89 hapa nchini, ambapo kule Mkoani Njombe kuna shule mbili ambazo zilipata fedha ya kukarabati ambayo ni shule ya Kivavi Sekondari iliyokuwepo Wilayani Makambako vilevile Njombe sekondari. Tunaendelea kuangalia ni namna gani tunaweza tukaendelea ukarabati wa shule kongwe ikiwemo zile zilizokuwepo Mkoani Njombe. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Kairuki analishughulikia hili suala kuona ni namna gani atapata fedha ya ukarabati wa shule hizi kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la Walimu wa Sayansi. Hivi sasa Serikali ipo katika ukamilishaji wa mchakato wa kuajiri Walimu wa Sayansi na walimu kwa ujumla ambao ni 13,390 ambao wataanza kazi muda Serikali mrefu. Kwa

hiyo, nikutoe shaka Mheshimiwa Neema Mgaya kwamba kule Mkoani Njombe nanyi mtapata mgao wa Walimu hawa ambao wanakuja. Mheshimiwa Neema amekuwa akilifatilia sana hili suala na nimwakikishie kwamba Serikali imekusikia na italifanyia kazi suala la upungufu wa walimu katika Mkoa wa Njombe.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo Mbunge wa Moshi Mjini aulize swali lake.

Na. 519

**Kuwezesha shule za kata kuwa na kidato cha tano na sita**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwezesha Shule za Kata kuwa pia za Kidato cha Tano na Sita kutokana na kuongezeka kwa ufaulu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiongeza shule za Kidato cha Tano na Sita kulingana na uhitaji. Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali ilisajili jumla ya shule 23 ambazo zilikuwa Shule za Kata kuwa Shule za Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza shule za Kidato cha Tano na Sita katika Halmashauri zote nchini kwa kuongeza miundombinu ya mabweni, madarasa mabwalo kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha na uhitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo Mbunge wa Moshi Mjini.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kuna Halmashauri zenye uwezo wa kuanza mchakato huu kwa kutumia mapato ya ndani kuweza kuweka hii miundombinu. Ni nini *commitment* ya Serikali kuzisaidia Halmashauri hizi kukamilisha utaratibu huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili je, kama kuna shule zenye miundombinu na ziko tayari kubadilisha baadhi ya madarasa kuwa ya kidato cha tano na sita. Je, Serikali iko tayari kuruhusu watumie *hostel* za binafsi wakati wanasubiri kujenga mabweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimo, kwanza kuhusu Halmashauri ambazo zina uwezo wa kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uko wazi kama, Halmashauri ina uwezo wa kujenga miundombinu inayohitajika kwa ajili ya shule yenye mkondo wa Kidato cha Tano na Sita hawakatazwi kujenga miundombinu hiyo lakini ni lazima wafuate taratibu za kukaguliwa na Mkaguzi wa Elimu kwa kuomba usajili wa Kidato cha Tano na Sita kutoka Wizara ya Elimu na kisha shule hii iweze kupandishwa hadhi. Lakini kama wana uwezo wa kujenga hawakatazwi kuweza kujenga lakini wafuate taratibu za usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili kuhusu shule ambazo tayari zina miundombinu. Kama kuna shule ambazo tayari zina miundombinu hii hawakatazwi nao kuandika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili na tuweze kukagua kuona miundombinu iliyopo na kisha kuwasiliana na Wizara ya Elimu kuweza kuomba sasa usajili wa mkondo wa Kidato cha Tano na Sita. Hivyo, niwaombe wenzetu wa Manispaa ya Moshi Mjini kama wanazo shule ambazo tayari wanaziona zinakidhi vigezo basi waombe kwa

maandishi kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tuweze kutuma timu kwa ajili ukaguzi na kisha kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu kuweza kuona ni namna gani tunapandisha hadhi shule hizi.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Deogratius Ndejembi Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu hayo. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo aulize swali lake.

Na. 520

**Viongozi wastaafu wa vitongoji kutokuwa wanufaika wa *TASAF***

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, kwa nini viongozi wastaafu wa vitongoji na vijiji wenye sifa siyo wanufaika wa *TASAF*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uratibu wa awamu ya kwanza ya mpango wa kunusuru walengwa wa kaya maskini ulipoanza, taratibu zilibainisha kuondoa baadhi ya makundi wakiwemo watumishi wastaafu wanaopokea pensheni, watu walioajiriwa na kuwa na kipato cha uhakika, Viongozi wa Vijiji na Wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii miongoni mwao ni Viongozi wa CCM katika ngazi za Kata na vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maboresho ya taratibu za utambuzi na uandikishaji wa walengwa ya mwaka 2021, Kaya za Viongozi wa kisiasa wakiwemo Mabalozi wa Nyumba Kumi na Viongozi waliopo na wastaafu wa vijiji na vitongoji zinazokidhi

vigezo zilipewa fursa ya kutambuliwa na kuandikishwa kwenye mpango huo wakati wa zoezi la utambuzi na uandikishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa viongozi wastaafu wa vijiji na vitongoji ambao kipindi cha zoezi la utambuzi wa walengwa linafanyika walikubalika na jamii kuorodheshwa awali kuwa katika kaya maskini wajiandishe ili nao waweze kuingia katika mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali na kwa kuwa wananchi hawa viongozi wa vijiji, wastaafu na wa kisiasa ni wananchi ambao walikuwa hawapati mshahara wala hawana pensheni. Kwa Serikali kuwatambua sasa hivi kuwa wao kuwa na fursa miongoni mwa wananchi wengine wa kawaida wa kaya maskini kutambuliwa katika mfumo huu wa *TASAF* mimi sina swali zaidi ya kuishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hana swali, kwa hiyo nakushukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Kikwete kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba swali langu Namba 529 lipate majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae tunakwenda kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwanza kuna dharura, Mheshimiwa Daktari John Danielson Pallangyo Mbunge wa Arumeru.

Na. 528

**Mpango wa ujenzi wa vizimba vya samaki Ziwa Duluti**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa ujenzi wa vizimba vya ufugaji wa samaki katika Ziwa Duluti?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvivu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Duluti ni sehemu ya Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Ziwa Duluti ambao unasimamiwa na Wakala ya Huduma za Misitu *(TFS)*. Hifadhi hiyo ni kivutio cha utalii wa ikolojia, picha, kutembea msituni, kuangalia ndege na viumbe wengine, boti za kupiga kasia na uvuvi wa burudani. Kutokana na hadhi ya eneo tajwa, shughuli za kiuchumi zinadhibitiwa ili kutokuharibu ikolojia na bioanuwai iliyopo katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuahidi Mheshimiwa John Danielson Pallangyo Mbunge, kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara yangu itafanya utafiti kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *TAFIRI* kwa kushirikiana na *TFS* ili kuona kama ufugaji wa Samaki wa vizimba unaweza kufanyika bila kuathiri ikolojia na bioanuai katika Ziwa Duruti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Pallangyo.

**MHE.JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka Serikalini lakini napenda kuuliza swali moja la ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi inaonekana kama sasa hivi ina mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa nchi. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kujengwa mabwawa maeneo ya Malula na maene ya Majengo ambako kila mwaka mvua zinaleta mafuriko, yale maji yavunwe yajengwe mabwawa kwa ajili ya kufugia Samaki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UVUVI NA UFUGAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza nibampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua mchango wa Uvuvi katika uchumi wetu na hata maoni ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza hapa kwamba tuanze sasa kujenga mabwawa kwa ajili ya kuboresha sekta ya uvuvi ni sehemu ya mpango tulionao sasa hivi. Kwa hiyo, tunachokifanya sasa hivi ni kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunafika kwenye maeneo yote hususan maeneo ambayo hayana maji mengi kwa maana ya Maziwa na Bahari, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo aulize swali lake.

Na. 529

**Ujenzi wa Soko la Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamalizia fedha za ujenzi wa Soko la samaki Bagamoyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu : -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo n Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Samaki Bagamoyo limejengwa kwa fedha za Serikali kupitia Halmashauri ya Bagamoyo na limeshaanza kutumiwa na wadau wa uvuvi. Kwa sasa soko hili lina miundombinu ya jengo la mnada, jengo la kuhifadhia samaki, jengo la maliwato, jengo la kuhifadhia taka, kibanda cha askari/mlinzi na jengo la kukaangia samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha soko hili kuendana na michoro iliyopo, inahitajika kuongezewa jengo moja la kukaangia samaki, jengo la mama lishe, jengo la maduka na jengo la ofisi. Aidha, katika mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kujenga miundombinu hiyo iliyosalia katika soko hilo kupitia Programu ya

Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Programme - AFDP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi itaweka vichanja kumi (10) vya kuanikia dagaa, mahema mawili (2) ya kukaushia samaki kwa kutumia nguvu ya jua na mtambo mmoja wa kuzalisha barafu katika eneo la karibu na soko hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa mamalishe wengi waliokuwepo katika soko la zamani wamekosa nafasi katika soko jipya. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya ujenzi wa dharula katika jengo la mamalishe ili kuwanusuru mamalishe waweze kufanya shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Bagamoyo ina wavuvi wengi ambao wanavua bila kuwa na utaalam. Je, Serikali ina mpango gani wa kutuma watu kuja kutoa mafunzo ya ubora na dhana bora ili wavuvi wasiweze kugombana na Serikali mara nyingi katika uvuvi wao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza ni mpongeze vile vile Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo kwa kufatilia sana jambo hili na bahati nzuri katika soko analolieleza mimi binafsi nimefika na nimejionea hali halisi. Kwa hiyo, sisi kwa kushirikiana na Halmashauri yake tutazungumza na Halmashauri ili tuone namna bora ya kutekeleza huo udharura wa kuwasaidia wale mama lishe ambao walikosa nafasi katika soko la awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusu wataalam, nimhakikishie tu kwamba wataalam tunao na tutawatuma ili

waweze kupeleka elimu ya utaalam wa uvuvi kwa wananchi wake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga soko la kisasa la samaki katika Kata ya Mbweni ili wananchi waweze kujipatia kipato lakini kuiletea Serikali mapato?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Mbunge ameeleza jambo jema kuhusu soko la kisasa la uvuvi katika Kata ya Mbweni ambalo lipo katika sehemu ya mipango yetu kama Wizara, kikubwa tu sasa hivi ni kwamba tunatafuta fedha na tukishapata fedha katika maeneo yote ya kimkakati tutajenga kama ambavyo tunataka kutekeleza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 530

**Mikopo ya Wavuvi Wadogo Wadogo**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, ni utaratibu gani umewekwa wa kuwapatia mikopo wavuvi wadogo wa upande wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mahitaji makubwa ya mikopo kwa wavuvi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinakamilisha maandalizi ya mradi wa uchumi wa buluu *(Tanzania Scaling Up Sustainable Fisheries and Acquaculture Management Project – TASFAM)* utakaotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia *(World Bank)* na utawawezesha wavuvi wa Tanzania Bara na Zanzibar kupata mikopo ya masharti nafuu kupitia taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika juhudi za kusaidia wavuvi wadogo, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi Bahari Kuu *(DSFA)* ina programu za kuwawezesha wavuvi wadogo upande wa Zanzibar kwa kuwapatia mafunzo ya uvuvi wa kisasa pamoja na fursa za upatikanaji wa mikopo ya zana bora za uvuvi kutoka Taasisi mbalimbali za kibenki ikiwemo Benki ya Kilimo Tanzania *(TADB)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo na kuonesha jinsi gani Serikali ina wajali wavuvi. Maswali yangu mawili ya ziada ni kama ifuatavyo: -

Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya mikopo kwa wavuvi wadogo ili iende sambamba na mafunzo ya uvuvi wa kisasa?

Swali langui la pili; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha masharti ya mikopo hiyo haiwakwazi na kuwabana wavuvi wadogo? Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Angelina Adam Malembeka kwa maswali mazuri na ya msingi.

Kwanza nimwondoe shaka kwa sababu haya ni maelekezo ambayo tumepewa na Marais wetu wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dkt. Mwinyi kwamba kabla ya mikopo hiyo ni lazima sasa tuwapatie watu elimu ambayo itawasaidia kutumia kwa usahihi mikopo hiyo ambayo itatolewa, kwa hiyo jambo hilo tutalitekeleza kabla mikopo hiyo kuwafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la masharti, jambo hilo ndio la msingi ambalo sasa hivi tumekuwa tukifanya kwamba tumepunguza masharti kwa kiwango kikubwa na asilimia kubwa ya hii mikopo haina riba, ni mikopo ambayo tunawawezesha tukianza na kuwapatia utaalam wa kisasa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wadogowadogo hasa Wilaya ya Ukerewe tayari wameshaunda vikundi na taratibu zote za mikopo wameshafata. Je, ni lini Serikali itawapatia mikopo ili waweze kununua nyavu na kuvua kwa halali na kuachana na uvuvi haramu?*( Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Dada yangu Mheshimiwa Furaha Matondo kwamba sehemu ya mikopo ya awamu ya kwanza ambayo tulitoa karibu asilimia 80 ya mikopo ilienda Kanda ya Ziwa kwa maana ya Ziwa Victoria, ni kwa sababu tu waombaji ni wengi na kiwango cha mikopo

kilikuwa kidogo. Kwa hiyo sisi tutaendelea kuwazingatia kwa kadri ambavyo tunakuwa tukipokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hilo lipo katika mapango wa Serikali. Ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde, Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa majibu hayo. Waheshimiwa Wabunge tunarudi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah Mbunge wa Donge, aulize swali lake.

Na. 521

**Fedha za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kwa miaka mitano iliyopita, Tanzania ilipata kiasi gani kutoka katika Mfuko wa Fedha za Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Mataifa *(LDCF)* ?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge Wa Donge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi sasa imeweza kutekeleza miradi minne ambayo inatekelezwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Fedha tulizo pokea ndani ya miaka mitano kutoka Mfuko wa Nchi Zinazoendelea *(Least Development Countries Climate Fund-LDCF)* ni Kiasi cha Dola za Marekani Milioni 19,343,743.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za miradi yote minne kwa kina inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais *www.vpo.go.tz.*

Aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kutafuta fedha zaidi kutoka kwenye Mfuko wa *LDCF* ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kadri fursa zinapopatikana kwa pande mbili za Muungano wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba moja, kwa kuwa *NEMC* ndiyo taasisi pekee Tanzania ambayo ina uwezo wa kuomba fedha kupitia huu mfuko wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Je, Serikali inashirikishaje taasisi nyingine pamoja na *NGO* katika kuwajengea uwezo ili waweze kuomba fedha na kuzipata kwa haraka?

Swali namba mbili; Je, kwa kuwa Zanzibar fedha hizi pia zinatumika. Je, Serikali haioni haja ya kusaini *memorandum of understanding* na taasisi moja Zanzibar kama vile *ZEMA* ili kuweza kuimarisha uratibu na kuwajengea uwezo Wazanzibar ili fedha hizo ziweze kutumika kwa ufanisi zaidi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano Mazingira hasa kupitia Baraza la *NEMC* tunao utaratibu wa kutoa uelewa kwa wale ambao wanakuja kuandika miradi na kuileta kwetu, zaidi wale ambao watakuja na miradi endapo miradi hiyo itakuwa haijakamilika taarifa zake, hapo ndipo tunawaita na kuwapa uelewa na kuwafahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kama kutakuwa na taasisi inataka kuandika miradi na hasa inataka kuleta kwetu basi tupo tayari kwenda kuwapa uelewa ili lengo na madhumuni wawe na ujuzi na

utaalam mzuri wa kuandika miradi ambayo itakwenda kusaidia kutatua changamoto za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar tunao ushirikiano na usimamizi mzuri sana wa fedha za miradi na ndiyo maana miradi mingi haijakwama na inaendelea vizuri kwa upande wa Zanzibar na upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendeleza ushirikiano huo ili lengo na madhumuni tutatue changamoto za wananchi hasa za kimazingira na zile ambazo zina lenga katika kubaliana na mabadiliko ya tabianchi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi ambao unatekelezwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ya Unguja kwa upande wa Zanzibar, mradi huo wa *EBA* ambao umedhaminiwa kupitia Mfuko huo ambao Mheshimiwa Waziri umetamka mradi wa *EBA* lakini mradi huo utekelezaji wake ilikuwa ni 2018 mpaka 2022, ukomo wa mradi huo tayari umeshakamilika.

Je, Wizara yako ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba mradi ule ambao tayari uko kule Wilaya ya Kaskazini Unguja kwenye Vijiji vya Matemwe na Shehia ya Mbuyutende unakamilika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu swali la Mheshimiwa Usonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Watanzania kwamba azma ya Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba inatatua changamoto zote zinazokabili

wananchi hasa changamoto zinazokabili kwenye upande wa mabadiliko ya tabianchi. Azma nyingine kubwa ni kuhakikisha kwamba miradi yote iliyokwishaanzishwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, ikiwa inasimamiwa na fedha kutoka nje, tutahakikisha kwamba miradi hii inakamilika ili sasa iweze kunufaisha wananchi na wananchi waweze kunufaika na hiyo miradi na mambo mengine yaende. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mifuko hii ambayo inatenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi iko mingi na Mheshimiwa Rais aliposhiriki mkutano kule Scotland aliwasisitiza Mataifa makubwa waheshimu ahadi zao na kutenga hizo fedha. Tatizo na changamoto imekuwepo katika kukosa utaalam.

Je, Wizara iko tayari kuvishirikisha Vyuo Vikuu, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SUA* na Chuo Kikuu cha Zanzibar katika kupata ule utaalam wa kuandika hayo maandiko ili tupate hizo fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miradi mingi tumekuwa tunawashirikisha wataalam hasa wataalam kutoka Vyuo Vikuu. Tumekuwa na miradi mingi na miradi hii mara nyingi kwenye masuala ya utafiti tunawashirikisha wanafunzi na walimu wa vyuo vikuu, hata kwenye masuala ya maandiko ya hii miradi kwa maana ya hizo *proposal* pia huwa tunawapa nafasi ya kuchukua mawazo yao ili lengo na madhumuni tuweze kupata mawazo ya kitaalam kwenye miradi hii, kwa sababu wenzetu wanapokuja kukagua miradi hii huwa zaidi wanaangalia utaalam ambao tumeutumia na zile *pocedure* ambazo tumezipitia katika kuimarisha miradi hii. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari na kwa sababu tumeshaanza hilo jambo. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini, aulize swali lake.

Na. 522

**Hitaji la minara ya simu maeneo ya Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, ni lini minara ya simu itajengwa maeneo ya Endahagichang, Tumati Juu, Qalodaginwe, Aidurdagawa, Qamtananat na Migwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Endahagichang imeingizwa katika mpango wa kufikisha huduma ya mawasiliano kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali, ambapo vijiji vitakavyonufaika ni Endadubu, Miqaw na Endahagichan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya tathmini katika maeneo mapya yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge ambayo ni Tumati Juu, Qalodaginwe, Aidurdagawa, Qamtananat na Miqaw ili kubaini changamoto za huduma za mawasiliano zilizopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri naomba niweke kumbukumbu sawa ya majina haya. Miqaw, Aidurdagawa, Qamtananat, Endahagichan.

Swali langu la nyongeza, Je, ni lini sasa minara hii unakwenda kuijenga hasa vijiji nilivyotaja na Endahagichan?

Swali la pili, kwa kuwa umefika Jimbo la Mbulu Vijijini na wewe mwenyewe umeona kabisa. Ninaimani hakuna sababu ya kufanya tathmini kwa kuwa umefika mwenyewe na minara haipo katika vijiji nilivyovitaja na iko mbalimbali. Je, ni lini sasa unaweka kwenye mpango huu unaokuja ili vijiji hivi vikapata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei ameweka sawa lakini siyo rahisi kila mtu kutamka hivyo kwa hiyo Mheshimiwa Waziri endelea kujibu.*(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na namna ambavyo amesahihisha majina namna anavyoyatamka lakini pia nakubaliana na hali halisi ya changamoto ya mawasiliano katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara na Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake na tulipita meneo mengi. Maeneo mengi yalikuwa na changamoto ya mawasiliano lakini ukubwa wa tatizo tumeupunguza. Mheshimiwa Rais amekubali kutoa fedha kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano katika Kata zifuatazo:-

Kata ya Endahagichan yenyewe ambapo tumepata mtoa huduma wa Airtel pia kuna Kata ya Eshkesh ambayo pia tumepata Artel, kuna Kata ya Geterer ambayo imepata Tigo, kuna Kata ya Masqaroda wamepata *TTCL*, Kata za Yaeda Ampa na Yaeda Chini wote wamepata Halotel na *TTCL*. Kwa hiyo,

tunaendelea kupunguza ukubwa wa tatizo la changamoto ya mawasiliano ndani ya Jimbo la Mbulu Vijijini. Hivyo tunaamini kwamba awamu ijayo vijiji ambavyo tumesema tutavifanyia tathmini vitakapokamilika tutafikisha huduma ya mawasiliano. Ahsante.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Jimbo langu la Manyoni Mgharibi Halmashauri ya Itigi kuna vijiji vya Mhanga, Tulieni, Mnazi na Vijiji Itagata na Vijiji vya Lulanga havina mawasiliano kabisa. Je, Serikali iko tayari sasa kuingiza katika mpango ujao wa bajeti vijiji hivi navyo vipate huduma ya minara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira kuu ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inafikisha huduma ya mawasiliano. Kwa sababu ameiomba Serikali kama iko tayari, Serikali tuko tayari kuhakikisha kwamba tunaingiza katika mpango ujao wa kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya mawasiliano, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Mathayo David.

**MHE. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Same Magharibi, Kata za Milimani kuna shida sana ya mitandao. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kuziangalia Kata hizo za milimani vilevile, ziletewe huduma ya simu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Same Mashariki pamoja na Magharibi nilifanya ziara katika maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Ni kweli kuna changamoto lakini habari njema kwa wananchi wa Same ni kwamba, Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika Kata zaidi ya 12 katika Wilaya nzima ya Same. Kwa hiyo, naamini kwamba katika maeneo ambayo yatakuwa bado yana changamoto tutatuma wataalam wetu waende wakajiridhishe. Kama tutahitaji kuongeza nguvu ya minara iliyopo tutafanya hivyo, kama tutahitaji kuweka minara mipya basi tutafanya hivyo, lengo likiwa ni kutatua changamoto ya mawasiliano kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Shamsia na Mheshimiwa Nashon.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Je, ni lini Serikali itatupatia minara ya mawasiliano katika Kata ya Tangazo na Kijiji cha Namgogori hakuna kabisa mnara wa mawasiliano ili wananchi wangu waweze kufurahia huduma hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, maeneo ambayo ameyataja baada ya Bunge lako Tukufu tukutane ili tuweze kuyaweka vizuri na tutume wataalam wetu wakafanye kazi na baada ya hapo tuhakikishe kwamba tunafikisha huduma ya mawailiano, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon, nilikutaja.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba na mimi niulize swali. Ni lini mawasiliano yatafika Ilolanguru, Chagu, Songambele, Ubanda na Mumbala? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa bado tuna changamoto baadhi ya maeneo katika nchi yetu lakini tunakwenda awamu kwa awamu. Tunapeleka minara 758 vilevile tumefanya tathmini ya vijiji 2116, baada ya hapo tunapeleka minara 600 na baada ya hapo tutapeleka minara 1000. Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge aniletee maeneo hayo kwa maandishi ili niyaweke katika mpango wa utekelezaji wa awamu inayokuja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kila Mbunge anayesimama anaomba minara na maeneo mengi hata Mjini mtandao unasumbua. Ni upi mkakati wa Serikali kutumia *satellite* ili kuondokana na changamoto hii ya mawasiliano ambayo hata maeneo ya Mijini yenye mabonde na miteremko kumekuwa na vurugu sana za kukosekana kwa mawasiliano. Ni upi mkakati wa Serikali wa kutumia *satellite* ili mawasiliano yapatikane nchi nzima?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikakati mingi. Serikali iliingia kwenye utatatibu wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa ili tuondokane na matumizi ya *microwave* ambayo ilikuwa na changamoto kubwa sana, ni ya gharama lakini kulingana na jiografia ya nchi yetu ilivyo ilileta changamoto kubwa. Vilevile, kuna maeneo ambayo tunatumia *satellite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa maelekezo mahsusi ili tuanze mchakato wa kupata *satellite* yetu kama nchi. Tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetatua chanagamoto nyingi sana za mawasiliano ambayo ni mchango mkubwa sana katika uchumi wa sasa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaji–*engage* na kila teknolojia inayoibukia ili kuhakikisha kwamba kwanza kabisa tuwe na teknolojia rahisi na inayoweza kwenda kutatua matatizo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mara nyingine unakuta kuna mnara hapa lakini sehemu ya pili mawasiliano hauwezi ukapata, kunakuwa na *dark sports* za kutosha. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tumejipanga na tunaendelea na uchambuzi wa kina kuangalia ni teknolojia ipi ambayo itakuja kutupa majibu sahihi kwa ajili ya kutatua changamoto ya mawasiliano kwa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Andrea Mathew Kundo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 523

**Huduma za afya na dawa katika zahanati na vituo vya afya**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza huduma za afya na dawa zinazotolewa na Bima katika zahanati na vituo vya afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuongeza huduma za afya na dawa zinazotolewa na bima katika Zahanati na Vituo vya Afya imefanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza idadi ya dawa, vifaa na vifaa tiba ngazi ya zahanati kutoka aina 254 mwaka 2015 hadi kufikia aina 451 mwaka 2023.

(ii) Kuongeza idadi ya dawa, vifaa na vifaa tiba ngazi ya kituo cha afya kutoka aina 414 mwaka 2015 hadi kufikia aina 828 mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa zilizoongezeka zipo katika miongozo ya Serikali na hivyo zinalipiwa na Bima ya Afya kwa wanufaika wa mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongeza dawa Serikali imeboresha miundombinu, uwepo wa vifaatiba, huduma za maabara pamoja na rasilimali watu. Hata hivyo, Serikali inatambua kwamba kuna maeneo ya nchi ambayo uboreshaji huu haujafikia, hivyo ipo katika mikakati wa kuyafikia maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Kwa kuwa, Serikali imeshaongeza vifaatiba na dawa kwa zaidi ya asilimia 100 kwenye Zahanati na Vituo vya afya. Ni lini sasa watatoa hadhi kwenye vituo hivyo ili viweze kutoa huduma zote za Bima ya Afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali inatambua kwamba yapo maeneo ambayo bado huduma hizi hazijafika na amesema ipo mikakati ya Serikali kwa ajili ya kufikisha huduma hizo. Ningependa kujua sasa ni ipi mikakati hiyo ya Serikali ili kuhakikisha kwamba Watumishi kwa maana ya rasilimaliwatu wanaongezeka, vifaatiba pamoja na miundombinu inaimarika? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake ambalo ni *strategic* kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. Swali lake la kwanza kwamba ni lini vituo hivyo vitapewa vibali vya kusajili? Mheshimiwa Mbunge ni kwamba vituo vyote, zahanati, vituo vya afya ambavyo vimesajiliwa ni kwamba Bima wanatakiwa wawaruhusu pia kutumia dawa hizi ambazo ziko kwenye mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge kama kuna zahanati au kituo cha afya chochote ambacho hakijasajiliwa nawaagiza Bima ya Afya wapitie nchi nzima wahakikishe vituo vyote ambavyo vimetimiza hivi vigezo basi viwe vimesajiliwa na kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu kufikiwa vituo vingine. Moja, tunajua mwaka huu vifaa vingi sana vimenunuliwa na viko njiani vinakuja, kwa hiyo, vitasambazwa kwenye vituo vyetu lakini kwenye bajeti ya mwaka huu tunakwena ku–*cover* hivyo vituo na ajira zitaendelea kufanyika kila mwaka unaokuja kuhakikisha tunawafikia wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Parreso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa ya kisukari kwa wagonjwa wa sukari imekuwa ni changamoto sna kwenye vituo hivi vya afya mpakla waende Wilayani. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa ku-review utaratibu huu ili kwenye *level* za Vituo vya Afya pia waweze kupata?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo lilikuwa linaleta malalamiko mengi hasa kwenye zahanati na vituo vya afya hasa kwa wazee wetu wagonjwa wa kisukari na presha ni eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Ukiona hapa tumeongeza dawa kwa kiasi hiki ni moja wapo ya dawa hizi za sukari na presha kuhakikisha sasa hiyo shida iliyokuwepo huko nyuma haitatokea tena.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya Dkt. Godwin Mollel kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Na. 524

**Wananchi wa vijijini waliolipia umeme kwa bei ya mijini – Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapitia upya uhalisia wa malipo ya umeme kwa Vijiji vya Mkolango, Kiumba, Ikwete na Malombwe ambapo walilipia kwa bei ya Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Vijiji vya Ikwete na Mkolango, wananchi wote wa maeneo hayo wanalipia gharama ya shilingi 27,000 kwa ajili ya kuunganishiwa umeme. Aidha, Vijiji vya Malombwe na Kihumba ni miongoni mwa vijiji vyenye sura ya Vijiji-Miji ambavyo kwa tathmini ya awali, vilionekana vinastahili kulipia shilinigi 320,960 kama garama ya kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini changamoto katika tathmini ya awali, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kufanya tathmini ya maeneo yote yenye sura ya Vijiji-Miji yakiwemo maeneo ya Malombwe na Kiumba ili kuyapatia suluhisho la gharama za kuunganishiwa umeme. Serikali inaendelea kuomba wananchi wa maeneo hayo wawe na subira wakati suala hili linashughulikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo Wizara hii ndiyo Wizara pekee iliyotengewa bajeti ya zaidi ya shilingi trilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa majibu ya Serikali ni mazuri vipo baadhi ya Vijiji – Miji vinavyofanana na hivi alivyovitaja ikiwemo Ibumila na maeneo mengine. Je, Serikali iko tayari sasa kuwapatia wananchi umeme kwa bei ya vijiji kama alivyotaja vikiwepo Vikwete, Mkolango na Malombwe?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Makambako wa Kata ya Kivavi na Kata ya Majengo wameathirika kwa muda mrefu wakisubiri umeme wa upepe na kulipwa fidia zaidi ya miaka 20. Je, Serikali inawapa majibu gani wananchi hawa ili kama haiwezekani wananchi waendelee na shughuli zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kwanza la swali la Mheshimiwa Sanga, Serikali inayo nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba wananchi wanaunganishiwa umeme kwa gharama nafuu ambazo wanazimudu. Kama tulivyosema juzi kwenye bajeti yetu, tunaendelea kufanya tathmini na upembuzi yakinifu kubaini ni maeneo gani yanaweza yakawa yanakidhi gharama hizo za shilingi 27,000 pia kutafuta chanzo kizuri na cha uhakika cha kuweka ruzuku katika eneo hilo, kwa sababu ni kweli gharama za kuunganisha umeme ni kubwa. Pale ambapo tunatakiwa kuunganisha kwa shilingi 27,000 basi inabidi kuwekwa ruzuku kubwa na tunapounganisha kwa 320,000 basi tunaweka ruzuku kama nusu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Sanga na wengine wote kwamba jambo hili Serikali imeshalichukua na inalifanyia kazi tunaamini litakamilika siku chache zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili, ni kweli kwamba wananchi wa maeneo ya Makambako wameahidiwa kupewa umeme wa kutumia upepo na maeneo yao yalainishwa kwamba yatalipiwa fidia kwa muda mrefu. Tumechukua muda

mrefu kwenye mazungumzo na wale waliotaka kuwekeza ninapenda kusema kwamba tumefikia hatua ya mwisho ya mazungumzo hayo, ambapo *TANESCO* tayari wamekwishatengeneza mkataba wa makubaliano na wanaupitisha kwenye taasisi yao na baadae utakuja Wizarani ili utolewe sasa kwa ajili ya kuendelea na hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Makambako kabla ya mwezi wa Tisa shughuli zitaanza *site* kwa kulipa fidia na kuanza kutekeleza mradi utakaotuongezea umeme wa upepo kwenye gridi yetu ya Taifa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na sintofahamu sana kwa wananchi wengi wakiwepo wa Jimbo la Kibamba kubambikiwa madeni makubwa ya ununuzi wa umeme au LUKU bila kuelewa kutokana na kukosewa kwa makadirio ya awali na *TRA*. Je, Serikali mko tayari kuwaelekeza *TRA* waweke mpango mzuri ambao wananchi hawa wataweza kupunguza madeni yale kila mwezi wakiwa wanalipa LUKU zao kila mwezi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mtemvu, kwa swali lake. Juzi wakati tunapitisha bajeti jambo hili lilijitokeza na ulitolewa Mwongozo na Mheshimiwa Spika kwamba, Wizara ya Nishati pamoja na wenzetu *TRA* ambao hasa ndiyo wenye hizo pesa tukae na kuweka utaratibu mzuri. Sisi tumeshawafikishia wenzetu, tumewapelekea *concern* hiyo wanatengeza utaratibu mzuri wa kuonesha deni na mwananchi aweze kulipa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili Wizara ya Nishati kupitia *TANESCO* ni kama bomba la kupitisha mapato hayo ambayo yanatoka kwa mwananchi kupitia *TRA*. Hata hivyo, tunashirikiana na wenzetu kuweka mifumo mizuri ili wananchi wanaopata huduma ya umeme sasa wasipate adha ya kulipa kodi hii ya majengo ambayo inapitia kwetu. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi kwa pamoja Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi ni Mbunge wa Tarime Vijijini, pale Nyamwata, Kerende, Nyangoto ni vijijini kabisa. Maeneo haya yote wananchi wanalipa umeme kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, Jimbo limegawanywa kuna watu wanalipia umeme kwa bei ya chini ya shilingi 27,000 na wengine bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue ni lini mchakato huu wa kurudisha bei ya shilingi 27,000 ya umeme kwa watu wa vijijini inarudishwa ili watu wapate umeme sawa? Huu mchahakto umechukua muda mrefu.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwikwabe Waitara, kwamba ni kweli tumebaini yapo maeneo mengi ambapo tulipofanya tathmini awali tumeyaacha, wale wataalam wameelekezwa warudi tena ili wakifanya iwe ni *once and for all.* Kwa hiyo, wanapita kwenye maeneo yetu, kazi ni kubwa inahitaji weledi na utulivu mkubwa ili tuweze kuwahudumia wananchi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waitara na Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie kidogo tulikamilihse hili kwa usahihi na ufasaha kabisa. Tutakapokuja kuleta mbele yenu liwe ni tatizo ambalo tumelikamilishwa tuende kwenye hatua nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka nilikutaja na Mheshimiwa Dorothy ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Liwale unaoundwa na Kata tatu, Kata ya Likongole, Liwale Mjini na Nangando vipo vijiji zaidi ya kumi lakini vijiji vile vimegawanya, kuna vijiji vinalipa shilingi 27000 na kuna vinavyotakiwa kulipa shilingi 350,000. Je, Serikali haioni kwamba kwa sababu vyote hivi ni vijiji viingizwe kwenye kulipa shilingi 27000 ili kuweka usawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nifafanue kidogo jibu ni lilelile lakini niliongezee nyama kidogo.

Mheshimiwa wenyekiti, Wizara ya Nishati kupitia *TANESCO* tulibaini maeneo ya Vijiji na Miji kutoka kwenye taarifa za wenzetu wa TAMISEMI ndiyo waliotupatia taarifa za hapa ni mjini na hapa ni kijijini. Baada ya ku– *implement* hicho tulichokipata ndiyo yakatokea maoni mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi. Tukaona ni vema tuende *site* wenyewe ili tukabaini, pamoja na kwamba enzetu wa TAMISEMI wamesema hapa ni mjini lakini maisha ya pale yanaonesha kuwa ni kijijini na hilo ndilo zoezi tunalolifanya na tukilikamilisha tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili kuweka usawa kama ulivyoshauri Mheshimiwa Kuchauka ili wananchi waweze kulipa ile gharama ambayo wanaweza kuilipa kutokana na mapenzi na utashi mwema wa Serikali kuhakikisha kwamba inawahudumia wananchi wake salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy nilikuona na Mheshimiwa Matiko atamalizia.*(Makofi)*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nina swali moja.

Je, Serikali hamuoni umuhimu wa kumaliza utengenezaji wa umeme katika Jimbo la Temeke hasa Jimbo la Mjini, ukizingatia kuna wakati umeme unakatika kwenye viwanja hasa katika mechi hizi za Kimataifa, ni lini sasa mtarekebisha umeme huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Dorothy Kilave ni la msingi kabisa. Tunayo nia ya dhati kama Serikali kumaliza tatizo la kukatika umeme Tanzania nzima. Tunashukuru kwamba juzi mmepitisha bajeti ya Wizara ya Nishati yenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha tunaondokana na tatizo hili. Tuwahakikishie litakwisha kupitia mradi wetu wa gridi imara tutaendelea kuimarisha maeneo mengi ambayo yana changamoto kubwa ya ukatikaji wa umeme ikiwemo Jimbo la Temeke. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwepo na kukatwa kwa kodi za majengo kwa wale ambao hawastahilin kukwatwa kwa mfano, wazee na zile nyumba za tembe. Sasa, ninataka kujua ni lini Serikali itafanya *reconciliation* ili iweze kuwarudishia gharama zote ambazo wamekatwa hawa ambao hawastahili kukatwa kodi hizi za majengo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema na kama tulivyosema kwenye *budget speech* ya juzi, wenzetu wa Wizara ya Fedha wameshalichukua nasi tulichowa-*supply* ni namba za LUKU kwa ajili ya wao kuwa-*identified* nani anastahili kulipa kiasi gani na kwa wakati gani na kwa utaratibu gani. Tunashirikiana nao wenzetu ili waweze kuweka utaratibu mzuri ambao utahakikisha yule anayetakiwa kulipa kweli ndiye anayelipa kama tulivyosema juzi kiwanja kimoja kinaweza kuwa kina vyumba vitano, sita halafu kila mmoja analipa wakati hakutakiwa kulipa kilo mmoja, lakini tunafahamu

pia sheria nyingi zinaeleza kwamba wale wazee wa miaka 60 na zaidi wawe-*exempted* kwenye hayo maeneo na wastaafu wengine tumeshawasiliana na wenzetu na tunalifanyia kazi naamini wenzetu wa Wizara ya Fedha watakamilisha na tutafikia sehemu nzuri.

**MWENYEKTI:** Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa na Mheshimiwa Tunza Malapo kwa niaba yake.

Na. 525

**Vijiji vyote kupata umeme wa *REA* – Songwe**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Vijiji vyote vya Mkoa wa Songwe vinapatiwa umeme wa *REA*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe una jumla ya vijiji 307 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Mei 2023, vijiji 240 vilikua tayari vimepatiwa umeme, Vijiji 67 vilivyosalia viko kwenye mkataba wa Mkandarasi *M/s Derm Electrics Ltd* anayetekeleza mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu III Mzunguko wa II katika Mkoa wa Songwe. Kazi za ujenzi wa miundombinu na kuunganisha wateja katika vijiji hivyo inaendelea na mradi unatarajiwa kukamilika Desemba, 2023, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ilivyo Mkoa wa Songwe pia katika Mkoa wa Mtwara kuna vijiji 102 bado havijapatiwa umeme. Nataka kujua Serikali ni lini itavipatia vijiji hivyo umeme?

Swali la pili, kwa kuwa umesema mnafanya mchakato wa kutambua Kata ambazo zina hadhi ya Miji lakini ni Vijiji. Nataka kujua ni lini mchakato huo utakamilika ili watu wapate huduma kwa sababu hata katika Jimbo la Mtwara Mjini kuna baadhi ya Kata mfano Kata ya Naliendele, Kata ya Jangwani na zingine zinaonekana ziko Mjini lakini maisha ya watu wake ni kama wako vijijini, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyosema kama ilivyosomwa lakini na Mtwara pia tunao Wakandarasi wawili, wanafanya kazi katika Mkoa wetu wa Mtwara na juzi tulikaa kikao na Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara tukajadiliana kwa upana namna ya kumaliza haraka kazi hizo, tunaamini kwa mkakati tuliouweka kabla ya Desemba mwaka huu kazi yetu ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Mkoa wa Mtwara itakuwa imekamilika na hilo tunauhakika nalo na tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwa kutupitishia bajeti juzi tutaendelea kusimamiana na wenzetu ili kazi hii iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni lini tutamaliza kazi hii, tunatamani hata tuimalize leo lakini kwa sababu ya kutaka kufanya ushirikishwaji mkubwa na kubaini changamoto za maeneo mbalimbali tunaomba mtuongezee muda kidogo halafu baadae tutakuja kusema ni lini tutamaliza ili tuweze kukamilisha hii kazi kwa Pamoja, tusingependa kuikimbiza harafu ikawa kama ya awali ambayo haikuleta majibu tuliyokuwa tunayatarajia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay Mheshimiwa Mwita Getere na kule nyuma maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naishukuru Serikali kwa kuwa tayari Mkandarasi wa *REA* katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ameshasimika nguzo

kwenye vijiji vyote yapata miezi minne. Je, ni lini sasa wananchi wale wa Vijiji vya Mbulu Mjini watapewa umeme kwa kuunganishiwa nyaya na kuunganishiwa umeme kwenye makazi yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema miradi yote ya *REA three round two* itakamilika kufikia Desemba mwaka 2023 lakini kwa nyakati tofauti tofauti vijiji mbalimbali vitaendelea kuwashiwa umeme. Kama alivyosema Mheshimiwa Issaay hayo maeneo ambayo tayari wameshasimika nguzo tunatarajia kwenye mwezi mmoja mpaka miwili tayari kazi itakamilika wakati maeneo mengine tunaendelea kuchimba, kusimika nguzo na kuunganisha umeme, lakini ifikapo Desemba kazi yote itakuwa imekamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, Mheshimiwa Masaburi nilimtaja

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Vijiji 33 vya Bunda vilipewa umeme kilomita tatu kwa kila kijiji na sasa Mkandarasi amepeleka kilomita moja kwa kila kijiji. Ni lini kilometa mbili zitaongzwa katika vijiji 33 vya Jimbo la Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Wabunge wa Mkoa wa Mara kwamba katika zile *lot* ambazo Wakandarasi wao tayari wamekamilisha *original scope* kwa asilimia 100 na Mkandarasi wa Mkoa wa Mara tayari naye yumo katika orodha ile, kwa hiyo tuendelee kusukuma kwa pamoja ili tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia mwishoni mwa wiki hii wanzetu wa *REA* watasaini mikataba na wale ambao wamepata

nafasi ya kuongeza hizo kilomita mbili ambazo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa bilioni 351 kwa ajili ya kuongeza kilomita mbili kwa kila Kijiji. Tunatarajia wiki hii zitasainiwa na hivyo mwanzoni mwa mwezi unaokuja kazi za kusimika nguzo na kuvuta waya utaanza katika maeneo hayo ambayo nyongeza ya kilomita mbili inaenda kufanyika.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Masaburi

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni dogo. Je ni lini mradi wa kilomita mbili za nyongeza katika mradi wa *REA III round two* utaanza kutekelezwa katika Mkoa mzima wa Mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Getere nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masaburi kwamba tunatarajia Ijumaa ya wiki hii wenzetu wa *REA* watakaa na wakandarasi. Tayari wameshapewa idhini ya kuendelea na maeneo hayo ya kutekeleza kilomita mbili na wakishasaini mikataba mwishoni mwa wiki hii tunatarajia mwanzoni mwa mwezi unaokuja kazi itaanza na kwa kuwa ni kazi ndogo tunatarajia itakamilika pamoja na kazi kubwa mwezi Desemba mwaka huu kwa sababu ni kupeleka line ndogo za kuwasha umeme katika vijiji vyote ambavyo vilikuwa katika *REA III round two* kwa maana ya kuongeza kilomita mbili kwa kila kitongoji. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Majengo, ramani ya umeme imepeleka umeme kwenye kitongoji cha Nshepa badala ya makao makuu ya Kijiji. Je Serikali iko tayari kutoa maelekezo katika vile vitongoji 15, makao makuu ya Kijiji cha Majengo yapelekewe umeme mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitongoji 15 ambavyo tumepata pesa jumla ya shilingi bilioni 357 kwa ajili ya kuongeza vitongoji 15 kwa kila Jimbo, tulisema juzi katika bajeti na nirudie tena, litakuwa ni chaguo la Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kuchagua ni wapi hivyo vitongoji 15 apelekewe. Kwa sababu kama anavosema Mheshimiwa Aweso kwamba anayelala na mgonjwa ndiye anajua mihemo yake, tunaamini Waheshimiwa Wabunge mnatambua zaidi mahitaji yako wapi kutuzidi sisi. Kwa hiyo, tuyashirikishana pamoja na ninyi kujua na kutambua ni maeneo gani ya vitongoji viwe vya kipaumbele wakati tukiwa tunaelekea kupata pesa nyingi ili kumaliza vile vitongoji 36,101 ambavyo bado havijapatiwa umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali fupi la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi mingi ya *REA* katika baadhi ya vijiji hawa Wakandarasi wamekuwa hawawalipi vibarua na kuna malalamiko mengi. Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha hawa Wakandarasi wanawalipa wale vibarua ambao wanafanya kazi hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mwakasaka, tumekuwa na changamoto hiyo ya Wakandarasi ama kuchelewa sana au kutolipa kabisa malipo ya vibarua wanaofanya nao kazi. Tumelichukulia hatua kwa kuwa tunawasiliana na wale watumishi wa hao Wakandarasi na kuwashauri wanapokuwa wanaingia katika e*ngagement* hizi watengeneze vikundi na wawasiliane na

Ofisi zetu za Serikali zilizopo kwenye maeneo husika ili changamoto inapotokea tuibaini mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Tabora tumeendelea kushughulikia matatizo hayo nasi ofisini tumeshapata watu mara kadhaa ambao wamekuja na tumewapeleka *REA* pesa yao imeweza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yetu yote wale wote wanaofanya kazi ujira wao halali utalipwa kwa sababu Serikali inamlipa Mkandarasi na Mkandarasi lazima alipe kwa wale vibarua ambao amefanya nao kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Byabato ,Naibu Waziri Wizara ya Nishati kwa majibu haya ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo Mbunge wa Bahi, aulize swali lake

Na. 526

**Kufufua Skimu ya Umwagiliaji Mtitaa - Wilaya ya Bahi**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Mtitaa Wilayani Bahi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji Mtitaa iliyopo katika Kijiji cha Mtitaa, Kata ya Mtitaa Wilayani Bahi, ilijengwa kupitia Mpango Shirikishi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji *(PIDP)* katika mwaka wa fedha 2002/2003 na kuanza uzalishaji mwaka 2003/2004. Skimu hii pia ina miundombinu ya bwawa

dogo la kuvuna maji msimu wa mvua na zao linalolimwa ni Mpunga. Skimu ina jumla ya hekta 107 na ina jumla ya wakulima 215.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha za ukarabati wa skimu za Bonde la Bahi ikiwemo skimu ya Mtitaa ambazo zimeharibiwa na mafuriko ili kuzirudisha kwenye uzalishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Chikopelo linategemewa na Kata za Chali na Kata ya Nondwa. Bwawa hili limekuwa na uwezo wa kutunza maji msimu wote, hata hivyo lina changamoto ya kupungua kwa kina kutokana na kujaa kwa matope.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati bwawa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine dogo ni kwamba Kilimo cha Zabibu ni kilimo kinachotegemewa hapa Mkoa wa Dodoma hata hivyo kilimo hiki bado kinategemea kwa kiasi kikubwa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu ili tuanze kupata umwagiliaji kwa ajili ya kilimo na kupata tija? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu Bwawa la Chikopelo. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kiambatisho namba 13 tumelitamka Bwawa la Chikopelo kati ya

mabwawa ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi mwaka ujao wa fedha. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Kata za Nondwa alizozitaja na maeneo ya jirani kuwa bwawa hili linakwenda kufanya kazi na wananchi watanufaika kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu zabibu, tunatambua kwamba Dodoma ni kati ya eneo ambalo lina uzalishaji mkubwa sana wa zabibu hapa Tanzania na hivyo kuna umuhimu pia wa kuunganisha zao hili na kilimo cha umwagiliaji. Kwa kuanzia tunao tayari mfumo wa umwagiliaji katika eneo letu la Chinangali ambapo tunalo shamba kubwa la umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha zabibu. Sambamba na hilo hata hili Bwawa la Chikopelo pia na lenyewe tutaangalia ikolojia yake kama ita-*support* kilimo cha zabibu pia tutaunganisha mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwamba tumetamka hapa tunakwenda kuchimba visima 150 kila Halmashauri nchi nzima hivyo wakulima wa bahi pia watanufaika na visima hivi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji cha zabibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mheshimiwa Sylivia Sigula.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mii swali la nyongeza. Je, Serikali imefikia wapi kwenye ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Wilayani Mbarali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa na miradi ya umwagiliaji katika Wilaya ya Mbarali na ninavyozungumza hivi sasa Wakandarasi wapo *site* katika mradi wa Msesule, Isenyela, Matebete, Hemanichosi na Gwanakubagogolo kote huko tayari wakandarasi wako site na kazi inaendea. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba kazi inaendelea na wananchi watanufaika na kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylivia.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa iliyobarikiwa kuwa na vyanzo vikubwa vya maji lakini bado suala la umwagiliaji halijapewa kipaumbele. Nataka kujua, wananchi wa Kasulu, Buhigwe na Uvinza ni lini watanufaika na miradi hii ya umwagiliaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yetu ya bajeti kiambatisho namba tano tumeyatamka mabonde 22 ambayo tunakwenda kuyafanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya umwagiliaji. Bonde mojawapo ni Bonde la Mto Malagarasi ambalo lina hekta 7000 na litahudumia eneo la Buhigwe, Kasulu pamoja na Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika eneo la Kasulu tuna miradi miwili pale ambayo tunaifanyia kazi katika mwaka ujao wa fedha mradi wa Ahsante Nyerere na Kilimo Kwanza ambayo ina jumla ya hekta 3,500 ipo ndani ya mpango itafanyiwa kazi na wakulima wa Kigoma watafanya kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuwapatia skimu ya umwagiliaji watu wa Mkinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba lazima tufanye kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuleta tija kwenye kilimo.

Katika eneo la Mkinga pamoja na Lushoto tumeanza kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la Mto Umba ambalo lina hekta zaidi ya 5,560 na tunaamini kabisa kwamba wananchi wa eneo la Mkinga watanufaika na mradi huu mkubwa ambao unakuja kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Anthony Mavunde tunamalizia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba aulize swali lake.

Na. 527

**Kutoa Ithibati kwa pombe zilizokidhi viwango**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa ithibati kwa baadhi ya pombe za kienyeji ambazo zimekidhi viwango?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mwezi Oktoba, 2022 jumla ya leseni 43 za ubora zimetolewa kwa bidhaa mbalimbali za pombe za kienyeji zilizokidhi viwango na maombi mengine mapya 22 yapo kwenye hatua mbalimbali za tathmini kuelekea kwenye kupata ithibati ya ubora. Aidha, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania itaendelea kutengeneza viwango vya pombe za kienyeji kwa kadri ya mahitaji yatakavyojitokeza, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka kumweleza Mheshimiwa Waziri kwamba suala la pombe za kienyeji ni kwa lengo la kulinda viwanda vyetu vya ndani pia kulinda ubunifu wa watu wetu, kuongeza ajira na kuongeza uchumi kwa ajili ya kulinda mawazo ambayo yamezalishwa na wananchi wetu. Naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nimechangia hoja yangu ni mwezi umepita sasa. Je, ni upi mkakati wa Serikali kwa mwezi huu mmoja mmeshaanza kuzipatia leseni zile pombe ambazo mmezikataza kutumika kwenye jamii, mfano gongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Je, kwa nini Serikali isiongeze kodi kwenye pombe zote ambazo zinaingizwa kutoka nje mithili hiyo ya *spirit* na pombe zingine ili kuzipa thamani pombe zetu za ndani na kuwavutia wawekezaji wote waje wawekeze kwenye pombe zetu za ndani ili tulinde soko letu la ndani na mawazo ambayo yametokana na watu wetu wa ndani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli tunajua mchango mkubwa sana wa sekta hii ya pombe na hasa pombe za kienyeji ambazo akina mama wengi ndiyo wanashiriki huku kama wajasiriamali kutengeneza pombe hizi za kienyeji na ndiyo zimekuwa nguzo na msingi mkubwa kulea familia katika kaya nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati madhubuti na ndiyo maana nimesema tumeshaweka mikakati mojawapo ni kuona namna gani tunawasaidia kuwafundisha na kuwawekea teknolojia sahihi ili waweze kuzalisha pombe za kienyeji zinazokidhi viwango na ambavyo vitakuwa havina madhara kwa wanywaji. Kupitia *TBS* kwa maana ya shirika la viwango na *SIDO* tumeshaweka fedha katika bajeti ambayo itatumika kama ruzuku kuwafundisha, kuwafuata kwanza wazalishaji wa pombe hizi za kienyeji kule waliko vijijini lakini kuwafundisha namna ya kuzalisha

pombe ambazo zinakidhi viwango ili ziweze kuendelea kutumika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zile pombe ambazo zilikuwa na madhara ambazo ndiyo wanasema zimepigwa marufuku tunataka tuwasaidie ili athari ile isijitokeze na baada ya hapo zitaruhusiwa kuendelea na kupewa ithibati ya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali inafanya juhudi mbalimbali na hili ni dhahiri kwamba katika kuhakikisha tunafungua uchumi wa nchi yetu ni pmoja na kuruhusu biashara huru kulingana na taratibu na kanuni zilizopo, kwa maana ya kurusu pia bidhaa kutoka nje ya nchi kama vile ambavyo sisi tunauza nje ya nchi bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu. Kwa hiyo, tunaendelea kuweka mkakati madhubuti kulinda viwanda vya ndani pale ambapo tutaona kwamba vinatakiwa kufanya hivyo na tumeshaanza kufanya na katika sekta hii ya pombe pia tutafanya hivyo ili kuwasaidia wananchi kunyanyua kipato lakini kuinua uchumi wa nchi yetu. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba nimekuona umesimama Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Nilitaka tu nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelipokea wazo lake la kuongeza kodi kwenye pombe na tutakamilisha kufanyia kazi na tutatoa majibu tutakapokuwa tunatoa kauli ya Serikali kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ahsante sana pia Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Naibu Waziri, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa maswali yetu kwa siku ya leo na sasa ni wakati wa matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tunao wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 101 wa Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Kisarawe, wakiongozwa na Mwenyeketi wa CCM, Wilaya ya Kisarawe, Ndugu Halfani Sika, pia yupo Ndugu Zainab Matitu Vullu, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Pwani, karibuni sana wapiga kura wetu wa Halmashauri ya CCM, Kisarawe, pamoja na hawa ambao wameongoza, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri Kilimo ambao ni viongozi wa CCM Kata ya Mnadani kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wangu hapa, Maafisa kutoka Jumuiya ya Wazazi Makao Makuu na UVCCM Makao Makuu, naomba wasimame wote, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 36 wa Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara kutoka Tarime Mjini Ndugu Kichichi Marwa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni kumi wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni Wajumbe Kamati ya Siasa Wilaya kutoka Liwale Mkoa wa Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni familia yake kutoka Tarime Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Tecla Ungele ambae ni Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Nachingwea, Ndugu Rashidi Ally Likondo, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo nao ni wanafunzi 100 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi Notra Dame ya Jijini Arusha, karibu sana wanafunzi wetu katika Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 33 na Wahadhiri watano kutoka Chuo cha Bibilia cha Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa kuna semina ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 pamoja na sensa ya majengo ilikuwa ifanyike leo siku ya Jumatatu hata hivyo kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo sasa itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana.

Kwa hiyo, badala ya tarehe 5 Juni ina maana itakuwa tarehe 12 Juni, 2023.

Waheshimiwa Wabunge pia tunalo tangazo lingine kwamba Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na wadau wake wameandaa maonesho ambayo yanaendelea kwa sasa katika viwanja vya Bunge, maonesho hayo yanahusu huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na sekta mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Pamoja na maonesho hayo kila Mbunge atapata Kamusi moja ya Kiswahili pamoja na mipira miwili ya soka ili kuhamasisha michezo kwenye maeneo yao, Wabunge wote mnakaribiswa. *(Makofi)*

Pia tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa matokeo ya mechi iliyofanyika siku ya Jumamosi Tarehe 03 Juni, 2023 kati ya timu ya *Bunge Sports Club* na timu ya *Mwanza Veteran* kutoka Mkoani Mwanza ni kama ifuatavyo:-

Timu ya *Bunge Sports Club* ya mpira wa miguu ilipata magoli mawili na timu ya *Mwanza Veteran* ilipata magoli matano. Wafungaji wa magoli kwa upande wa Bunge ni Mheshimiwa

Cosato David Chumi na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan.

Aidha, kwa upande wa michezo ya mpira wa pete timu ya *Bunge Sports Club* ilipata magoli 39 na timu ya *Mwanza Veteran* ilipata magoli 21. Katika mchezo huu kinara wa magoli alikuwa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Tutaanza na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kusimama hapa na kuchangia katika Wizara hii. Nashukuru sana Wizara kwa kufanya maboresho makubwa katika bustani ya wanyamapori iliyopo pale Tabora Mjini. Wamefanya maboresho makubwa pale wameongeza wanyama wa aina mbalimbali, sasa hivi kuna simba, kuna chui, kuna pundamilia, kuna fisi kuna nyani na kuna ndege wa aina mbalimbali wakiwepo aina ya tausi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Tabora tunashukuru kwa sababu lile eneo lilikuwa ni pori, pori kabisa na ni eneo la Mjini karibia na Hospitali ya Kitete. Kwa hiyo, walivyoweka ile bustani kwa upande wetu sisi kwanza kabisa tumeshapata maeneo ya utalii. Sasa hivi Tabora imefunguka barabara za lami ni nyingi, hata sasa wanaokwenda Mwanza, wanaokwenda Kigoma, wanaokwenda Shinyanga wanaokwenda Kahama lazima wapitie Tabora ndiyo waweze kufika kwenye maeneo yao kutokana na barabara kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tu tunaendelea kuwakaribisha sana watu wote wa Tanzania wanaopita katika Mkoa wetu wa Tabora. Sasa hivi tuna bustani nzuri ambayo kuna wanyama wa kila aina tunatangaza utalii wetu wa Tanzania. Niwashukuru sana *TAWA* lakini naomba kuishauri Serikali endeleeni kuboresha eneo lile hasa kwenye masuala ya miundombinu ili kuweza kuongeza vivutio pia kuongeza watu ambao wanaweza wakaja pale kwa sababu watavutika na mambo mengi ambayo yatakuwa pale. Naamini bado lakini mtakuwa kwenye *process* hivyo naomba sana Serikali iweze kuongeza ili tuweze kuwa na vivutio vizuri katika Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusiana na maslahi ya watumishi. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, Serikali mmeunda Jeshi Usu, Jeshi hili linafanya kazi kwenye taasisi mbalimbali za Wizara hii, lakini wote wanafanya kazi ya aina moja. Changamoto iliyopo na ambayo mimi niliiona na mpaka sasa naomba niiseme ni utofauti wa mishahara kwa watumishi hawa. Haiwezekani hawa mnawapa hiki, hawa mnawapa hiki wakati wote wanafanya kazi ya aina moja. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ili kuondoa huu mkanganyiko, ili kuondoa kuombwa kuhama hama kwa hawa wafanyakazi, kwa sababu wengi wanatoka kwenye eneo ambalo halina mshahara mzuri wanataka waende kwenye taasisi ambazo zinalipwa vizuri kama *TANAPA* na *NCAA*. Kwa hiyo, hawa wengine wanaona kwa nini wakati sisi wote tunafanya kazi moja. Kwa hiyo, ninaomba sana na niiombe Serikali angalieni maslahi ya watumishi hawa, wawe na maslahi ya aina moja ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi hizi kazi ni ngumu, ngumu kwa wote.

Wanaolinda mapori kazi ni ngumu na wanalinda hizi hifadhi zetu kazi ni ngumu. Kwa hiyo, wapeni maslahi yao ya aina moja ili wote waweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na mapori ya akiba kwenye Kanda yetu ya Magharibi. Kanda ya Magharibi tunayo mapori ya Luganzo, Tongwe, Igombe, Ugalla, Inyonga na Wembera, haya mapori yameshapandishwa hadhi. Pamoja na kupandishwa hadhi hifadhi hizi zinasubiri kukamilika kwa zoezi la mapitio ya mipaka, zoezi hili lilianza lakini lilisimamishwa. Kwa hiyo, tunaomba sana zoezi hili liendelee ili mipaka hii waipitie, wakishaipitia pawekwe zile *beacon* ili wananchi wetu waweze kupata maeneo ya kufanya kazi kwa utaratibu mzuri ili kuondokana na kugombana baina ya wahifadhi pamoja na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ugomvi katika maeneo yao, hivyo tunashauri sana hii Kamati ambayo imeundwa, tunaomba sana iendelee na zoezi hili ili basi waweze kumaliza hii kazi na wananchi wetu waweze kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine suala la Msomera. Kwanza kabisa mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuamua kwa dhati kabisa kutaka kuiponya Hifadhi yetu ya Ngorongoro. Wananchi wa Ngorongoro walioamua kuondoka wenyewe kwa hiari wameshafika Msomera, lakini hawa wafugaji wameniomba niwaombee wanachangamoto kubwa ya maji pamoja na maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali kupitia Wizara hii wawafanyie kila linalowezekana wafugaji hawa, kwa sababu wao wanachotegemea ni mifugo yao. Kazi nzuri iliyofanyika, nyumba nyingi zilizojengwa na wananchi ambao wameshahamia kule wanachoomba wapewe maji pamoja na maeneo ya malisho, mifugo ndiyo kitu wanachokitegemea katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wengine ambao wapo kule Ngorongoro wamekaa wanasubiri, Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yako tunaomba sana wale ambao tayari wanasubiri kwa hiari yao kuondoka kule kurudi huku fanyeni kila linalowezekana, malizeni huu mpango ili kuweza kuunga mkono juhudi za Mama. Kuweza kuhifadhi zaidi Mbuga yetu ya Ngorongoro na kuweza kuwa salama. Tulikuwa tukienda Ngorongoro unaanza kukutana na kondoo, ng'ombe, mbuzi lakini sasa hivi angalau hawajaisha lakini angalau kumepungua hata ukipita unaanza kuona, unajua kwamba kweli sasa hili ni eneo la uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba na mazungumzo pia yaendelee hata kwa wale ambao bado hawapo tayari muendelee kuwaomba siyo kuwalazimisha kama ambavyo mmefanya tangu mwanzo ili waendelee kuhama wenyewe kwa hiari, waweze kuondoka pale na waweze kwenda Msomera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msomera sasa hivi shule zipo, tumeona kuna zahanati, tumeona kuna kila huduma za kijamii. Sasa changamoto iliyopo wapewe maji pia wapewe na maeneo ya malisho ili wasipate hamu tena ya kurudi Ngorongoro na kuanza tena kufukuzana kama ambavyo watu wanatarajia. Kwa sababu hili zoezi siyo watu wote walilipenda, hasa hata wenzetu majirani walilichukia na matokeo yake walianza kama kufanya hujuma lakini Mungu amebariki msimamo wa Rais wetu umekwenda vizuri na leo watu wengi wako Msomera kwa hiari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu nilikwenda na nimejionea mwenyewe na tumpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliyeko sasa kwa kazi nzuri anayofanya ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kuwa na utulivu na wanaendelea kupata mahitaji yao katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya muda naomba kushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama,

Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia asubuhi ya leo. Nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanampongeza sana Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi kubwa, ubunifu na uzalendo mkubwa aliounesha katika utendaji wake Serikalini tangu alivyoanza kuteuliwa kwenye Wizara mbalimbali na sasa kwenye Wizara hii, Mheshimiwa Mchengerwa ameonyesha ubunifu wa hali ya juu sana na mimi nina mpongeza sana huyu Babu yangu kutoka Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Naibu Waziri Mary Masanja, mpambanaji huyu mama, amefika mpaka Madaba na amefanya kazi na Wanamadaba pamoja na Wanawino kwa kweli mchango wake kwa Taifa letu hautasahaulika na hasa kwa Wanamadaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninayo mambo machache ya kuchangia lakini niliona ni vema nikaanza kuwapongeza na kuwashukuru viongozi hawa wakubwa wa Wizara hii na katika orodha hiyo naomba uniruhusu nimuunganishe na Mkurugenzi Mkuu wa *TFS,* Dos Santos Silayo ambaye anafanya kazi kwa karibu sana na Mhifadhi Mkuu wa Shamba letu la *TFS* lililopo Wino, Madaba, kwa uzalendo mkubwa sana waliouonesha kwa wananchi wa Madaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapompongeza Ndugu Silayo na Dada yetu Glory Kasmiri ambaye ni Mhifadhi Mkuu wa Shamba letu la Wino, ninakumbuka na kutambua mchango mkubwa sana wanaoutoa kwa wananchi wa Madaba. Moja, ieleweke kwamba Mheshimiwa Waziri nadhani unajua kwamba Shamba la Wino la *TFS* liko katika Halmashauri ya Madaba na shamba lile lina hekta 39,711. Shamba hili linagusa vijiji vitatu muhimu, Kijiji cha Wino, Ifinga na Mkongotema. Kazi inayofanyika kwenye shamba hili ni kubwa na uwekezaji uliofanyika kwenye eneo hili ni mkubwa na shamba hili linaweza likashika nafasi ya tatu hadi ya tano Kitaifa.

Kwa hiyo, mnaweza mkaelewa ni ukubwa gani wa uwekezaji umefanyika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru viongozi wangu hawa kwa kusaidia pia shughuli zingine za maendeleo ambazo wanazifanya kwenye Vijiji vya Wino, Ifinga na Kijiji cha Matetereka. Natambua michango ya *cement*, natambua mchango wa mabati, natambua mchango wa wajasiriliamali, vifaa vya kuvunia asali lakini mitaji na vifaa vya kufuga nyuki kwenye misitu. Kazi inayofanyika ni kubwa nilitamani niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua miche mingi ya miti mnaizalisha na mnagawa kwa wananchi hawa kupitia programu yetu ya panda miti kibiashara, wananchi wa Madaba wamepata miche mingi sana na tunaendelea kupanda, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Wanamadaba tuendelee kupanda miti kwa bidii kubwa kwa sababu miaka 10 ijayo Madaba itakuwa moja katika Halmashauri tajiri sana hapa Tanzania, tutakuwa tunafukuzana na Halmashauri ya Mafinga, kwa hiyo niwaalike sana Wanachi wa Madaba kutumia hii fursa ambayo tunaipata *TFS* kwa ajili ya kuandaa na kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba pamoja na kazi nzuri ambayo tumeifanya kupitia *TFS* Madaba, huduma kwa wananchi, tunazo hifadhi na maeneo ambayo yanafaa kuwa hifadhi ya wanyapori. Tumeleta kwako kupata kibali cha kuanzisha Hifadhi ya Wanyamapori Ifinga. Mheshimiwa Waziri naomba nikufahamishe kwamba Ifinga ni Kijiji ambacho kinapakana na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere au Selous katika maeneo hayo lakini tunapakana na Malinyi. Tunayo hifadhi kubwa ambayo tulitamani hifadhi hii ichangie kwenye Pato la Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kijiji ni maskini sana ukilinganisha na vijiji vingi Tanzania, ndiyo kijiji pekee ambacho ndicho kijiji na Kata yaani tuna Kata na kijiji kimoja ndicho hicho hicho. Hawa wako mbali sana hawafikiki kirahisi. Tunayo changamoto ya barabara, tunayo changamoto ya kipato cha wananchi, tunayo changamoto ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Tumeomba

Mheshimiwa Waziri utusaidie eneo hili lina heka 37,225 tunaomba eneo hili litumike kuwa hifadhi ya jamii kwa maana ya *WMA*. Hatua zote tumezimaliza tunachosubiri ni Wizara yako itume wataalamu wakafanye tathmini ya utoshelevu na mahitaji mengine ya eneo hilo lakini tunaomba sana Mheshimiwa Babu yangu Mchengerwa tupe eneo hili tukafanye hifadhi ya wanyamapori ili kuchangia kipato cha wananchi wetu na kuchangia uhifadhi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba bonde hili linachangia sana maji yanayoenda Rufiji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi maeneo haya kama ambavyo tumefanya kwenye misitu ni ushiriki wa wananchi katika kuchangia kuhakikisha kwamba tunahifadhi Bwawa letu la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Halmashauri ya Madaba inapakana na Hifadhi ya Mbarang'andu, hifadhi hii ipo ndani ya Halmashauri ya Namtumbo lakini kuna Kijiji cha Ngadinda, Kijiji cha Mbangamawe, Kijiji cha Lutukila. Vijiji hivi vyote vinapakana na hifadhi hii na vijiji hivi vyote wananchi wake wameshiriki katika kuhifadhi mazingira ya eneo hili. Tunaomba basi kunapokuwa na gawio linalotokana na mapato ya *WMA* vijiji hivi vitatu vinufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kijiji cha Ngadinda kimepoteza mpaka miundombinu ya umwagiliaji ambayo ilijengwa kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa wananchi wale. Ile miundombinu ya umwagiliaji imeangukia kwenye eneo la *WMA* na wananchi wanashindwa kulitumia, basi mapato yanayotokana na uhifadhi huo yakasaidie maendeleo ya wananchi wetu wa Ngadinda, Mbangamawe na Lutukila. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa maslahi ya muda nikuombe sana hiki Kijiji cha Hifinga kama nilivyokwambia huko nyuma miaka ya 1950 kilikuwa kwenye Wilaya ya Ulanga, kwa hiyo hakikuwa Songea. Sasa kimekuwa *adopted* Songea kwa sababu ya mazingira yake ya kijiografia. Tumepata wawekezaji kama *SUA* wana hekta 10,000 za kupanda miti. Tuna KKKT, hawa

hawajafanya lolote lakini wana eneo kubwa sana wamelichukua kutoka kwa wananchi. Tunayo *program* ya *FDT Concession* lakini tuna Mufindi *Wood Poles.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wadau ambao ninawashukuru sana mbele yako nimetamka kuhusu *TFS,* na Mufindi *Wood Poles* ninawapongeza sana kwa kuchangia sana maendeleo ya kijiji kile sasa tunajenga kituo cha afya kwa kupitia mchango wa wadau hawa. Ninawashukuru na ninawaomba waendelee, *SUA* tunawashukuru kwa sehemu wameanza kufanya sehemu fulani lakini bado ahadi zao hazijatekelezwa kwa asilimia 100. Ninaomba ushirikiane nasi kuwataka wadau wote waliowekeza kwenye kijiji cha Ifinga waliochukua ardhi ya kijiji cha Ifinga wakatekeleze ahadi zao na wakapande miti. Kama hawatafanya hivyo Mheshimiwa Waziri tutaomba ushauri wako ili maeneo haya muhimu yarudi kwa wananchi ili waweze kunufaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri ninarudia kukupongeza na ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Neema Mgaya wajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu rahimu kwa ruzuku ya uhai na afya, pia nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa Waziri, *CPA* Mary Masanja Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas na Naibu Katibu Mkuu Anderson Mutatembwa na Watumishi wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza na suala ambalo linatupa usumbufu mkubwa sana katika Jimbo la Kilosa nalo ni

tembo kuharibu mazao na miji ya watu na kwa muda mrefu wananchi wetu hawajapewa kifuta machozi kwa uharibifu huo wa tembo na maeneo ambayo yameathirika sana ambayo ningeomba Wizara itusaidie kuwalipa kifuta machozi kwa haraka ni Kata ya Kimamba A katika maeneo ya Soko Msuya, Mkwajuni na Sikutari, Kimamba B, maeneo ya Uhindini, Kigamboni, Pusa na Mji Mwema, Kata ya Ludewa eneo la Peapea na Kata ya Madoto eneo la Mbwade na Kata ya Parakwio eneo la Mkata Stesheni na Mkata. Tutashukuru sana kupata kifuta jasho kwa wananchi lakini pia tupewe kituo cha kupambana na tembo hao kwa sababu tembo kutoka Hifadhi ya Mikumi wanakuja sana katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu Dodoma. Dodoma sasa ni Makao Makuu ya Nchi yetu, Dodoma sasa ni Jiji na ningependa kabisa kutoa ushauri kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Makao Makuu ya Nchi yanastahili kuwa na hifadhi kubwa. Kwa hiyo ninashauri Dodoma ipewe hifadhi, ianzishwe hifadhi kubwa inayoendana na heshima ya Mkoa huu lakini heshima ya Jiji hili. Pamoja na hayo tufikirie kuanzisha eneo kubwa la msitu *(park)* ambayo Miji mingine mikubwa wanayo, Berlin wana *park* kubwa sana ya *Tiergarten*. Sasa imefika mahali Dodoma pia tuwe na *park* kubwa sana ili Mji huu na eneo hili lilingane na hali na hadhi ya Mji. Tunaomba hifadhi kubwa ianzishwe katika Mji wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia eneo jingine na hili ni kuhusu utalii.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayechangia kwamba Kondoa tayari tuna hifadhi mbili. Tuna Hifadhi ya Mkungunero ambayo ina wanyama wote na tunayo Hifadhi ya Swagaswaga nayo pia ina wanyama wote na pia pale Kondoa

tuna eneo ambalo tumelitenga ni kubwa kwa ajili ya hichi anachokiongelea Mheshimiwa Mbunge Wizara inaweza ikachukua ikatengeneza hiyo *park* kubwa na Dodoma ikawa ina eneo kubwa ambalo litakuwa ni kivutio kwa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo lakini naiboresha huko ni Mkoa wa Dodoma lakini Dodoma ni kubwa ni pamoja na Jiji la Dodoma. Kwa hiyo, naipokea hiyo taarifa lakini naongezea Jiji la Dodoma na lilikuwa maarufu sana kwa tembo na ndiyo maana inaitwa Dodoma, Idodomia maana yake hapa tembo walikuwa wanazama na njia yao ndiyo leo *University* hii ya *UDOM* ndiyo maana mara nyingi hurudi kuja kusalimia maeneo waliyoishi miaka na miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ningependa kulichangia ni kwenye utalii na hapa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *Royal Tour* na tunasubiri kwa hamu sana hii *film* nyingine ya *The Hidden* Tanzania na ninaamini katika *film* ya *The Hidden Tanzania* hifadhi ya Kitulo itakuwemo. Ni hifadhi ya aina yake kabisa duniani na inastahili kutangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine katika utalii ni upekee wa Tanzania katika utalii duniani na eneo la upekee wa Tanzania katika utalii duniani ni eneo la utalii wa vivutio vitokanavyo na hali ya jiolojia ya nchi *(geo - tourism)*. Huu ni wakati sasa wa kusukuma *geo – tourism, geo – conservation* na kuanzisha *geo – park* nyingi iwezekanavyo. Hapa nataka nitoe maeneo 11 ambayo tukiyafanyia kazi hiyo, mengine tayari yametambuliwa na kuhifadhiwa, mengine bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Kilimanjaro. Sasa tuutangaze Mlima Kilimanjaro kuwa ndiyo mlima mrefu kuliko yote duniani wa aina ya *volcano*. Ndiyo mlima mrefu kuliko yote

duniani wa aina ya *volcano* na Mlima Kilimanjaro hauna vilele viwili, una vilele vitatu kijiolojia navyo ni Shira ambayo ni *extinct,* Mawenzi ambayo ni *extinct* na Kibo ambayo ni *dormant*. Taarifa hizo zimo kwenye kitabu kinaitwa, "*Kilimanjaro Mountain Memory and Modernity*" kimechapwa na Mkuki na Nyota mwaka 2006, kina kurasa 321. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili muhimu sana ni *Mautia Hill* – Kongwa. Hiki ni kilima pekee duniani chenye madini ya aina ya *Yoderite* na jambo la kusikitisha, nakuomba Mheshimiwa Waziri chukua hatua za haraka hata ikiwezekana leo kwenda kukinusuru kilima hiki. Saa hizi ukipita pale karibu na Kongwa *Ranch* utaona wanachimba *limestone*. Kilima hiki kikipotea tumepoteza kilima pekee duniani chenye madini ya aina ya *Yoderite*. Kitangazwe kuwa ni kimehifadhiwa kiwe *geo–park* na wewe Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Madini tukinusuru kilima hiki. Wanakuja watalii na wanasayansi toka Marekani, Ujerumani, Austria kwenda pale *Mautia Hill* – Kongwa na sasa ukona pana mchirizi kuna mtu anachimba *limestone*. Tukinusuru kilima hiki ambacho ni utajiri duniani wa pekee. Hakuna mahali pengine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni Ngorongoro. Tulitangaze sasa Bonde la Ngorongoro kuwa ndiyo bonde kubwa duniani la aina ya *volcano (the largest caldera in the world, the largest caldera in the world)*. Sehemu ya nne ni Empakai. Hili ni moja ya bonde la *volcano* lenye kina kirefu duniani *(one of the deepest calderas in the world)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ni Yalumba kule Ludi -Kibakwe na Ikora kule Katavi. Hapo una miamba ya zamani kuliko yote duniani ya mfumo wa aina ya *eclogites* hupati sehemu nyingine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sita ni Oldonyo Lengai. Huu ni mlima pekee duniani wenye *volcano* ya aina ya *cobaltite* na saba ni Kimondo cha Mbozi *(iron meteorites)* na nane ni Mwadui. Mwadui ni moja ya *Kimberlite* kubwa duniani inayozalisha almasi kwa faida. Tisa ni Igwiti – Tabora, hiki ndiyo kilima chenye *volcano* ya aina ya *kimberlite* kule Igwiti – Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi ni Tendaguru. Tendaguru ambayo najua iko kwenye Jimbo la Mchinga la Mama Salma Rashid Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tendaguru ndiyo kwenye masalia ya viumbe wakubwa duniani hawa *dinosaurs,* ambao walichimbuliwa na sasa wako katika Jumba la Makumbusho Berlin. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumezungumzia kujenga kituo kule. Kituo hicho kijengwe kiboreshwe na wenzetu Wajerumani sasa nyaraka na taarifa zote zipo na wametoa kitabu katika mambo yote ya Tendaguru kinaitwa, "*Dinozauria Fragmente Zur Geschichte dea Tendaguru Efbideschion Undiire Objecte Nohis Hundadet Enzeks Bisdoiz Zauthousand Axzen*" yaani kwa Kiswahili ni "Vipande vya Dinosauria, historia na masalia ya msafara wa kipaleontolojia kwenda Tendaguru Tanzania mwaka 1906 – 2018" na Mheshimiwa Waziri miaka yote tisa niliyokaa Berlin kila walipokuja wageni niliwapeleka kwenye *museum* Naturkunde ambayo iko kwenye Chuo Kikuu cha *Humboldt Universitat zu Berlin* ambako kwa bahati Mke wangu Dkt. Amina alifanya *PhD* yake pale, na ninazo picha ambazo nitazileta za watu wote walioshiriki kuchimba ile masalia. Tutengeneze Tendaguru iwe ni moja ya vivutio vikubwa vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 11 ni *Olduvai Gorge*. Hii ndiyo bonde la kwanza duniani kukaliwa ni viumbe vya kwanza vyenye umbile la binadamu. Ndiyo chimbuko la kwanza la binadamu, ndiyo *the first home of Zinjathropus Australopithecus Boisei.* Hapa tufikirie upya zile nyayo. Wataalamu wa sayansi watusaidie ziendelee kufukiwa au sasa zifukuliwe ili watu wazione na katika kundi hili sehemu ya 12 ni Mapango ya Amboni. Haya ni mapango yanayotokana na *limestone* na yalitokea miaka milioni 150 iliyopita na katika kipindi cha *Jurassic* na kwa miaka milioni 20 yalifunikwa na maji. Najua yako mapango 10 ni moja tu ambalo linatumika. Tuone hayo tisa kama tunaweza tukaongeza mengine ili eneo nalo hilo liwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Mchengerwa na Wizara tuyahifadhi maeneo haya, tuyatambue maeneo haya, tuyatangaze maeneo haya na tuwe ndiyo watu wa kuonyesha dunia tunavyo vitu vya pekee ambavyo sehemu

nyingine duniani havipo isipokuwa Tanzania tu na hii ni hali ya jiolojia ya nchi yetu ambayo Mwenyezi Mungu ametusaidia kuiumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa kushukuru ni kwenye upande wa malikale na kumbukumbu za Taifa. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako ukurasa wa 93 umetangaza kwamba Pango la Magubike katika Jimbo la Kilosa ni moja ya maeneo sita ya malikale ambayo mmebaini yanakidhi vigezo vya kuwa Urithi wa Taifa. Nawakaribisha sana mje tufanye, tutunze hilo pango la Magubike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakushukuru sana kuwa njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa kutoka Ujiji hadi Bagamoyo pia vijiji viwili vya Jimbo la Kilosa vimo, Mamboya alikozaliwa Babu yangu na Rubeho. Nawakaribisha sana kufika katika maeneo hayo ili tuhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kilimatinde ambako anatoka Baba yangu na hapa Kilimatinde Mheshimiwa Naibu Waziri ameshafika. Ile nyumba waliyokaa Askari wa Kijerumani iliyokuwa *officers mess* leo ndiyo nyumba ya Kasisi pale inaanza kubomoka. Lile boma la mawe linaanza kubomoka. Yale makaburi matatu ya Maafisa wa Kijerumani waliofia Kilimatinde yameanza kuharibiwa. Yale makaburi saba ya Wajerumani Askari yameanza kuharibiwa. Naomba na kile kisima ambacho watumwa walikunywa maji kabla ya kushuka kwenye bonde la ufa pale Kilimatinde na ninaamini ndiyo iliyozaa Kilimatinde ya Pemba na ndiyo iliyozaa Kilimatinde ya Oman na ndiyo iliyozaa Kilimatinde Liverpool, ningeomba maeneo hayo pia yahifadhiwe ili yawe urithi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kilosa naomba Stesheni ya zamani ya Kondoa, jengo ambalo halitumiki kati ya Kimamba na Kilosa lije litengenezwe ili ibaki kuwa ni kumbukumbu ya aina ya stesheni ambazo Wajerumani walizijenga lakini ile stesheni ina umuhimu mkubwa sana. Hiyo ndiyo ilikuwa njia ya watumwa na inaelekea watumwa hao kutoka Kondoa walipitia njia ya kutoka Kondoa kuja Mamboya wakashuka kuja mpaka

pale, na tufahamu kwamba sehemu kubwa ya reli ya kati kutoka Morogoro mpaka Dodoma zamani ndiyo ilikuwa njia ya utumwa na njia ya biashara ya vipusa. Kwa hiyo nitashukuru sana lile jengo mkishirikiana na Shirika la Reli Tanzania kulitengeneza kulihifadhi kati ya Kimamba na Kilosa limepandwa miti linahitaji utaalamu ili nalo liwe sehemu ya vivutio vya utalii katika Kilosa ambayo sasa tuna *tunnel* zile tano za *SGR* lakini pia tunaomba kufungua sasa geti jipya kutoka Mji wa Kilosa kuingia katika Mbuga ya Mikumi ili watalii wakifika Kilosa na *SGR* waweze kwenda Mikumi na ninaamini kabisa katika hilo mtatusaidia kufungua haraka sana geti la Kilosa Mjini ili watalii hawa waweze kuingilia Mikumi lakini pia waweze kuingilia Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa hayo yote nakushukuru sana kwa kuchangia na ninaunga mkono hoja asilimia 100 na ninaomba fidia ya kifuta jasho kwa ajili ya tembo kule Kilosa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi. Nilimtaja Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Yahya Mhata ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhanahu wata'ala* kwa kutujalia uhai, uzima na salama lakini pia nikimshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye ni mhifadhi namba moja kwa jitihada ambazo amekuwa akizichukua katika kuendeleza masuala mazima ya uhifadhi wa maliasili Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli amechukua ofisi hii muda mfupi uliopita lakini jitihada zake zinaonekana wazi kwamba anakwenda kufanya kitu. Jitihada tumeziona na mimi juzi wakati anazungumza kwenye semina pale niliwaambia wenzangu naona Mheshimiwa Waziri hii *tune* ambayo ameizungumza hapa leo, hii ndiyo *tune* ya maliasili. Maana yake kuna *tune* ambayo unaweza ukaiongea mahali pengine lakini kuna *tune* nyingine hiyo ndiyo ya kuiongelea

kwenye Maliasili na ndiyo ile Mheshimiwa Waziri uliyozungumzia ukamalizia pale kwenye semina juzi, ile ndiyo *tune* ya kuizungumza katika uendelezaji wa maliasili popote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia mambo manne kama muda utaruhusu. Jambo la kwanza ninazungumzia kuhusu suala la uendelezaji wa hifadhi zetu. Kama inavyofahamika kwamba hifadhi zetu zimeongezeka kutoka hifadhi 16 mpaka kwenda kuwa hifadhi 22, eneo la hifadhi limeongezeka kufikia karibu kama sijakosea kilometa za mraba sasa hivi 105,000 hivi kama. Eneo ni kubwa lakini bajeti haikuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumzia hili hapa hali kadhalika wakati tunatoa ripoti ya nusu mwaka Kamati pia ilipendekeza kwamba lazima tuangalie uwezekano wa kuongeza bajeti katika hifadhi zetu ili ziweze kukidhi changamoto ambazo zinatokea kwenye uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwaka jana wakati ana-*conclude speech* yake hapa aliahidi kwamba hifadhi atazipatia bajeti ya miezi miwili kwa utangulizi ili bajeti moja ibakie kama *spare in case* ikitokezea dharura za moto, dharura za uhifadhi zote zile itatumika lakini utatuzi huu haukusaidia sana. Hifadhi zetu bado zinateseka na tatizo la kibajeti na zinahitaji mchango mkubwa kwenye bajeti. Kwa hiyo mimi napendekeza kama alivyozungumza Mheshimiwa Hawa Mwaifunga hapa kwamba pamoja na changamoto za *retention* ambazo zilipelekea *retention* kuondoshwa, mimi naomba tena *retention* tuirejeshe hata kwa asilimia siyo ile iwe pungufu lakini *retention* ni muhimu katika masuala ya uhifadhi. Hiyo ni kama utaratibu wa kidunia. Masuala ya uhifadhi lazima kuwe kuna *retention* ambayo inatumika kwa sababu ukifuata utaratibu wa kawaida wa kibajeti basi hutozisaidia sana kwa sababu mambo mengi ya kidharura yakitokezea hutoweza kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ningependa kuzungumzia kuhusu mwenzangu ambaye amechangia kuhusu Msomera. Nahisi kama tunakwenda kusahau changamoto ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Tulipelekea kufanya

maamuzi yale tuliyopelekea watu waende Msomera kwa sababu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iko hatarini, hizi hatari zilizungumzwa hapa na watu wakafika mpaka kutoa machozi kutokana na tatizo la Mamlaka ya Ngorongoro lakini sijui ni utaratibu wetu au utamaduni wetu watanzania, jambo tunaweza tukalichukua kwa kasi kubwa lakini baadae tukapoteza *mood*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi *mood* ya Ngorongoro imeanza kupungua. Sasa nilichangia hapa katika ripoti ya Kamati ya nusu mwaka nikazungumza kwa sababu wenzetu wameshafanya utafiti wamesema wakipata shilingi bilioni 200 basi hii kazi inakwenda kuisha. Nikazungumza kwamba kwa sababu makusanyo ya Mamlaka ya Ngorongoro yenyewe tu yanakaribia shilingi bilioni 200, sasa kama hatuna fedha basi Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuwaruhusu wenzetu wa Ngorongoro wanachokikusanya wakitumie ili tuondoshe hili tatizo, lakini kama kuna uwezekano mwingine basi tuwakopee, tutafute mahali tukope hili jambo tulimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema, "Mchuzi wa mbwa unywewe ukiwa wa moto." Sasa suala la Ngorongoro tulimalize likiwa liko moto moto, tukikaa hapa miaka mitatu, minne, mitano tutapoteza dira nzima ya masuala ya Ngorongoro ambayo tilishakubaliana nayo hapa. Kwa hiyo niombe Wizara na zaidi Waziri wa Fedha tuwapatie wenzetu Mamlaka ya Ngorongoro, tuwapatie wenzetu wa Maliasili fedha kwenda kumaliza hili suala. Tusifanye kazi zetu kwa vipande vipande, tunafanya kazi nusu, nusu inabakia mwaka mzima, matokeo yake tuna vipande vipande dunia nzima hatuendi hivi. Kwa hiyo mimi naomba hili tukalisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni kuhusu Jeshi USU ambalo pia mwenzangu hapa amelizungumzia, sasa hivi limepandishwa daraja limekuwa Jeshi la Uhifadhi. Tunalo tatizo kubwa kuhusu suala zima la Jeshi la Uhifadhi maslahi yao siyo mazuri. Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa na alikuwa anakaribia kutoa machozi, Jeshi la Uhifadhi wanapata shida sana. Wanakufa, wanauliwa, wanajeruhiwa lakini maslahi yao hayaendani na kazi wanayoifanya. Watu wa Jeshi USU au Jeshi la Uhifadhi wako kwenye mapambano mwaka mzima, wawe

mitaani mwaka mzima anaingia kazini *bismillah* kwanza ana mapambano na wanyamapori lakini ana mapambano na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuende tukarebishe maslahi ya Jeshi la Uhifadhi na hili mimi nilitegemea, kwa sababu tunaambiwa kwamba watu wa utumishi ndiyo wanalishulikia hili suala, kuna suala sijui waraka tayari umeishapelekwa wapi? jamani tusifanye kwa mazoea hebu tukifanya mambo tuyamalize, hawa watu wanauhitaji. Hapa nitoe ombi maalum vijana wetu wanaomaliza Olmotonyi, Mweka ambao ndiyo tunategemea tuwaajiri kwenda kuwa Jeshi la Uhifadhi, kwa sababu hatuajiri kila mwaka tunakaa miaka miwili, miaka mitatu wanapitwa na umri, sasa hili suala la umri Mheshimiwa Waziri hebu liangalie hili, tusiwaache hawa vijana ambao tayari wameishamaliza chuo na wana vigezo vyote, lakini suala la umri linakwenda kuwasumbua. Kwa hiyo ningeomba tu suala la umri ingawa lipo kisheria, hebu tukaliangalie kwamba wanafunzi wote ambao hawajaajiriwa wanachuo wetu basi ikitokea nafasi wawe na nafasi sawa ya kuomba kuweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni kuhusu suala la hewa ya ukaa. Nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo amepiga hatua kubwa kwa kutayarisha mwongozo wa suala zima la biashara ya hewa ukaa, lakini bado hatuendi kwa hatua kubwa hasa katika uelimishaji. Kwa sababu inaonekana kwamba biashara ya hewa ya ukaa ni kama vile Serikali ndiyo itaongoza kila kitu. Hii ni biashara huria isipokuwa Serikali inatakiwa iweke vigezo na kuwaruhusu wadau kuingia kwenye hii biashara. Kwa hiyo, tuende tukatoe elimu kwa sababu ina faida kubwa katika uhifadhi wa misitu yetu hii ni *incentive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa uharibifu wa misitu ni mkubwa sana kwa Tanzania. Tunapoteza karibu hekta laki nne kila mwaka, sasa watu wanafikiria kwamba ukishakuwa na msitu tayari wewe uko *eligible* kuweza kupata fedha za hewa ya ukaa. Kupata fedha za hewa ya ukaa ni *incentive* ya uhifadhi, umehifadhi kwa kiwango gani? kwa hiyo, kile kiwango ambacho kinaongeza *(additionality permanence)* ya uhifadhi ndiyo inayokwenda kukupa *credit* ya biashara ya hewa ya ukaa. Kwa

hiyo, twende tukatoe elimu kwa wananchi wetu, tukawambie kwamba kuwa na msitu ni jambo moja lakini suala la kuulinda, kuhifadhi usichomwe moto, usikatwe hovyo, usiharibiwe ndiyo utakwenda ku – *add value* wewe kupata fedha za hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala zima la utafiti. Tuna taasisi zetu za utafiti za *TAFORI* na *TAWIRI* lakini nazo hizi zina tatizo kubwa la kibajeti na tumelizungumzia hapa, ukienda *TAFORI* kwa mfano, inafika wakati hata kuweza kulipa umeme hawawezi, ile kulipa umeme hawawezi inamaana inabidi wachangishane ofisini wakalipe umeme wa ofisi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeliomba Mheshimiwa Waziri, tukazingalie hizi Taasisi za Utafiti, kwa sababu hakuna nchi ambayo itaendelea bila utafiti, hakuna eneo ambalo utalifanyia kazi bila utafiti, ili wafanye utafiti vizuri lazima tuendeleze kibajeti. Sasa ningeliomba tu angalau fedha ambazo zilikuwa zinatengwa tuwaongezee ziongezeke kidogo kadhalika na fedha zenyewe zipatikane kwa wakati, siyo fedha zinatengwa asilimia 100 lakini wanapata asilimia 26 mwaka ukimalizika, hii haitusadii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Yahya Mhata na Mheshimiwa Benardeta Mushashu ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uhai kwa kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote ndani ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza Mhifadhi namba moja Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye programu ya *Royal Tour* na tumeona watalii wanaendelea kuongezeka ndani ya nchi yetu na naamini wataendelea kuongezeka kama vile walivyo ongezeka katika nchi ambazo zili – *practice* programu hii ya *Royal Tour* kama wenzetu wa Mexico, Poland, Ecuador na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunamshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja Mkoa wa Njombe tarehe 26 Agosti, 2022 alisema kwamba itakuja *phase two the hiding place of* Tanzania na hii ita – *cover* maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha nia ya dhati ya kukuza utalii wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyanda za Juu Kusini tuna vivutio vingi sana. Ukianza Iringa tuna Hifadhi ya Ruaha ambayo ina simba ambao wanatembea kwa makundi makubwa, ambayo huwezi ukaona simba hao kwenye Hifadhi zingine nchini. Vilevile ukienda Rukwa kuna maporomoko ya Karambo, maporomoko haya ni ya pili kwa ukubwa Afrika yakitanguliwa na yale ya Victoria *Fall* kule Zimbabwe. Ukienda Songwe tunakuta Kimondo, kivutio pekee ambapo huwezi kukiona sehemu nyingine. Ukienda Njombe unakuta Hifadhi ya Kituro ambayo ni ya kipekee ulimwenguni, lakini ukirudi huku Mbeya unakuta Kijungu, maji yanapanda mlima, utakuta Kisimba vilevile utalikuta Ziwa Ngosi ambalo lina ramani ya Afrika na lina maji mazuri yenye rangi ya bluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fukwe nzuri Matema *Beach,* ukienda Ruvuma utazikuta fukwe hizi Njombe pia kule Ludewa. Ushauri wangu kwa Serikali, iendelee kuvitambua na kuvifanyia kazi vivutio vya Nyanda za Juu Kusini ili kuweza kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine Serikali iharakishe kumaliza *phase one* ya *regrow* ili ianze *phase two* ambayo itatoa fursa kwa hifadhi ambazo hazikuingia kwenye *phase one*. Hifadhi kama ya Kituro na Katavi ziweze kufaidika na mradi huu. Kwa

kufanya haya itarahisisha programu ya *phase two* ya *The hidden place of* Tanzania kuja kufanya kazi vizuri kwa sababu muda huo tutakuwa tumeishajiandaa vizuri kutambua na kuainisha vivutio vya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaombi kwa *TANAPA* Serikali iangalie namna ya kuwaongezea bajeti *TANAPA*. Kwa sababu wakati wana hifadhi 16 *TANAPA* walikuwa wanapata bilioni 104. Sasa hivi hifadhi imeongezeka ziko 22 wanapata bilioni 111, lakini hitaji halisi la Bajeti ya *TANAPA* ni bilioni 222 unaweza ukaona hapo ni *fifty percent* tu ya wanayoipata kutokana na hitaji lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TAWA, TAWA* mapori yameongezeka lakini bajeti ni ndogo. Serikali iangalie namna ya kuwaongezea pesa ili waweze kufungua njia au barabara kwenye mapori hayo lakini vilevile wawaongezee watumishi. Baada ya kumaliza hiyo Nyanda za Juu Kusini, sasa napenda nizungumzie utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inabidi sasa ifanye mikakati mikubwa ya kuhakikisha ya kwamba tunaendeleza utalii wa fukwe. Tunazo fukwe nzuri lakini Serikali bado hawajazifanyia kazi. Ukienda *Seychelles* wamefanikiwa sana katika utalii wa fukwe na wanafanya vizuri, kwa sababu wao wana mamlaka maalum ya kusimamia fukwe na hiyo mamlaka iko chini ya Bodi ya Utalii. Kazi ya mamlaka hiyo kuandaa mipango ya matumizi ya hizo fukwe vilevile kusimamia utekelezaji wa mipango ya hizo fukwe, pia wanakazi ya kuratibu na kuzitangaza fukwe hizo kwa kushirikiana na sekta binafsi, kwa mikakati hii madhubuti ndiyo maana Seychelles imefanikiwa sana kuuza katika utalii wa fukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa kwa Serikali, jambo la kwanza Serikali inatakiwa irudishe fukwe ziwe chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Serikali ikirudisha hizi fukwe kuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii inaweza ikapeleka kwenye Taasisi kama ya malikale. Vilevile irudishe na Visiwa vyote viwe chini ya Wizara ya Malisili na Utalii na hivi Visiwa vinaweza vikasimamiwa na Jeshi USU kule maliasili wana Jeshi USU kwa ajili ya sababu za kiusalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo Serikali inatakiwa itoe fursa kwa wawekezaji, wananchi waweze kujenga *hotel* ili kuiongeza idadi ya vyumba. Hivi sasa tuna vyumba 132,667 ukilinganisha na *competitive* wenzetu hawa hapa Kenya maana hao ndiyo washindani wetu wakubwa, wanavyumba zaidi ya milioni moja. Kwa hiyo, Serikali ione umuhimu wa kuangalia jambo hili na kulifanyia kazi ili tuweze kuongeza mapato katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la pale Kilwa, yale majengo ya kale, Serikali ione umuhimu wa kuyakarabati ili kuanza kufungua utalii na watalii waendelee kwenda zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia masuala la migogoro. Migogoro ya binadamu na wanyama, migogoro ya ardhi kati ya Hifadhi na Vijiji. Nilikuwa naiomba Serikali, Wizara hii ya Maliasili na Utalii ifanye kazi kwa ukaribu na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Mifugo, Wizara Kilimo ili kuweza kutatua na kuweza muda mwingine kuepusha migogoro isiyokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni ile Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pale Mvomero, imejengwa ndani ya muda mfupi, lakini pale kuna mgogoro kwamba wanyama wanakwenda, wanapita mpaka kwenye baadhi ya vijiji pale, lakini inawezekanaje Ofisi ya Serikali wanapewa hati, wanapewa kibali cha kujenga, mipango inafanyika katika Wizara ya TAMISEMI, wanaelekeza ijengwe pale na baadae inakuja kuona kwamba imejengwa katika maeneo ambayo wanyama wanapita! Nafikiri kuna haja sasa Wizara hizi za Serikali zote kabla hamjafanya matumizi ya ardhi mkae kwa pamoja, mshauriane ili muweze kufikia muafaka muone je hili jambo linalofanywa ni sahihi ama litakuja kuleta madhara baadaye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sasa hivi kuna programu inaendelea ya *BBT,* Wizara ya Kilimo kule kwa Kaka yangu Hussein Bashe, ninataka kujua yale mapori, mashamba waliyoainisha ya kuweza kufanya hizo programu za *BBT* wamewasiliana na Wizara ya Maliasili? Isije ikawa baadaye tena waanza kulima mazao

yamekua tembo wanaingia wanaanza tena kulalamika kwamba tembo wanapita, isije ikawa wameweka hizo programu zao katika maeneo ambayo yanaushoroba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiria ni wakati muhimu sasa wa kuangalia umuhimu wa kujua matumizi ya ardhi katika sehemu sahihi kwa wakati sahihi ili baadaye isije kuleta migongano na migogoro hii hifadhi, vijiji, Wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Nilimtaja Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Benardeta Mushashu, Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchukua kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kuwa mchangiaji katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kama ilivyo ada na mimi naomba niungane na Wabunge wenzangu kushukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii inachangia kwa kiwango kikubwa mapato na uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshiumiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa kina kwamba Wizara hii inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 21 la Pato la Taifa. Hili jambo ni hongera sana kazeni buti ili mapato haya ya Serikali na Pato la Taifa liweze kuongezeka mara dufu katika mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tunaimani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri, kwa kipindi kifupi ambacho cha miezi mitatu na siku 22 leo juzi ilikuwa siku 19 leo siku 22, kuna mambo mengi umeyafanya ambayo yanaoesha kabisa kwamba umekuja *serious* kufanya kazi. Ndugu yangu hapa jirani yangu Mheshimiwa Waitara amekubali anasema huyu Mheshimiwa ana kitu ndani yake na mimi nakubali kwamba una kitu ndani yako Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza ili uweze kutumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, ambao mimi najua hawa kwa njia moja au nyingine wameshiriki kikamilifu katika uandaaji wa bajeti hii. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu naomba pia nimpongeze sana, sana Mtendaji Mkuu wa *TAWA* Kanda ya Kusini. Kwa kweli Mtendaji yule anafanyakazi nzuri sana masaa 24 Mheshimiwa Waziri Mtendaji wako yuko kazini. Mimi nilipata majanga makubwa sana ya tembo nilimpigia simu Mtendaji yule alitoa gari yake na Askari wakaja katika eneo la tukio, nampongeza sana Mtendaji yule kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimuombe sana ndugu yangu Waziri, kuna changamoto zipo nyingi ndani ya Wizara yako, nami naomba nizieleze zile changamoto ambazo ziko ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu. Changamoto ya kwanza Mheshimiwa Waziri, ndani ya Jimbo langu kwa mwaka huu tumepata ongezeko kubwa la maafa linalosababishwa na wanyama waharibu hasa tembo. Hili ni jambo la kushangaza haijawahi kutokea ndani ya Jimbo langu watu zaidi ya 200 wamepata mashambulizi na tembo, tembo wameharibu mashamba ya watu, hili jambo kwa kweli linauzunisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kwenye Kata ya Sengenya Mheshimiwa Waziri, vijiji vya Mkumbaru, vitongoji vya Naivanga, Narunyu vimeharibiwa zaidi mashamba 73 ya wananchi yameharibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata ya Sengenya pia Kijiji cha Kinyanyila mashamba ya wananchi yameharibika, kwenye Kata ya Sengenya hiyo hiyo KItongoji cha Igunga zaidi ya wananchi 92 mashamba yao yameshambuliwa na tembo. Katika Kata ya Nangomba Kijiji cha Kiuve mashamba zaidi ya 50 ya wananchi yameshambuliwa na Kata ya Kilimanihewa Kata ya Mjini kabisa tuna Kijiji cha Mnonia mashamba ya wananchi yameshambuliwa. Sasa ninachoomba niliwahi kuchangia hapa na nikasema zaidi ya wananchi 200 wameshambuliwa, nina imani Mheshimiwa Waziri majina haya yako ofisini kwako, rai yangu wananchi hawa mashamba ndiyo ajira yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana kuchukua mwaka mzima wananchi kulipwa fidia au kifuta jasho, ni matarajio yangu Mheshimiwa Waziri utachukua kipindi kifupi wananchi hawa waweze kupewa hicho kifuta jasho.

Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umenifurahisha sana, umekiri kwamba kifuta jasho kinachotolewa ni kidogo na uko tayari kukifanyia marekebisho. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, Mwenyezi Mungu akupe nguvu kabla ya Bunge hili hatujamaliza muda wake huu mwezi wa Saba ulete hayo mabadiliko ili wananchi waweze kupata nafuu ya vifuta jasho ambavyo vinasababishwa na hawa tembo. Jambo hili kwa kweli linaudhunisha sana Mheshimiwa Waziri na wananchi watakuombea mema sana endapo utafanya marekebisho haya ya haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa pia nikuombie ni mgogoro mkubwa uliopo juu ya sekta. Hawa Mawaziri wa kisekta Nane ambao walizunguka Tanzania nzima kutatua changamoto za migogoro. Niliwahi kuzungumza hapa ndani ya Bunge lako, ndani ya Kata ya Mkonona kuna vitongoji vya Chawanika, Kitongoji cha Nambunda na Kitongoji Namaromba, vile vitongoji vimeamuliwa wale wananchi watoke. Mheshimiwa Waziri wananchi hawana tatizo na hilo na tumekubaliana watoke. Changamoto iliyopo wanatokaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza ni Mwezi wa Sita wale wananchi ndiyo kipindi cha kuandaa mashamba. Mpaka sasa hivi hawajui watatoka wapi, watatokaje pale na watakwenda wapi? Kwa kuwa tathmini imeshafanyika na maeneo ya kwenda yameshajulikana, walipeni fidia Mheshimiwa Waziri waende huko walikopangiwa, vinginevyo wasipolipwa fidia mwaka huu, mwezi huu au mwezi unaokuja maana yake wale wananchi tunazidi kuwatia umaskini zaidi. Watakwenda wapi kama mpaka sasa hivi hawajui hatma yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wale wananchi pale walipo kulikuwa na shule wameondolewa, shule kule wanakokwenda haijajengwa. Kulikuwa na huduma za maji wale wananchi wangu walikuwa wanatoa maji Mto Ruvuma, walikuwa

wanaenda kwa mguu tu kuchota maji, leo wamepelekwa mbali na Mto Ruvuma, kule wanakokwenda wanapataje huduma ya maji? Kule wanakokwenda wanapataje huduma ya afya? Mambo haya yote yangeangaliwa. Sasa mimi ninaomba Mheshimiwa Waziri nina imani na wewe, tufanye haraka iwezekanavyo wananchi hawa waweze kwenda walikopangiwa na hizi huduma muhimu zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni changamoto ya mabucha. Mheshimiwa Waziri Wizara yako ilihamasisha wananchi wale ambao wamezungukwa na hifadhi na mbuga waanzishe mabucha ili kupunguza ujangili na wananchi wetu waweze kupata kitoweo kwa halali. Inahuizunisha wananchi wale mfano mimi kwangu pale, kuna vijana walijiunga Sahachi *Company,* Sahachi *Group* walijiunga wakatengeneza bucha, leo ni mwaka wa pili hawajapata kitoweo hata kimoja cha kuuza. Waliuza mara moja tu tena kwa bahati. Sasa Mheshimiwa Waziri, naomba maamuzi yaliyofanywa na Wizara yalikuwa ya busara kabisa ili kupunguza ujangili tuanzishe mabucha ili wananchi wapate kitoweo na wao wawe walinzi wa yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mpaka sasa hivi hakuna utaratibu mzuri uliopangwa wa kuwawezesha wananchi hawa kupata kitoweo, kwa kweli tunawahangaisha sana. Nina kesi pale kwangu ndugu yangu kuna bwana amehukumiwa miaka mitatu au kulipa faini 500,000 kwa kukutwa na nyama ya nguruwe pori jikoni, amekamatwa jikoni nyama inapikwa nguruwe pori amepigwa miaka mitatu au miezi mitano jela, amekaa jela mpaka ndani ya wiki moja ndugu kuchanga changa wameuza shamba ndiyo kwenda kumtoa. Hii kwa kweli ni unyanyasaji haiwezekani! Hawa Askari wako wanachokifanya siyo sawa, kamateni majangili siyo mtu anayepika, unakwendaje mpaka jikoni? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi nakuomba hiyo 500,000 nikitoka hapa unirejeshee ili nimpelekee yule mtoto.

**MBUNGE FULANI:** Kabisa. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo sawa, siyo sawa hata kidogo na kwa kweli tunawavunja nguvu sana wananchi wetu. Kama wananchi wetu wanalinda maliasili, leo anakutwa na nguruwe pori, mimi kwa kweli jambo hili limenihuzunisha sana, limenihuzunisha sana Mheshimiwa, na ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili uwakemee sana watu wako. Wanavyofanya siyo sawa na hiyo shilingi 500,000 naiomba ili nimrudishie yule kijana. Wameuza shamba la mikorosho ambalo wamelihudumia kwa miaka 50 lile shamba wameliuza wale wametiwa umaskini, walikuwa na shamba lao sasa wanaingoja *TASAF*. Maisha gani haya tunawapelekea wananchi wetu? Kwa hiyo hili nakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa naomba sana na mimi nichangie katika masuala mazima ya utalii ni kukupongeza sana katika hotuba yako, umeongea mambo mazuri sana jinsi ya kuboresha na kuongeza utalii na mimi naomba nichangie kidogo. Naomba tutumie Balozi zetu kikamilifu ili ziweze kuchochea utalili wetu. Kule Balozini peleka Maafisa hata Watano kutoka Wizarani kwako, wakawe waambata wa utalii ndani ya Balozi zetu, tusiwategemee Maafisa wa Ubalozi wafanye shughuli ambayo hawana taaluma nayo, peleka Maafisa kule ili wakasimamie shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo najua muda siyo rafiki nitachangia kimaandishi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Mhata, nilimtaja Mheshimiwa Benardeta Mushahu. Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge kwa uamuzi wake wa kugombea nafasi ya Urais wa Bunge la Dunia *(IPU)*. Mheshimiwa Tulia Ackson unastahili, unaweza, wote humu ndani tunatambua uwezo wako na tunataka dunia watambue hilo. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, akubariki

na akuwezeshe kupata nafasi hiyo ya Urais wa Bunge la Dunia. *We wish you all the best. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri ya bajeti lakini pamoja na kazi nzuri inayofanyika katika Wizara hii. Mheshimiwa Mchengerwa nakufahamu sana nikiwa kwenye Kamati ya Huduma nilikuona makali yako ukiwa kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na nina uhakika kwa kuwa sasa hivi unaye na Naibu Waziri ambaye ni makini mchapakazi, mnaenda kuipaisha hii Wizara, mnaenda kupaisha hizo sekta ambazo mnazisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana kipenzi chetu Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kushiriki kwenye Tanzania *the Royal Tour* ambayo sasa hivi imetuwezesha unaona wawekezaji wanaendelea kuongezeka, unaona watalii wanaendelea kumiminika na mchango wa utalii kwenye Pato la Taifa, umeongezeka. Tukumbuke kwamba kwa mwaka 2014 mchango wa utalii katika Pato la Taifa ilikuwa ni asilimia 4.4 tu, lakini kwa mwaka jana 2022 ulipaa mpaka umefikia asilimia 17.5. Watalii wameongezeka kutoka 1,700,000 mwaka 2021 mwaka 2022 wamefika 3,800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ahsante sana Mama Samia Suluhu Hassan, tunasema ahsante sana kwa mikakati mliyoweka Wizara imeanza kuzaa matunda. Ombi langu kwenu ni kwamba watalii wamekuja ndiyo sasa lazima tuweke tuhakikishe kwamba huduma wanazozipata wakiwa ndani ya Tanzania kwenye mahoteli, kwenye ndege, kwenye mbuga ni za kiwango cha hali ya juu, kusudi kesho na kesho kutwa watamani kurudi ndani aya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera tunawashukuru sana, mwaka 2018 mlipandisha yaliyokuwa mapori ya akiba yakawa Hifadhi za Taifa tukapata Burigi - Chato, tukapata Ibanda, tukapata na Rumanyika, lakini kasi ya kuziendeleza hizo hifadhi ni ndogo sana. Tulitegemea kwamba baada ya kuzipata uongozi wa Mkoa wa Kagera walihakikisha kwamba wamefanya operesheni mbalimbali, wakaondoa mifugo yote iliyokuwa

kwenye hifadhi hizo na mifugo mingine ilikuwa inatoka nchi za nje, uoto ukaongezeka wa asili, Wanyama wakaanza kurudi wanyamapori lakini na Serikali mkatusaidia kutuongezea wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacholalamikia ni kwamba hatuoni kama kuna kasi ya kuziendeleza hizo hifadhi, kwa maana ya kutujengea barabara, njia zile *routes,* kuweka mahoteli, tunaona kwamba bado. Unakuta sehemu nyingi ndani ya hifadhi hizo hakuna mitandao. Sasa mtu ameenda kutalii amefika kule labda kapata shida akitaka kuwasiliana na mtu ambaye yuko nje ya hifadhi hawezi kwa sababu hakuna mtandao, au vijana wenyewe siku hizi wanataka wajipige picha karibu na mnyama, arushe ile picha na yule mtu aliye nje ya hifadhi aone hawezi kufanya hivyo kwa sababu hakuna mitandao. Tunaomba *TANAPA* itekeleze mpango mkakati wa kuendeleza hizo hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tupatiwe wataalam, kwa Mkoa wa Kagera tangu kwenye Mkoa mpaka ngazi zote za Halmashauri zote hatuna Afisa yeyote anayehusika na utalii. Kwa hiyo, utakuta mara ni Afisa Utamaduni, mara ni Afisa wa Misitu ndiye anapewa lile jukumu, yaani hatuna yule ambaye anaweza kwenda kwenye Halmashauri akatetea hata haki *I mean* ule mpango wa kuendeleza utalii. Kwa hiyo, tunaomba tupewe hao kusudi tuweze kuendeleza utalii Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka jana Serikali mlituahidi kwamba sasa mnaenda kuchonga barabara kwenye hii Hifadhi ya Burigi - Chato lakini mkasema mnaenda kuanzisha utalii wa faru weupe kwenye hii Hifadhi ya Burigi - Chato. Naomba kujua kwenye bajeti hii kuna nini au kitu gani kimeshafanyika kwenye kuanzisha huo utalii wa faru weupe katika Hifadhi ya Burigi – Chato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiomba kama mkoa lakini na Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo *Eng.* Ezra Chiwelesa amekuwa akiliongelea sana kwamba sasa lile lango la kuingilia Burigi - Chato lipite mahali ambapo wale wataliii sasa watatakiwa wapite katikati ya Biharamulo wakati wanaenda kwenye kutalii huko Burigi - Chato. Kusudi waweze kuchochea uchumi ndani ya

Biharamulo Mjini, naomba kujua huo mpango umefikia wapi na nikuombe Mheshimiwa Waziri ukija kuhitimisha uniambie kwneye bajeti hii tulishapata hifadhi mpya zaidi ya moja Burigi - Chato ndiyo kuna mipango naiona kwenye bajeti, Je, hii Ibanda ya Kyerwa na Rumanyika ya Karagwe kuna mipango gani sasa ya kuziendeleza hizo hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tembo. Tembo wamekuwa tembo. Tembo tunawapenda, tembo ni maliasili tulipewa na Mwenyezi Mungu lakini sasa hivi wameamua kuhama kutoka kwenye hifadhi wanakuja mahali wanapoishi binadamu. Ukienda kule Missenyi kule Mabale, ukienda Karagwe kule Muramba ukaenda Kyerwa, ukaenda Ngara wanaingia kwenye mashamba, wanakula ndizi, haishii hapo hata na mgomba wenyewe anaula na anauchanachana unakuwa kama nyuzi. Wanaingia Kagera *Sugar* waanakula miwa ya Kagera Sugar, imekuwa ni kero, tunaomba msaada wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna nyani na ngedere. Sisi huko Uhayani huwa tunalima mahindi yanawekwa kwenye mashamba ya migomba, sasa hawavuni maana yake ni ngedere na nyani ndiyo wanakuja kuvuna. Hata ukienda pale Manispaa ya Bukoba unakuta ngedere na nyani wanatambaa hata kwenye miji, kwa sababu huku zamani kila Halmashauri ilikuwa na kitengo kinaitwa *bail in control,* ambapo kulikuwa na Maafisa ambao walikuwa nahusika kuwavuna, kuwaua na kuwapunguza na kuwarudisha hifadhini wale wanyamapori wakali na wale ambao ni wasumbufu wanaharibu mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hicho kitengo hakipo ndiyo maana hawa wanyama wanatawala na hakuna anayewashughulikia, tunawaomba mtuletee wataalam ambao wamesomea mambo ya wanyamapori ambao wanajua sasa ni kwa namna gani wanaweza kuwarudisha huko wanakotoka kusudi tusiendelee kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebahatika na Mwenyezi Mungu akatupa vivutio vingi vya utalii. Nina uhakika kwamba kila Mkoa, kila Wilaya ikiwemo na Kagera kuna vivutio vingi, kwa sababu ya muda leo nitazungumzia vivutio vitatu tu.

Mkoa wa Kagera tuna visiwa 48 ndani ya Ziwa Victoria ambavyo viko Mkoa wa Kagera. Kati ya hivyo 48 ni 27 vina watu wanaishi visiwa 21 hakuna mtu anayeishi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ni *opportunity* ya kuweza kuanzisha utalii. Wizara tuende mkajenge mahoteli kule tuweze kuanzisha *picnic sites,* tuweze kuanzisha uvuaji wa Samaki - *sports fishing,* tuweze kuwa na utalii wa boti, mtu anasafiri kwenye boti anaendesha mwenyewe mtumbwi, anaenda upande ule kwenye kisiwa anastarehe na kurudi. Kwa hiyo, tunaomba tufanyiwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo misitu mikubwa, tunao msitu mmoja mkubwa unaitwa Minziro, huu msitu ni mkubwa una hekta zaidi ya 25,000 na inasadikiwa kulikuwa na nyoka mkubwa sana ambaye anaishi zaidi ya miaka 209 na huyo nyoka aliweza kuishi kwa siku zaidi ya 68 bila kula chakula anakunywa labda maji tu na katika msitu huo huo, nina uhakika watu wangependa kuja kuona msitu huo unafananaje. Lakini katika msitu huo huo kuna *species* nyingi aina ya miti mingi mamia na mamia na kati ya hayo mamia aina 12 ya miti hiyo inapatikana Tanzania tu, kwa hiyo nina uhakika watu wengi wangependa kuja kufanya utafiti na kuiona hiyo miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao vipepeo wa rangi zote, tuna aina zaidi ya 600. Wanene, wembamba, wekundu, weusi, rangi zote wanapendeza ni kivutio tosha. Tunao ndege zaidi ya *specie* 238 na kati ya hao hizo *specie* 51 zinapatikana Mkoa wa Kagera tu. Huu msitu ukiendelezwa unaweza ukatuvutia utalii na watu wengi wakaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtufungulie utalii wa fukwe, Mkoa wa Kagera kwenye Ziwa Victoria tunayo fukwe moja nzuri sana ndefu. Ukianzia kule Muleba Kusini, ukaja Kaskazini ukaenda Kusini Kaskazini ukaja Bukoba Vijijini, Manispaa ya Bukoba ukaenda mpaka Missenyi ni fukwe moja ndefu sana ina mchanga mweupe mzuri na mawe mazuri ya ajabu. Mkiweza kuuendeleza ule ufukwe unaweza vilevile ukatuvutia utalii ambao utachochea kipato cha ndani ya Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. Nilimtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Joseph Kakunda na baadae ajiandae Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na tuko hapa leo tuna afya nzuri sana. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa filamu ya *Royal Tour*, filamu ya *Royal Tour* imefungua nchi yetu imetuongezea watalii wengi sana, tatu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Ndugu Mchengerwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana leo na *I think* ndiyo wakati pekee nitaongea leo *a bit calm,* kuliko wakati mwingine wowote. Utalii na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni sekta muhimu sana inaongezea nchi yetu mapato lakini inasaidia kufungua nchi yetu, kuna uhifadhi vilevile ambayo ndiyo *conservation,* sasa na mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri utalii na uhifadhi ni vitu viwili tofauti. Uhifadhi ndiyo *hard core* ya uhifadhi lakini utalii ndiyo *soft part, the business element,* sasa hivi ni vitu viwili tofauti tukivichanganya sana pengine tutashindwa ku - *appreciate* tofauti zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mtu anayelinda maeneo ambaye ni mtaalam wa wanyamapori, ambae atakuwa natuambia *study* za wanyamapori zikoje, atakuwa anapambana na majangili huyo huyo mtu ndiyo atuuzie kweli hifadhi zetu *the business element?* Mimi siamini hivyo. Mheshimiwa Waziri hebu angalia tengeneza timu zako, timu inayo - *deal* na watalii peke yake na timu ambayo inafanya mambo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya hivyo nadhani tutapata namna ya kufaidika vizuri zaidi. Wale ambao ni wahifadhi tena ambao ni Jeshi USU siku hizi, tena ndiyo kabisa wanatakiwa wao

waanze kupambana na majangili, mimea vamizi, waandike vitabu, waandike *articles* waende kwenye *scientific conferences,* wajaribu kuuza nchi yetu kwa *scientific element part* ya *conservation.* Watu ambao watafanya kazi ya utalii ambayo ndiyo *business element,* lazima tuwe na timu ambayo ni tofauti kidogo ambayo ni *sharp* ni *creative* ni *innovative,* kwa sababu biashara tunashindana na wengine *it is about competitiveness,* lazima tuwe na timu nyingine, hebu mui–*organize* kidogo tunaweza tukanufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na pengine ndiyo maana leo *am very calm* na kauli zako mbili ulizotoa baada ya kuteuliwa. Umesema wananchi ni wahifadhi namba moja, lakini ukasema vilevile watu wa hifadhi watapimwa kutokana na wanachosema wananchi juu yao. Mheshimiwa Waziri hizi kauli zote mbili ukishikilia unaweza ukawa *the best Minister of our life* tangu nchi hii ipate uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama mahusiano kati ya wananchi na wahifadhi wanyamapori maeneo ya hifadhi ni mbaya, Mheshimiwa Waziri Ilani ya Chama cha Mapinduzi nikupe tu *comfort* ukurasa wa 113 inazungumzia kwamba tulisema tutaimarisha mahusiano kati ya wahifadhi na maeneo ya hifadhi na wananchi na Ilani inasema kabisa hivi na ninukuu "kuimarisha mahusiano kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi na kulinda mali za wananchi na wananchi wenyewe, vilevile kutoa elimu. Ili sekta ya Maliasili iwe endelevu ni lazima ijali haki na maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ukienda na hizi mbili, kwa kweli utakuwa *an exceptional Minister of our life* nikuambie tu ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine Mheshimiwa Waziri, unajua kati ya maeneo ambayo bado tuna *elements* za kikoloni ni kwenye eneo hili la *conservation.* Nilikuwa naangalia Sheria ya *Fauna Conservation* ya mwaka 1951, nikakutana na kipengele ambacho kinatutesa mpaka leo, hiki cha *forfeiture.* Ku-*forfeit* magari, mifugo ya wananchi pale ambapo wanaingia kwenye hifadhi zetu. Kumbe nikagundua

kwamba ilianza wakati ule wa ukoloni, *forfeiture! Fauna Conservation, Section 53,* utakutana nayo na bado ipo mpaka leo kwenye Sheria yetu ya Wanyamapori. Mheshimiwa Waziri lazima tu-*decolonize* hizi sheria na *policies* ambazo zinaendelea kutesa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuingia kwenye hifadhi ni kosa, lakini isiwe sababu ya mtu kuwa maskini. Mimi na-*subscribe* na *conservation* ambayo, na kauli zako zina-*support* kwamba, *conservation for people and by the people*. Hiyo tukienda hivyo tutafanya vizuri sana kwa sababu, *after all* hifadhi *for whose benefit?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni wananchi hawa wa Tanzania hawa wanufaika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ukienda hivyo tuangalie sheria hizi ambazo zina-*colonize*. Sasa kwa mfano siku hizi ng'ombe wakikamatwa watu wanafanya *compound* halafu una-*charge* laki moja kwa kichwa cha ng'ombe, *which is fifty percent of the price*. Sasa kama tukiamua kwenda kwa njia hiyo, basi tukiwa tunakamata magari *on traffic offences* kama gari lako ni *Vits* tuseme *fifty percent* ya bei ya hili gari tu-*charge* kama *fine* kama ndiyo tunataka kwenda huko, lakini mimi siamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lilishasema *maximum fine* na *minimum fine,* una-*charge* kwa kosa siyo kwa kichwa cha ng'ombe. Hapa nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo hapa kwamba, Wizara yenu mkapitie na mkaangalie sheria. Haiwezekani ng'ombe ni laki moja na nusu, halafu unataka kunichaji laki moja kama *fine,* siyo sawa! lakini Mheshimiwa Waziri kuna ng'ombe wengi sana wamekatwa kwenye maeneo haya, kuna watu wamekwenda wameshinda kesi Mahakamani, lakini mpaka leo wananchi hawa hawajapewa mifugo yao na wapo wengi sana. Hebu wewe tizama na uangalie vizuri sana na pengine ukae na timu yako tena mu-*re-evaluate* hii kushika ng'ombe kila wakati. Mtengeneze mahusiano, mkitengeneza mahusiano mimi nadhani hakutakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Dkt. Mbunge wa Muleba nae ana shida hiyohiyo, wananchi wake

wanahangaika kila mahali. Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri tengeneza mahusiano haya, wananchi wakifurahi uhifadhi utaendelea na sote tutafurai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza unajua wakati mwingine ukipata *report* za hawa wataalam wako wa maliasili na utalii, achana na hizo ripoti njoo *field* tena, tembea. Nenda kaongee na wananchi wale, tembelea maeneo yale, utanufaika zaidi kwa kuwasikia wananchi wanasema nini kama ulivyofanya Serengeti. Hiyo ilikuwa ni *innovation* kubwa na nzuri sana, Mheshimiwa Waziri ukiendelea hivyo itakuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni *WMA*. Mheshimiwa Waziri hii *strategy* ambayo umeianzisha na nikushukuru kwamba, juzi mmezindua *strategy* ya kuendesha *WMA*. Nami najua wewe kwako una *WMA* hata mimi nina *WMA,* wananchi hawa wamefanya mambo mengi sana na kutoa ardhi hizi ziwe kwenye *WMA* na wao sasa waanze kushindana na mbuga za wanyama na maeneo mengine yote yenye *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuombe Mheshimiwa Waziri, hapa tuna Wabunge wengi sana wa *WMA,* tufanye mpango, tengeneza *group* la Wabunge wa *WMA*. Zile *WMA* zi-*protect* kutokana na wale *investors* ambao wengine wakorofi, wanawashitaki Mahakamani. Ukifanya hivyo nadhani sekta hii itafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naunga mkono hoja na ninakutakia kila la heri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nianze kwa pongezi, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anazipa kipaumbele sekta zetu za uzalishaji na hasa sekta hii ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana alifanya *Royal Tour* ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa sana kuongeza mapato kwenye hii sekta. Nami nitoe wito kwa Mawaziri wetu hawa wawili, niwakaribishe Sikonge waje wafanye *Royal Tour* ya kwao sasa kwa Sikonge ambayo naamini itatusaidia kutuinulia mapato kutoka kwenye hifadhi zetu na utunzaji na kutoa elimu kubwa zaidi kuhusu utunzaji wa hifadhi zetu Sikonge. Kwa hiyo, ninawakaribisha mwezi Julai au mwezi Agosti njooni Sikonge. Najua Mheshimiwa Waziri tangu azaliwe hajawahi kufika Sikonge, namkaribisha afike Sikonge kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza kwa nukuu za Katiba. Katiba yetu Ibara ya 8(1)(b) inasema: *"Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi."* Ibara ya 9(h) Katiba yetu inasema kwamba: *"Aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini."* Yaani ni Serikali itafanya hivyo, itasimamia hilo. Ibara ya 9(i) inasema kwamba: *"Matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada za kuondosha umaskini, ujinga na maradhi."* Na mwisho 11(1) Katiba inaelekeza kwamba: *"Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya kila mtu kufanya kazi halali."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma Biblia vilevile. Katika Biblia Isaya 32:18 unasema: *"Na Watu wangu watakaa katika kao la amani; na katika maskani zilizo salama na katika mahali pa kupumzikia penye utulivu,"* lakini Mheshimiwa Mchengerwa unafahamu katika Quran Tukufu pale Mwenyezi Mungu aliposema *"Alladhi Ja'ala lakuml-ardh firshan wassama'a binaan."* Amekufungulieni ardhi kuwa kama busati na akateremsha maji kutoka mbinguni ili humo muweze kupata riziki zenu. Kwa hiyo, sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya binadamu kwa sababu, hii ndiyo sekta ambayo kila binadamu anaitegemea kwa ajili ya maisha yake na humo ndiyo tunapata hewa safi na humo ndiyo tunapata kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunazo hifadhi Tisa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, hifadhi Nne za Serikali Kuu ambayo ni Iswangala, Nyahwa, Itulu *Nature Reserve* na

*Iyunga East,* na misitu mitano ya Halmashauri ambayo ni Pembamkazi, Ugunda, Wala, Sikonge na Goweko, tunaelewa maana halisi ya utunzaji wa hifadhi zetu. Vilevile tuna hifadhi moja iko chini ya *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba masuala ya kufanya kazi wananchi wetu katika misitu yetu yanakumbana na changamoto nyingi sana. Sisi tuna kazi nyingi tunazifanya kwenye misitu, kufuga nyuki, kurina asali, kuvuna miti, kuvuna uyoga, kuvua samaki kwenye mito iliyomo humo na kazi nyingine. Sasa ili mtu aingie mle afanye kazi hizi halali lazima apate kibali cha mamlaka, taratibu za kupata vibali wakati mwingine zimekuwa ngumu sana zinasumbua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri aangalie hizi taratibu za kupata vibali kwa wananchi wetu, kufanya kazi za misitu, zirahisishwe na wananchi waelimishwe ili wapate vibali kwa njia rahisi waweze kufanya kazi zao za kiuchumi katika misitu yetu. Sheria nyingi na kanuni nyingi kwa kweli zimekuwa siyo rafiki, hilo eneo nalo lilivyo Mheshimiwa Waziri naomba lifanyie kazi kama Katiba ambavyo imeelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika misitu ya *TFS* ili mwananchi aingie mle kwa mfano ana kazi ya kuweka mizinga yake, ili aingie mle kwenye misitu anapewa kibali. Kibali analipia, lakini vilevile kila siku lazima alipie shilingi 2,000. Kwa hiyo, kama anaingia yeye na watoto wake wawili anaingia yeye analipa shilingi 2,000 kila siku na watoto wake wawili kila mtoto shilingi 2,000, maana yake ni kwamba, kama atakaa siku 50 anatakiwa alipe shilingi 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shilingi 300,000 kwa wananchi wetu wa kawaida, maskini wa vijijini, ni nyingi sana. Je, hata atakapopata mazao yake atauza apate shilingi ngapi? Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. Kwenye Misitu ya *TAWA* ndiyo gharama ni kubwa zaidi kuliko hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu suala lingine ni pikipiki. Mimi nimesikiliza hoja nyingi za Serikali kuhusu kuzuia pikipiki katika misitu yetu, sawa, lakini hivi Mheshimiwa Mchengerwa nikupe wewe

baiskeli utembee kilometa 200 utaweza kweli? Wananchi wetu wanapata shida kubwa sana kutembea kwa baiskeli kilometa 200 hadi 300 kwenda kwenye mizinga yao. Mimi nilikuwa naomba sana tuende na wakati, kwa nini tusiweke taratibu za unampa mtu kibali anakwambia mimi nitatumia pikipiki halafu afuatiliwe. Kama hiyo pikipiki ataitumia vibaya aadhibiwe kwa kuitumia vibaya pikipiki, lakini siyo alazimishwe kutumia baiskeli karne hii, kilometa 250, kilometa 300, akitoka kule amerina asali aweke debe lake kwenye baiskeli kilometa 200, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa huko ni kuwatengua viuno wananchi, naomba sana hizi taratibu ziangaliwe kwa umakini na zirahisishwe na ikiwezekana hivi vyombo vya kutumiwa kwenda porini na kubeba mizigo viruhusiwe vyombo vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi kuhusu Jimbo. Kwanza naipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya mwaka 2019 ambayo ni uamuzi wa kwanza wa Serikali ulikuwa ni kufuta mapori 12 ambayo yalikuwa yamekosa sifa, haya mapori yana ukubwa wa ekari 707,659 siyo jambo dogo lazima tuipongeze Serikali, vilevile Serikali ilifuta misitu 12 yenye ukubwa wa ekari 46,755 hii ni pongezi kubwa sana kwa Serikali, vilevile uamuzi ambao ni mgumu kabisa ambao Serikali iliufikia ni kuhalalisha vijiji 975 vilivyokuwa ndani ya hifadhi, huo ni uamuzi mkubwa sana, Serikali inahitaji kupongezwa sana kwa uamuzi huo. Pia kuondoa zile mita 500 ambazo zilikuwa ni *buffer zone* ulikuwa ni uamuzi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sikonge vijiji na vitongoji ambavyo vimehalalishwa navitaja, Miseseko kaya 533, Isenga kaya 527, Mwanzagata kaya 418, Myesuu kaya 314, Simbamdeu kaya 271, Ngakalo kaya 196, Kayemimbi kaya 193, Manyanya kaya 115, jumla kaya 2,567 zenye jumla ya wakazi 25,000 zote hizi Serikali ilisema hizi zirudi kwa wananchi. Hili jambo siyo dogo ni kubwa sana Mheshimiwa Mchengerwa, naomba simamia maamuzi haya yatekelezwe kikamilifu kama ambavyo Serikali iliamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nimeona kwamba, kuna baadhi ya maombi yameanza kufanyika huko kupitia baadhi ya wataalam wetu wanaanza kutaka kupindua ule uamuzi. Ule uamuzi ulikuwa mzuri sana na wenye tija, haiwezekani watu

wamekaa mle miaka 25 miaka 30 halafu leo hii uje uwaondoe kwa hiyo, uamuzi wa Serikali ulikuwa sahihi, ninaomba sana simamieni ili wananchi wetu waendelee kupata maslahi kama ambavyo walikuwa wametegemea kwenye uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchengerwa nikuambie nakuunga mkono kwa asilimia 100 kwenye kazi zako zote, wataalam wangu kule Sikonge nawaunga mkono kwa kazi zao zote, ninachoomba tu taratibu zirahisishwe na mambo yakae vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, baada ya ziara ya Mawaziri Nane timu ya Serikali ya Wataalam, watu wa ardhi, watu wa idara ya usalama na maliasili walitembelea mipaka yote na wakakubaliana kwamba, hapa ndiyo mwisho, hawa waliozidi huku mbele wanatakiwa warudi nyuma. Sasa kule ambako walisema hapa ndiyo mwishio na wakaweka rangi ninaomba Serikali ikaweke *beacon* hata kesho ili wale ambao wako mbele kule tuwaelimishe warudi nyuma waache hifadhi na wananchi wa Sikonge watashirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba, misitu inalindwa vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la mwisho. Serikali iruhusu kutoa eneo la hekta 650 kwenye eneo la Bwawa la Uluwa ambalo limeingia kidogo kwenye hifadhi ya Ipembampazi. Hii hifadhi ni ya kwetu Halmashauri siyo ya Serikali Kuu ni ya kwetu Halmashauri na Baraza la Madiwani limeomba Waziri wa Maliasili na Utalii, utupe hizo hekta 650 ni eneo letu, lakini tunazingatia heshima ya kuheshimu sheria kwamba, msimamizi wetu, mlezi wetu ni Waziri wa Maliasili na Utalii, basi tunaomba Mheshimiwa Waziri kwa mamlaka uliyonayo utupe hizi hekta 650 ili wananchi wajikimu kwa kulima mpunga kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alilenga eneo hilo liwe ni la mradi wa kilimo cha umwagiliaji tangu mwaka 1976 alipotembelea eneo hilo. Alizindua bwawa lile akasema mwaka 1977/1978 tutaleta fedha kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji, lakini bahati mbaya sana tukaingia kwenye vita, fedha zikachelewa, zimekuja hivi karibuni. Kwa hiyo, tunaomba sana ruhusa yako wakati utakapokuwa unahitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Ahsante sana, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Nilimtaja Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nami nijielekeze kwenye kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Nampongeza kwa sababu ameanza vizuri, ameanza kwa usikivu, ameanza kwa kujishusha kwenda kuwatumia Watanzania kwa kuwasikiliza. Mheshimiwa Mchengerwa hongera sana. Endelea kuwa *humble* katika kuwatumikia Watanzania hawa, endelea kuwa *humble* katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nizungumzie hali yetu kule Mkinga. Tuna changamoto kubwa sana ya uvamizi wa tembo kwenye Wilaya yetu ya Mkinga. Wilaya ya Mkinga ina Kata 22, hivi ninavyozungumza Kata 13 tembo wanavuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni maeneo yaliyokuwa yanashambuliwa sana ni Daluni, Bwiti, Duga, Gombero na Mwakijembe. Haya ndiyo yalikuwa maeneo yaliyokuwa yanashambuliwa kwa kiasi kikubwa, lakini leo hii tunapozungumza Kata nyingine Barongo Kasera, Mtimbwani, Doda, Moa, Mapatano, Duga Sigaya, nasikia Maramba wamepita na vilevile Mnyenzani wamepita, hali ni mbaya sana. Hali ni mbaya kwa sababu wananchi wanapoteza…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna Taarifa Mheshimiwa Kitandula.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba anavyozungumza tembo hali mbaya, kwenye Jimbo la Bunda karibu Kata zote tembo wako barabarani saa hizi, wako makundi 40, 20, 30, Kata zote toka usiku mpaka leo saa hizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge taarifa ni moja.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda huu ni mdogo. Waheshimiwa Wabunge waache wenzao watumie muda waliouomba kuchangia. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, kuna taarifa nyingine hapa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa inakuwa ni moja. Hajaanza hata kusema taarifa inatoka wapi? Muache aseme kwanza. Mheshimiwa Kitandula naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, daah, mambo mengine yanaudhi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkinga wanataabika, tumeleta maombi baada ya mazao yao kuharibiwa ili waweze kupata fidia, huu ni mwaka wa tatu hakuna kifuta jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Kamati ya Siasa ilikuwa inafanya ziara *feedback* waliyoipata kutoka kwa wananchi, wananchi wamekata tamaa. Wananchi wanasema Serikali inathamini tembo kuliko wananchi, hili si jambo zuri kwa Serikali

yangu ya Chama cha Mapinduzi. Twendeni tukawasaidie wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni, mazao yaliyokuwa yanaathirika ni mahindi na mikorosho, lakini sasa hali imekuwa mbaya kwenye zao la mkonge. Tembo sasa mkonge ndiyo imekuwa, sijui nisemeje, wanavuruga kwelikweli. Chama cha Wakulima wa Mkonge kule Mkinga kimeleta malalamiko haya nimeyafikisha, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Kaka yangu Ngenya tukiwa kwenye bajeti hapa akawa ananitania ananiambia Mheshimiwa Mbunge, naendelea kuwa maskini. Mwaka huu nilikuwa nategemea nianze kuvuna mkonge, tembo wamemaliza shamba zima. Hali, Mheshimiwa Mchengerwa, ni mbaya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri, nilikuja kumueleza mwanzoni mwa mwezi Mei, baada ya siku mbili akaongeza kikosi pale Mkinga. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana, kikosi kile kilienda tarehe 19. Lakini kwa ukubwa wa tatizo hili kikosi kile hakitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tulikuwa tunazungumza asubuhi, tembo wamevamia Mavovo, wamekula mahindi ya wananchi, Kikosi kile kimeitwa kiende Muheza kwenda kufukuza simba, kwa hiyo kule shughuli inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nakuomba tukimaliza Bunge hili hebu tuende Mkinga ukaone hali. Hali ni mbaya. Mlituahidi kwamba mtakuja kufundisha vijana kumi kwenye kila kijiji, mtawapatia vifaa ili watusaidie tuwe na usimamizi wa karibu, jambo lile halijafanyika, tunaomba fanyeni jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikosi hiki kilichowekwa ni cha muda, tunahitaji kuwa na kikosi pale cha kudumu kwa sababu tatizo ni kubwa. Tunapata tembo kutoka Tsavo - Kenya, tunapata tembo kutoka Mbuga ya Mkomazi. Njooni mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni changamoto ambayo imeletwa na hili tunalolifanya la kutatua migogoro, hatujalifanya vizuri kule Mkinga. Kata ya Mwakijembe kuna kilio, ushirikishaji haukuwa mzuri. Tarehe 30, ilikuja timu kule kwenda kufanya tathmini, timu ile haikushirikisha hata wenyeviti wa vijiji, tunawezaje kufanya mambo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wale wanapita wanawaambia wananchi ukifika mwezi Julai mnaondoka. Tunazalisha taharuki bila sababu ya msingi, tunachukua maeneo yao hatuwaambii fidia tunayowapa ni ipi! Mheshimiwa Mchengerwa, nakuomba hebu tuende Mkinga tukaondoe changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya kazi nzuri sana mwaka 2017, tuliwashirikisha wananchi tukapata muafaka wa Kimkoa na Kitaifa, tukasubiri jambo lile sasa tuende tukalifanyie kazi. Kikosi kazi mlichotuma kimekwenda kutupa yale yote tuliyokuwa tumekubaliana, kimekuja na maamuzi yao tofauti ambayo hawakushirikisha wananchi, hatuwezi kufanya hivi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji kule wanazuiwa, hata sasa wanaambiwa hawatapeleka mifugo yao kwenda kunywa maji kwenye Mto Umba, mto ambao unatiririka kwenda Kenya, wenzetu wananufaika, sisi tunazuia watu wetu. Tunawezaje kufanya mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ile ya kwanza ilipokuja ilijiridhisha kwamba eneo lile hakuna uwezekano hata wa kuchimba kisima. Kwa hiyo, eneo pekee ni kwenda kunywa maji kwenye Mto Umba. Leo tunawaambia wafugaji wale kwanza tunachukua maeneo yao, hatuwaambii fidia tutakayowapa ni ipi, halafu tunawazuia wasiende kunywesha maji kwenye maeneo yale. *This is…*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Nilimtaja Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Daimu

Mpakate, Mheshimiwa Emmanuel Shangai na Mheshimiwa Aida Khenani wajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naanza pia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa mawili. Kwanza, kama ambavyo tumesema siku zote, nampongeza sana kwa matokeo chanya yanayotokana na ile *Royal Tour*. Tumeona ongezeko la utalii na katika taarifa imeonesha kwamba kuna ongezeko la utalii kwa asilimia 123. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaendelea kuidhinisha fedha kwenda katika miradi ambayo itaendelea kuchochea na kusisimua sekta ya utalii. Kwa mfano, watu wa Iringa tunamshukuru na kumpongeza sana kwa sababu ameendelea kuidhinisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa pale Iringa ambapo utakapokamilika utachochea sana utalii hasa kusini kwa maana ya Mbuga ya Mikumi na Mbuga ya Ruaha. Kwa hiyo, kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake na vyombo vyao vyote. Watu wengi wamempongeza sana Mheshimiwa Waziri alivyokuwa amefanya vizuri kwenye Wizara ya Michezo, nami napenda tu niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, alifanya vizuri kwa sababu pia ni mwanamichezo, pamoja na kuwa sasa hivi ametukimbia kwenye *Bunge Sports Club,* ndiye aliyekuwa namba tisa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michezo ya pale Mombasa ya Mabunge ya Afrika Mashariki, yeye ndiye alichukua kiatu cha dhahabu pale Mombasa, lakini baada ya kuja mdogo wake, Mheshimiwa Sanga, naona amerithi ile nafasi kutokana na majukumu mengi aliyonayo Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana. Kwa kutumia michezo, ninapenda kushauri kwamba tuendelee kutumia michezo katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza sana chama cha wanaosimamia uratibu wa mshindano ya magari. Tarehe 14, Mei walifanya mashindano ya magari katika Msitu wa *Sao Hill* kama sehemu pia ya kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza sana waandaaji wa *Great Ruaha Marathon.* Hii ni mbio ambayo itakimbiwa Julai, 08. Yaani *marathon* hii itafanyika ndani ya Mbuga ya Wanyama ya Ruaha, maana yake ni katika kushirikisha michezo kuendelea kutangaza utalii. Pia Mheshimiwa Waziri na timu yako, nikuombe, kwa kutumia wataalamu wako, wako baadhi ya watu wanapendekeza na kushauri kwamba kama inawezekana na kama taratibu za kitaalamu zinaruhusu, basi kule kwenye mbuga zetu kuwe hata na viwanja vidogo vya michezo kama mpira wa kikapu, mpira wa *volleyball*, mpira wa pete, na hata viwanja vidogo vya kucheza mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watalii wanakuja wanatamani baada ya kutembea waende kufanya michezo ya namna hiyo. Kwa hiyo, kama taratibu za kiikolojia zinaruhusu, naomba Mheshimiwa Waziri uweze kulichukua jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwa, kwa kutumia michezo, naipongeza sana Timu yetu ya Wanawake ya *Under 17,* nawapongeza Tembo *Warriors,* wewe mwenyewe ulikuwepo kule Uturuki, pia nawapongeza wanariadha, nitawataja baadhi tu, akiwemo Alphonce Simbu na Gabriel Geay ambao wamekuwa wakishiriki katika mashindano mbalimbali ya *marathon. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na mimi nikushauri na timu yako na kupitia *TTB,* sina shaka kabisa na Damasi Mfugale, ni mtu ambaye ni *open-minded,* hebu tujaribu pia kuwekeza katika michezo kama sehemu ya kutangaza utalii. Kwa mfano, ukiwekeza kwa mwanariadha ukamsaidia vifaa, ukamsaidia *training,* kuweka kambi, ukamsaidia na walimu wa kuwasaidia kama timu ya watu watano, anapokwenda kushiriki kama *Boston Marathon,* ile tu kushiriki ni mvuto kwa Taifa letu, inaongeza kuchochea kuvutia watalii katika Taifa hili. Kwa hiyo,

naomba nikuombe pia utumie michezo katika kutangaza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nijielekeze kwenye sekta ya misitu. Watu wengi wanadhani kwamba misitu ni mbao tu, lakini mimi na wenzangu kutoka kwenye maeneo ya misitu tunapenda kutumia neno mazao ya misitu. Kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu pamoja na mbao, juzi tumepitisha hapa Bajeti ya Wizara ya Nishati, wamesema watatupa vitongoji 15 kila Jimbo, maana yake ni vitongoji kama 3,000 hivi. Katika kufanikisha ndoto hiyo ya kufikisha umeme tutatumia nguzo, ni mazao ya misitu. Lakini tuna ujenzi katika Mji wetu wa Serikali, katika kujenga pale tunatumia milunda, mbao, *marine board,* hayo ni mazao ya misitu. Kwa hiyo hii sekta ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mafinga, Mufindi na Njombe, kuna wawekezaji wakubwa ambao wametoa ajira kubwa sana kwenye viwanda vya *plywood*. Waheshimiwa Wabunge, niwafahamishe kwamba katika miti pia kuna utomvu, kuna makampuni yanagema utomvu, hayo ni mazao ya misitu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba wanasema kwamba sekta ya mazao ya misitu inachangia asilimia tatu tu ya Pato la Taifa, siyo kweli, kwa sababu wao wanangalia tu ule mti ukishatoka kuwa mti basi wamemaliza mchango wa sekta ya mazao ya misitu. Lakini sekta ya misitu ni pana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri kutembelea uone uwekezaji uliofanywa na Serikali, lakini na makampuni na watu binafsi. Halafu nikuombe tembelea viwanda vya mazao ya misitu na baada ya hapo kutana na wadau wa sekta ya mazao ya misitu. Hapa yapo mambo ambayo mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri na timu yako kuweza kuyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni suala la kurejesha kile ambacho makampuni yanakipata kwa jamii. Kwa kweli, napenda kuwapongeza sana *TFS,* wamekuwa wakishirikiana nasi,

wametujengea mabweni, wameshiriki nasi kuboresha mazingira ya soko letu pale Mafinga, lakini makampuni ambayo yananufaika na sekta ya mazao ya misitu, bado hatujaiona *Corporate Social Responsibility.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri na timu yako, mimi nawaamini sana, kama ambavyo tumefanya kwenye sekta ya madini na akina Mheshimiwa Doto, hebu tuje na utaratibu ambao hii sekta pia ya mazao ya misitu kile inachopata sehemu irejeshe kwa jamii, siyo tu wabaki *TFS* ndiyo warejeshe kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niwaombe mshirikiane na Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Kuna hiki kitu wananchi wetu wanatuuliza mambo ya hewa ya ukaa, tunaambiwa kwamba kuna fedha nyingi duniani zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, sasa sisi tumepanda miti ya kutosha, wananchi wamehamasika. Nitatoa pongezi hapa kwa wenzetu wa *FDT,* kwa wenzetu wapanda miti kibiashara, wamekuwa wanatoa elimu na miche kwa wananchi kama ambavyo wanatoa *TFS*. Wananchi wameitikia, lakini tunauliza, je, katika suala zima la hewa ya ukaa, nafasi yetu Wanamafinga, Wanamufindi, Wanairinga, Wananjome, iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe ushirikiane na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), je, na sisi, kwa sababu tunachangia sana ku-*regulate* haya mabadiliko ya tabianchi. Kwa kupanda miti maana yake tunachangia sana, kwenye mambo haya mazima ya kuleta *oxygen* na hewa safi, lakini pia tunatunza vyanzo vya maji. Kwa hiyo, nikuombe sisi kwenye kipengele hicho tutanufaika kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nitumie pia nafasi hii kuwapongeza watu wa *Ebony FM* Radio, katika kutimiza miaka yao 17 wamejitolea kuhamasisha kupanda miti 1,500,000. Kwa hiyo, unaweza kuona jinsi ambavyo hamasa iko juu sana. Tuendelee kuwaunga mkono lakini tuone wananufaika vipi na hewa ya ukaa, wananufaika vipi na hiyo *CSR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REGROW,* Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu nilikaa naye, nashukuru alinipa muda wa kutosha, nilimweleza. Ninaomba tumtendee haki Mheshimiwa Rais. Mradi huu wa *REGROW* sasa ni mwaka wa tano. Mradi huu aliuzindua Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais Tarehe 12 Februari, 2018 wadau wote na sisi watu wa Iringa na Mikoa yote ya kusini tulikuwepo katika shughuli hiyo, lakini lazima tukubaliane kumekuwa na kusuasua kwenye utekelezaji wa huu mradi. Mimi nakuamini na timu yako mkijipanga tutakavyouboresha huu mradi yako mambo ambayo yataendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufanya biashara ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona umeeleza mambo ambayo yanatarajiwa kufanyika hebu yafanyike kwa haraka. Nasi tunasema watu wa utalii Kusini, kwamba kama ambavyo tumesema Iringa ni kitovu cha utalii na Mkuu wa Mkoa wa Iringa na timu yake, nawapongeza sana, wameendelea kuhamasisha lile tukio la kila mwaka la utalii kusini. Hivyo, Mheshimiwa Waziri kwa hiyo hii *REGROW* hebu ifike wakati, narudia kusema, tumtendee haki Mheshimiwa Rais ambaye alizindua mradi huu lakini utekelezaji umekuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama ambavyo tunafanya katika masuala mengine ya utalii, kwa mfano wageni wanavyolipa leseni ni tofauti na wanavyolipa wenyeji. Hata tunapokwenda kwenye mbuga za utalii unapoingia pale getini kama ni Mikumi, Ruaha au Ngorongoro, anavyolipa mgeni tofauti na anavyolipa mwenyeji. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la uwindaji, mimi nashauri sana wawindaji wazawa ambao wengine wanawinda *for fun,* wengine wanawinda kwa sababu mbalimbali, ziwe za kibiashara, hebu tuweke utaratibu kwamba kwa mfano makampuni makubwa *giant* tuyatengee labda asilimia 70, hawa wawindaji wazawa na wenyeji tuwatengee asilimia 30. Wao washindane kama wao na haya makampuni yashindane kama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kiukweli wawindaji wetu ambao ni wazawa kwamba wataweza kushindana na haya makampuni ya ma-*giant* kutoka *America*, Urabuni, Ulaya na Asia? Itakuwa ni ngumu. Kwa hiyo mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri,

hawa nao wanahitaji kama Watanzania ku-*enjoy* na kufurahia hii *nature* ambayo tunayo, hii ambayo Mungu ametujalia. Kwa hiyo, ili wenyewe pia wa-*enjoy*, wape asilimia 30 washindane wenyewe na makampuni makubwa yape asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napongeza tena Timu ya Yanga kwa sababu ilichofanya pia imetangaza Taifa letu, imetangaza utalii, ndiyo maana nasisitiza kwamba kupitia michezo tunaweza kutangaza sana Taifa letu na kutangaza sana utalii. Wenyewe mmeona Algeria Waarabu wamelala na viatu na wameijua Yanga, wameijua Tanzania, wamelijua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mungu atubariki sana, awabariki Watanzania, ambariki Mheshimiwa Rais, abariki kila kilicho chema kwa ajili ya Taifa letu na maendeleo ya wananchi wetu wakiwemo wananchi wa Mafinga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Nilimtaja Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Aida Khenani pamoja na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai wajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi mchana huu kuongea mambo mawili, matatu kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuifanya hii sekta ifufuke na iweze kufanya kazi vizuri kwa kutuletea kipato na kuongezeka kwa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitaongelea jambo moja tu ambalo ni tembo. Wilaya ya Tunduru kuna hifadhi za misitu za *TFS* ziko nne, Wilaya ya Tunduru kuna Mbuga ya Selous, Wilaya ya Tunduru kuna Hifadhi za *WMAs* za wananchi ambazo zina kilometa za mraba 2,288. Hizi hifadhi Nne za *TFS* zina hekta 711,834.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hifadhi hizi karibu Kata 13 za Jimbo la Tunduru Kusini kati ya 15 zimepakana na hifadhi hizi, *WMAs* pamoja na Selous. Kata zaidi ya 15 zimepakana na hizi hifadhi upande wa kaskazini. Kwa hiyo Tunduru maeneo makubwa ni sehemu ya mapito ya tembo, ushoroba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wanaotusumbua Tunduru wanatoka Msumbiji, wanapitia Mbuga ya Mwambesi – Chingweli – Nalika wanaingia Selous. Wengine wanatoka Selous, wanapita Mbuga ya Nalika – Chingweli, wanapita Hifadhi ya Sadawara na kwenda Msumbiji. Kwa hiyo miaka yote hii ndiyo tabia ya hawa tembo ambao wanapita maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya adha hii ya tembo kila mwaka inapofika mwezi Aprili au Mei, Tunduru hatuna amani. Kipindi cha mwezi Mei peke yake Jimbo la Tunduru Kusini limepoteza watu wanne. Kijiji cha Kazamoyo wawili, pale Mbati mmoja na Kijiji cha Masuburu mmoja, wote wamekanyagwa na tembo, zaidi ya watu 2,000 wameathirika mashamba yao kwa sababu ya tembo kula mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na adha hii watumishi wa Halmashauri Maafisa Wanyamapori wako sita tu, na hifadhi ziko nne ambazo ni za *TFS* na humo ndimo ushoroba hawa tembo wanamopita. Hawa *TFS* watumishi wako saba tu na walio wengi wamesomea mambo ya majani na miti, wakiona hata nyoka wanaruka na kukimbia. Kwa hiyo, hii kero ni kubwa, hawa wenzetu wa *TANAPA* na *TAWA* wamejenga kituo pale, tunashukuru, kina watu nane. Kule Kalulu wapo kama sita, nao wanaendelea na Mbuga yetu ya Selous, sasa utakuta maeneo makubwa hayana askari wa kuweza kusaidia kufukuza hawa tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali. Adha ya Tunduru kufa watu, watu kuliwa mazao yao imekuwa ni kubwa, tuongezewe askari na vituo vya kuweza kuwafukuza hawa tembo. Naomba sana Wizara hii iangalie kwa kweli Serikali Tunduru inatukanwa sana, hasa Jimbo la Kaskazini upande ule unaopakana na Selous na hasa Jimbo langu mimi kwenye Kata 15 ambazo ni zaidi ya vijiji 45, wote hawa wanaathirika na tembo.

Mazao yao yanaliwa. Anatukanwa Rais, anatukanwa Waziri Mkuu, anatukanwa Mbunge, anatukanwa *DC* na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi wakati tunaandikisha sensa kuna vijiji walikataa kujiandakisha wakasema nendeni mkawaandikishe tembo ambao wanatusulubu kila siku. Ndipo tulipofika Tunduru! Naomba sana, hili jambo kwa Serikali ni dogo sana, ni kuongeza askari waweze kusaidia kuwafukuza hawa tembo, vilevile kuongeza vituo ambavyo askari watakuwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampa taarifa mzungumzaji kwamba katika michango yangu hata mimi nilisema kwamba tupatiwe askari kwenye kila Kata ambayo inaonekana ina ushoroba wa hawa tembo ili tuweze kuwadhibiti, Serikali wakasema kwamba utaratibu huo unaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii kwa kweli na ninapendekeza katika hilo kwenye Jimbo langu kila Tarafa angalau kuwe na kituo kimoja ambacho kitakuwa na *platoon,* siyo askari watatu au wanne, waweke *platoon* kwa sababu hili tatizo ni la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tembo wa Msumbiji wapo kwa sababu tunapakana na Hifadhi ya Nyasa. Hii hifadhi ni ya muda mrefu na kipindi kirefu na kutoka Mto Ruvuma hiyo hifadhi

ina zaidi ya kilometa 100 kwenda Msumbiji, kwa hiyo tembo wanakuja Tanzania kutalii, kuzaana na kula mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Tembo hawa wameshakuwa na ratiba ya mavuno yetu. Kipindi cha mavuno wanatoka Msumbiji wanakuja wanashambulia mazao ya wakulima. Njaa Tunduru ni kubwa sana. Nashukuru mwaka jana Serikali ilitupa mahindi ya msaada ya bei nafuu, tunaomba hali mwaka huu ni mbaya zaidi kuliko mwaka jana, haya mahindi yapelekwe tena mapema sana kuanzia mwezi wa nane wa tisa kwa sababu mazao yao mengi tayari yameshaharibiwa na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu wa wafanyakazi wa wanyamapori kuwa sita na huko *TFS* kuwa saba yaani wawili ni Maafisa wa Nyuki, watatu wanakwenda na miti hiyo na wawili hawa ni Maafisa wao kwa maana ya kwamba ni ma-*in charge*. Maeneo yote ya hifadhi hizi ni mapito ya ushoroba wa tembo sasa naomba hata *TFS* waajiri watu ambao watasaidia kufukuza hawa tembo au watoe mafunzo zaidi kwa hao waliokuwepo kwa sababu kama anamuona nyoka anakimbia. Kuna askari mmoja kule safari hii wakati wanafukuza Tembo amekimbia ameacha bunduki amekimbia kwa sababu ya kumwogopa tembo. Ni kwa sababu hana mafunzo yale ya kufukuza tembo. Naomba sana Mheshimiwa Mchengerwa, unajua nimekusumbua mara nyingi. Nashukuru wiki iliyopita umepita umeleta askari angalau wamefukuza wale Tembo wameenda Msumbuji lakini juzi wamehamia upande mwingine kwenye Kata nyingine. Nashukuru na jana wameenda, leo hii nimepata taarifa kuna sehemu nako wamevamia kwenye Tarafa nyingine. Naomba sana tupelekeeni hivi vituo haraka pelekeni askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache wake kwa Tunduru peke yake tunahitaji zaidi ya askari 40, lakini bajeti iliyopita mlisema mtaajiri *VGS* 600, tunashukuru tumepewa *VGS* nane tu, wanne Pori la Ngorika halafu na wengine pori lingine la Nyarika. Jambo hili kwa kweli bado halina afya. Kila pori linatakiwa angalau askari 20 watasaidia kwa sababu mapori haya ya vijiji yana wanavy vijiji Zaidi ya 26 ambavyo vinahudumia vinapakana

na hivi na nikwambie ukweli Tunduru Kata zaidi ya 28 kati ya Kata 39 zote zimepakana na hifadhi, aidha *TFS* au *WMA* au Mbuga ya Selous, kwa hiyo umuhimu wa kupeleka askari kule kwa ajili ya kusaidia kuwafukuza hawa wanyama ni mkubwa kwa sababu hiki kilio kipo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa sasa hivi nikikuletea meseji niliyoletewa kwa kweli utasikitika sana, najua tunataniana na uliniambia babu yangu utakoma safari hii. Naomba uniokoe hali kule ni mbaya chama kinaharibika Serikali inatukanwa. Tunaomba mtusaidie kupeleka Askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa kuwa hawa tembo tumeshindwa kuwadhibiti basi tunaomba kibali, kule siku hizi wenzetu Wangoni, sisi Waislam hatuli lakini wenzetu Wangoni wanakula nyama ya Tembo. Tupeni kibali tuwapunguze wale tuwavune au wachukueni wengine muwapeleke huko ambako tembo hawapo kwenye hifadhi hizo. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa jambo hilo kulifanyaia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu waathirika. Mpaka sasa tulilipa mwisho mwaka 2021, tumelipa 2020 na 2021, 2022 bado lakini katika hao waliolipwa wale walioathirika na wanyama wakali hawajalipwa. Kipindi hicho wamekufa watu kama 14 wote hao hawajalipwa katika ile milioni moja moja. Mabadiliko yale ya Sheria hebu ifanyeni haraka. Huwezi kulinganisha uhai wa binadamu kwa kumlipa kifuta jasho kwa milioni moja. Mheshimiwa Waziri kwa kweli hili ulifanye haraka, sheria ibadilike na hata fidia ya kwenye mazao kila heka mmoja mtu analipwa laki moja, ikiwa chini ya heka moja hawapati chochote. Kwa kweli tunaomba sana hii sheria iletwe mara moja, ibadilishwe watu wetu wanaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye jambo la askari mlifanyie hima, zaidi ya askari 40 tunahitaji ili wakatusaidie kuokoa hali ya maisha ya watu wetu. Nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpakate. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa filamu yake ya *Royal Tour* tunaona watalii wanaendelea kuja nchini. Nimpongeze pia Makamu wa Rais kwamba amefanya ziara kwenye Wilaya yetu ya Ngorongoro. Kiuhalisia amefika na *at least* wananchi wanaona kwamba Serikali itaenda kutatua baadhi ya changamoto ambazo zipo kwenye Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua kwamba wakati zoezi la uwekaji wa *beacons* kwenye eneo la Ngorongoro eneo la Pori Tengefu la Loliondo alishatoa *road map* Tarehe 08 mwezi wa Sita mwaka jana. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba baada ya eneo lile kuwekwa *beacon*s kwa sababu ilitakiwa kushirikisha wananchi na wananchi hawajashirikishwa katika zoezi la uwekaji wa *beacon*s, kwa hiyo, ilitakiwa kwamba baada ya zoezi lile kukamilika kwa sababu wananchi hawajashiriki, ni vizuri sasa tukakaa na wale wananchi tuone yale maeneo ambayo yameumia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mchengerwa kwa nia ya dhati, wewe siyo wa kulaumiwa leo ni wa kushauriwa kwa sababu kila bajeti ikipita tunakuja na Mawaziri wapya kwa hiyo nikuombee usiwe Waziri wa bajeti moja nikuombee uwe Waziri mpaka mwisho. Ni kwa namna gani utaweza kuwa Waziri? Ni kuepukana na machozi ya wananchi. Wizara ya Maliasili imekuwa ni sehemu ya kusababisha machozi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngorongoro tukiangalia eneo la Pori Tengefu la Loliondo baada ya kutengwa, Mheshimiwa Waziri baadhi ya maeneo, kwa mfano tukiangalia Kata ya Arash, Kata ya Piyaya, Kata ya Malambo na Kata

Ololosokwan na Kata ya Soit Sambu ni Kata ambazo zimeathirika sana. Tukitolea mfano, Kata ya Arash toka eneo limetengwa Mwezi June mwaka jana mpaka Februari mwaka huu, mifugo zaidi ya 6,770 imekamatwa kwa sababu wananchi hawana eneo lingine la kulisha. Kama wananchi wangekuwa na eneo lingine la kulisha mifugo yao wasingeweza kupeleka tena katika lile eneo, mifugo zaidi ya 6,700. Ukienda Kata ya Soit Sambu vivyo hivyo, ukienda Kata Ololosokwan ni hivyo hivyo Kata Oloipiri hata jana, Kata ya Malambo Kijiji cha Sanjan mifugo zaidi ya 87 imekamatwa na kutozwa shilingi milioni nane na laki saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Waziri, mimi nadhani tuna uhitaji uhifadhi sana, lakini uhifadhi huu ni kwa ajili ya nani? Ni kwa ajili ya Watanzania. Kwa hiyo, uhifadhi unaowaumiza wananchi tusiendekeze. Niombe Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Mchengerwa, kwa nia ya dhati kabisa nikuombe tuende Ngorongoro, nitatenga muda wangu nitatembea na wewe, tuangalie maeneo yote ambayo yameathirika tuweze kuwasaidia wananchi, tuwasaidie kwa sababu haiwezekani leo, hivi Mheshimiwa Mchengerwa leo Kata ya Arash wametaifishwa mifugo 276, kaya zaidi ya 280 hawana mifugo tena, watoto wao wameacha shule waliokuwa kwenye vyuo, waliokuwa sekondari, wameacha shule. Sasa naamini kwamba uhifadhi huu siyo kwa ajili ya kuwaumiza wananchi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuombe wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kwa ujumla ukienda Kata, nikuambie tu niliuliza swali Namba 343 alijibu Naibu Waziri hapa. Alisema Kijiji cha Ngaresero hakipo ndani ya eneo la Poloreti. Mheshimiwa Waziri nipo tayari tusindikizane nikupeleke pale kama Kijiji cha Ngaresero hakijaingia kwenye Pori la Poloreti mimi nitajiuzuru Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *beacon* Namba 31 mpaka beacon Na. 159 zipo kitongoji cha Leparagashi, Kijiji cha Ngaresero zaidi ya kilomita tisa. Kwa hiyo, niwaombe wakati pia wa kujibu maswali hapa *consult* Mbunge anayehusika akupe ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile wakati unajibu nilikuwa Ngorongoro tulikuwa na Makamu wa Rais, wananchi walikuwa

wanacheka! Kijiji hicho mifugo zaidi ya mia tano wamekamatwa, hata ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngaresero ng'ombe 400 wamekamatwa, wakatozwa shilingi milioni 40. Sasa leo tukikaa tusidanganyane, ni bora tutatue matatizo ya wananchi kiuhalisia, kwa sababu utalii tunaupenda, uhifadhi tunaupenda lakini leo isiwe ni sehemu ya kuwafanya wananchi wa Tanzania kuwa maskini, iwe ni sehemu ya kuwasaidia kutatua matatizo yao. Pale tatizo linapotokea ni muhimu kukaa na wananchi tuyamalize. Naomba upange ratiba yako na tutamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Rais akuwezeshe utatue migogoro ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye Kata ya Ololosokwan, Soit Sambu, Oloipiri wananchi hawana mahindi. Tembo wameingia kwenye mashamba wamemaliza. Kutoa fidia mnatoa elfu ishirini na tano kwa heka imsaidie nani. Ni wakati muafaka pia tufikirie mtu shamba lake tembo wakila shamba zima tunakadiria tunapata gunia ngapi kwenye shamba mtu asiibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunafikiria nimeona kwenye mipango yenu. Mnafikiria tena kupandisha hadhi Pori Tengefu la *Lake Natron*. *Lake Natron* imebeba Kata ya Ngaresero na Pinyinyi pamoja imeingia kwenye Kijiji cha Jema Kata ya Oldonyo Sambu. Ukija huku Tarafa ya Ngorongoro, kwa hiyo Wilaya nzima ya Ngorongoro itakuwa uhifadhi kwa asilimia 85. Hawa wananchi sijui watakuwawapi tena kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuende kwenye suala la uhamaji wa hiari. Suala hili tulianza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema wananchi washirikishwe kwa dhati. Kwa jinsi zoezi linavyokwenda, ushirikishwaji umekuwa hafifu. Kuna timu zimeundwa kwa ajili ya kuandikisha watu wanaoenda. Zoezi lenyewe siyo wazi, mwananchi unamfanyia tathmini halafu unakuja kuvunja nyumba yake, siku hiyo anaondoka ndiyo unaenda kumwonesha unachomlipa. Humuoneshi kabla, lakini baada ya kuvunja makazi yake yote ndiyo unaenda kumuonesha kwamba utalipwa hiki. Mwananchi hana namna lazima aende kwa sababu umeshamvunjia makazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pamoja na zoezi lote, wewe umeona kwamba sasa hivi waliondoka ni wananchi 3,010 tu, wananchi waliopo pale ni zaidi ya laki moja na kumi ambao wamebaki walioandikishwa ni watu 5,000 maana yake ukishaondoa hapo tutabaki na zaidi ya watu laki moja na elfu mbili. Halafu Mheshimiwa Mchengerwa choo ikijaa unawanyima hata, naomba kwa sababu wewe ndiyo umeingia tujaribu namna ya ku-*consult* jamii, tuzungumze kwa pamoja tuone namna ya kutatua matatizo, kwa sababu leo huwezi ukasema kwamba wanaondoka hao watu 7,000 halafu ndiyo zoezi limeisha. Pia, kinachotakiwa zoezi liwe wazi tusifichane. Wananchi wanahitaji kujua kwamba ni watu wangapi wanahitaji kuondoka? Leo hii tunasema kwa hiari uwazi uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora tuanzishe tena vikao tuzungumze kwa pamoja jamii ishirikishwe, wewe binafsi kama Waziri, mimi niko tayari kama Mbunge tushirikiane pamoja kufanya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri lakini naomba masula yote ya Ngorongoro pamoja na Pori Tengefu la Loliondo tushirikiane kwa pamoja ili wananchi waache kulia. Nashukuru sana niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Shangai. Nilimwita Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uhai kusimama tena ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa muda mchache alioingia anaonesha uongozi, kwamba uongozi ni pamoja na kusikiliza wenzio, lakini ameshindwa kuonesha hali nyingine ambayo kwamba na yeye ni Mbunge kama Wabunge wenzake, tunakupongeza sana. Pia nimpongeze

Naibu wako anafanya kazi nzuri sana. Mapungufu mengine ni ya kawaida kwenye ubinadamu lakini naamini kwenye michango hii kuna kitu amejifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwanza kwenye suala la kifuta machozi. Ili uweze kuwajibika vyema bila migogoro kwenye Wizara yako lazima uanze kufanya maboresho makubwa sana. Maboresho yenyewe ni pamoja na hizi Kanuni za Mwaka 2011. Tunaposema tunahifadhi hakuna Mtanzania asiyependa kuhifadhi ila wataona manufaa ya uhifadhi watakapoona matokeo ya moja kwa moja, na ili waone matokeo ni lazima kuwe na ushirikishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili eneo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambae amekuwa anatoa miongozo mbalimbali na maelekezo ya namna ya kutatua migogoro hii bila kuacha makovu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nataka nianze kwenye kifuta machozi. Kama leo tukiacha ikabaki sura hiyo ilivyo kwenye sheria ilivyo pamoja na Kanuni tunaonesha ni namna gani Serikali yetu inathamini wanyama kuliko binadamu, sura hii siyo nzuri. Sote tunajua kwamba tunapohifadhi tunategemea kupata faida, leo tunapozungumzia utalii lazima uwekeze, unaanza kuwekeza wapi unaanza kuwekeza kwenye kuhifadhi lakini tunapohifadhi lazima mwananchi mwenyewe anaeishi hilo eneo ajue kwamba yeye ni mhifadhi namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nizungumzie kwenye maeneo machache tu kwenye hilo eneo ambalo lazima Mheshimiwa Waziri ufanye maboresho makubwa kwenye hizi kanuni. Mtu akipata majeraha ambayo anaweza akatibiwa akapona anatakiwa alipwe laki mbili, lakini mtu akipata jeraha la kudumu kwa mfano ameondolewa mkono labda alikuwa analima atalipwa laki tano. Mkono haupo kabisa analipwa laki tano, ikitokea mtu huyo ameuawa analipwa milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunataka kufananisha thamani ya mwanadamu na shilingi milioni moja, wakati unazungumza hapa kwenye hotuba yako nilikufatilia vizuri, kwamba nchi

nyingine wameshaondoa kabisa suala la kifuta machozi ili uondoe kifuta machozi lazima uje na mikakati thabiti ya kuzuia wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kabla ya kufikiri kuondoa hicho kifuta machozi kwanza kiboreshwe wakati mnajipanga sasa kuzuia hao Wanyama. Leo Watanzania hawa wanapomuona tembo anakwenda kwenye shamba lake, anajua hata nikitoa taarifa kwa sababu yule hajapewa mafunzo na ninyi mmetuambia mmewapa watu mafunzo, yule hana mafunzo yoyote ya namna ya kukabiliana na tembo. Ni vizuri kama Taifa haya mambo inawezekana yalifaa kwa kipindi hicho, haya ni mambo ya kikoloni kabisa yamepitwa na wakati. Lazima tuanze kufikiri upya ili na huyu Mtanzania yawezekana tuliweka hizo kanuni kwa ajili ya kulinda Wanyama, lakini mimi nasema kwenye kauli mbiu yako ulisema tulirithishwa na sisi turithishe. Hatukurithishwa wanyama, tulirithishwa maeneo yenyewe ya hifadhi na wanyama ila tumerithishwa sisi binadamu siyo wanyama wamerithishwa binadamu. Kwa hiyo, binadamu alipewa nafasi ya kwanza kwa sababu tunahifadhi kwa ajili ya nani? Tunahifadhi kwa ajili ya sisi wenyewe, kwa hiyo lazima tutengeneze mazingira rafiki kwa ajili ya uhifadhi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ni mfano mdogo kwa binadamu, nataka nije kwenye mazao. Wanasema kuanzia mita mia tano kutoka eneo la hifadhi, nikiwa ndani mita mia tano halipwi kabisa kama ikitokea wanyama wameenda kula mazao yake, lakini kuanzia mita mia tano na moja mpaka kilomita moja atalipwa shilingi elfu ishirini na tano kwa hekari moja. Leo Mheshimiwa Waziri tuambie mfuko mmoja wa mbolea ni shilingi ngapi, elfu 25 anakwenda kununua nini hata mfuko wa mbegu tu hawawezi kununua hizo ni dharau na ni mambo ya kikoloni na hayana maana kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni kilomita moja kutoka eneo la hifadhi mpaka kilomita nne kwa hekari moja mazao yake yaliyoliwa, ambayo hesabu ya kawaida tu Mheshimiwa Mchengerwa, yaani hesabu ya kawaida heka moja ile kuanzia kuandaa mpaka kuvuna ni laki saba. Ninyi mnasema ikiwa ni kilomita moja kutoka eneo la hifadhi mtamlipa fidia shilingi elfu

hamsini. Kanuni za wapi ni za Watanzania kweli hizi zilitungwa na Watanzania, tulikuwa tunatunga kwa ajili ya kumsaidia nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni kilomita nne mpaka kilomita tano kutoka eneo la hifadhi, heka moja atalipwa shilingi elfu 75. Kanuni za wapi? Tulikuwa tunawatungia nchi gani? Lazima haya mambo yaboreshwe Mheshimiwa Mchengerwa hata ufanye nini kwa hali ya kawaida. Ikiwa zaidi ya kilomita tano heka moja atalipwa laki moja, tena anasema zisizidi heka tano, ukiziona tu hizo kanuni zimejikita kuwatia umaskini Watanzania. Kwa nini zisizidi heka tano? Tunataka wananchi wetu, yaani wao waanze kufikiri heka tano tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa hapa ndani tunasema lazima wafugaji waanze kufikiri kufuga kisasa, kwa nini tusifikiri kuhusu kuwekeza kisasa? Namna ya kuhifadhi hifadhi zetu? Tunapowambia Watanzania kwamba lazima waache suala la kuhama hama na mifugo yao waanze kufikiri kufuga kisasa, kwa nini sisi kama Serikali hifadhi zetu tusianze kufikiri kuhifadhi kisasa? Tutumie maeneo madogo lakini kwa uhifadhi ambao una manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye ushauri, najua Mheshimiwa Mchengerwa ndiyo ameingia kwenye hii Wizara lakini tumeona maajabu yake kwenye hizo Wizara hizi mbili alikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, lazima mambo yote mnayoyafanya yawe shirikishi. Lazima wafikiri kujenga fensi kwenye hifadhi zao. Tukibaki hivyo hivyo Watanzania wataanza kufikiri sasa kwamba ukikutana na tembo malizana nae. Kwa sababu heka yako moja imeondoka, umechukua mkopo benki halafu unaambiwa utalipwa 25,000 nani atakubali hiyo habari Mheshimiwa Waziri? Tuanze kufikiri namna ya kuwatunza hawa wanyama lakini kwa miundombinu ambayo ni rafiki na Watanzania wabaki kuendelea na shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ukija hapa utuambie ni lini utapitia hizo kanuni ambazo zimepitwa na wakati?

Kanuni hizi zinaleta sura mbaya kwa Taifa letu pamoja na yote yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine, lazima muanze kufikiri inapotokea nyumba ya kwanza imeanza kujengwa kwenye hifadhi, ya pili mpaka ikawa Kijiji na uchaguzi ukafanyika akapatikana mwenyekiti wa Serikali, halafu mnakuja baadae mnasema watu hawa wapo kwenye hifadhi! Kwani Serikali ilikuwa likizo toka nyumba ya kwanza inajengwa mpaka ikawa Kijiji mpaka Mwenyekiti? Kwa bahati mbaya Serikali hiyo hiyo inatenga fedha kwa ajili ya uchaguzi hawajui kwamba Kijiji kile kipo kwenye hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapo shule inaanza kujengwa, *TANESCO* wanapeleka umeme, watu wa maji wanapeleka, Serikali ni moja. Kwa hiyo, ni lazima hivi vitu muanze kutengeneza mambo ambayo yatakwenda kama *uniform*. TAMISEMI, Wizara ya Ardhi pamoja na ninyi lazima mkae pamoja. Pia, kuna migogoro mingine Mheshimiwa Waziri unaibeba wewe kwa sababu unaenda kwa ajili ya wanyama kumbe ni watu wengine, ni Wizara nyingine ndiyo imetengeneza imeshindwa kuwajibika, lakini kwa kuwa Serikali ni moja lazima mkae muone namna ya kumaliza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba tuongeze vituo vya Askari. Mimi nawapongeza sana *TAWA* wilaya ya Nkasi wanajituma sana, wanajituma mno. Mheshimiwa Waziri, waongezee Askari, wapatie gari ili waweze kuwajibika. Kwa sababu wako kituo "A" wanaitwa kwamba tembo wamekuja mpaka watoke kule waende ni siku ya pili! inaonekana kama wao hawawathamini, kumbe ni kwa sababu mazingira yao siyo rafiki kwa ajili ya utendaji. Tunaomba tuwasidie *TAWA* waongezeeni bajeti lakini pia muongeze vituo. Wilaya ya Nkasi angalau tunaomba katika Jimbo langu muongeze vituo vinne kwa kuanzia ili tuweze kuondoa hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori lazima iangaliwe tena, tunatamani Sheria hizi tunazozitunga leo ziwe na faida kwa Watanzania zisiende kuwa kikwazo kama ilivyo sasa. Vilevile, Sheria ya Uhifadhi ya

Wanyamapori iangalie upya, kwa sababu ndiyo umeingia ili uweze kuboresha vizuri majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Mheshimiwa Waziri, suala la uvunaji wa tembo pamoja na wanyama wengine ikiwemo Mamba. Suala hilo limekuwa na kizungumkuti sana, ukiwauliza hawa wahifadhi wanasema kwanza hakuna sheria inayosema tuvune. Sasa kama hakuna sheria inayosema tuvune mnataka wananchi wawafundishe namna ya kuvuna? Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tukisema njooni muwaondoe mkiwaondoa leo kesho wanarudi, mmeshindwa namna ya kuwadhibiti, tofauti na hapo mtuambie kwamba mmekuwa na maeneo mengi ya hifadhi ambayo mmeshindwa kuyadhibiti. Kwa hiyo, mchague maeneo ambayo leo mnaweza kuyasimamia kikamilifu kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa kwa sababu ya muda nataka nizungumzie *TFS*. Hawa *TFS* ni watu ambao tunawahitaji sana, lakini leo huyu mwananchi wa kawaida ambaye amenunua mkaa debe moja akakamatwa barabarani, kuanzia huko alikotokea msituni anakuja kukamatwa nyumbani, hawa *TFS* kazi yao ni kuja kukamata au kusimamia kule ndani ili miti isivunjwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida tu hivi kweli hili eneo lina misitu na halina madawati na hao watu wanataifisha kila siku, hivi hizi mbao ambazo wanataifisha kwa nini zisiwasaidie wale watu ambao wako jirani kwenye hayo maeneo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani, nilimtaja Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya kazi kubwa ya *Royal Tour* na kwa Jimbo langu imeleta mafanikio makubwa sana. Mheshimiwa

Waziri ni shahidi mwezi uliopita alikuwepo katika Jimbo langu akiwa na Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Karatu limezungukwa na hifadhi mbili, Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na *Lake* Manyara *National Park,* pia Jimbo langu lina Kata 14, Kata Tisa zimezungukwa na hifadhi lakini vilevile vijiji 29 vimezungukwa na hifadhi katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wameongea changamoto kubwa ya tembo lakini niseme kwamba siku ya Ijumaa tulipoteza mwananchi mmoja katika Kata ya Oldean na leo hii siku ya Jumatatu wanampumzisha. Niseme ni kilio kikubwa kwa Jimbo langu la Karatu pia najiuliza watu hawa wa hifadhi ng'ombe wakiingia kwenye hifadhi wanakuwa makini kweli na sasa hivi ng'ombe mmoja anapigwa faini ya shilingi 100,000 lakini sasa hivi suala la faini ya 100,000 wameacha sasa hivi wamekwenda mbele zaidi wanataifisha mali za wafugaji wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wakiingia kwenye shamba la mkulima hana bei. Ndiyo Mheshimiwa mchangiaji aliyetangulia amesema kwamba kwa hekari moja unafidiwa kwa shilingi 25,000 wakati huo mita 500 hawawezi kuchangia chochote. Mimi pia najiuliza Mamlaka ya Hifadhi za Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 wakati huo wananchi walikuwepo na ikaweka *fire-line* katika eneo hilo, ikawekwa mpaka wa Hifadhi ya Ngorongoro na ikawekwa *fireline* kwenye mpaka upande wa wananchi. Leo wameweka kwenye kanuni zao mita 500 hamna kumchangia hata hiyo 25,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa kama ilivyoelezwa mita 500 mpaka 1000 kama ilivyoelezwa lakini kuanzia kilometa Nne mpaka tano shilingi 75,000. Lakini kilometa Nne mpaka Tano ni shilingi 100,000. Pia, ukiwa na zaidi ya hekari tano hawakupi fidia hata zikiharibiwa hekari 50, wao wanachojua ni hekari tano tu. Huu ni uonevu kwa wananchi wetu na wametuonea kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia najiuliza hao waliopitisha shilingi 25,000 kwa heka Wizarani au *TAWA* hivi kweli wameangalia na hao ni wakulima kweli? Hivi mwananchi unamsaidia kwa 25,000 kwa hekari? Hata kwa kilimo tu cha trekta haitoshi wakati huo mwananchi amegharamika mpaka anakaribia kuvuna tembo nakwenda kuharibu. Kwa nini tusitunge sheria tembo hawa ni mali ya Serikali na kuna watu wameajiriwa kwa ajili ya kuchunga. Kama tembo hawa wanatoka misituni wanaingia kwenye mali za wananchi siyo kwamba wale wanaowachunga msituni wamezembea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo mpaka wanafika kwenye mali za wananchi kama ng'ombe wetu wanaingia misituni wanakuwa makini kutu–*charge* shilingi laki moja kila ng'ombe, hao ng'ombe wao wanaotoka misituni wanakuja kwenye mali yetu sisi wananchi halafu wanatupangia na fidia wanatoa wanavyotaka na wanayoona wao inafaa. Pia, inaweza kuchukua hata miaka mitatu mwananchi anaendelea kudai hata hiyo 25,000 anaweza kudai miaka mitatu. Hii siyo sawa. Tukuombe Mheshimiwa Waziri, uangalie kwa upya, kwa sisi tuliozunguka na hizi mbunga tumeumia kweli kwa muda mrefu na wananchi wetu wanaendelea kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika Jimbo langu kuna changamoto kubwa hasa katika kata tatu; Kata ya Oldean, Kata ya Daa na Kata ya Ganako. Wananchi wale wamekuwa maskini kabisa katika muda mrefu kabisa kwa miaka yote ambao wanapakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorogoro. Mimi sisemi kwanini tumezungukwa na hizi hifadhi, lakini tunachoomba kwa Wizara waweze kuona ni namna ipi ili waweze kuwadhibiti wanyama hawa ambao wanaumiza wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa mfano Wilaya kama hii ambayo ina vijiji 29, ina kata tisa imezungukwa na hifadhi, hamna hata gari moja la kufanya doria, Wilaya nzima hamna hata gari moja la kufanya doria. Wale watumishi wamekaa pale hawana hata kazi yoyote, kwa sababu kazi yao kubwa ilikuwa wawasaidie wananchi wetu kuzunguka lakini hawana gari, wamekaa tu ofisini wanapiga mshahara wa bure

kabisa hamna kazi na wanaendelea kuwepo katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, katika Jimbo langu nina changamoto na nilikueleza siku ile ulikuwepo na Makamu wa Rais. Katika eneo la Kata ya Buger kulikuwa na changamoto kubwa na bahati nzuri nilipata bahati ya kwenda na Naibu Waziri, wanachobishainia pale wananchi na watu wa uhifadhi ikizidi sana kwa upana ni hatua 30 na maeneo mengine ni hatua 10. Hata hivyo, imekuwa ni mgogoro wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 *TANAPA* waliweka alama, 2014 wakaboresha, mwaka 2018 wakaingia kwa wananchi zaidi kama ninavyoeleza hatua 30 maeneo mengine hatua 14 lakini ikizidi sana upana huo ni hatua 30. Nilienda na Mheshimiwa Naibu Waziri lilipopata bahati ya kutembelewa, badala ya kupungua kwa ule mgogoro alichokifanya Naibu Waziri, ni kwenda kuongeza ule mgogoro na aliendelea kutoa matamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa Viongozi au Mawaziri tusiwe Mawaziri wa matamko, tujaribu kusikiliza wananchi wetu. Shida yetu kubwa ni kwamba tunawasikiliza viongozi wale ambao tunawakuta kwenye eneo lile na ambao wako upande wa Serikali. Tunashindwa kutoa fursa kama Kiongozi kuwasikiliza wananchi. Sasa kama Kiongozi wa Serikali upime sasa lile unaloambiwa na mwenzako kule chini linaendana na hali ya wananchi wa eneo husika? Mimi sioni sababu ya wananchi kuendelea kugombana na Serikali yao kwa hatua 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru uliahidi kwamba mwezi huu wa Saba unaweza kwenda kutembelea eneo lile la Buger na mimi nikukaribishe. Sioni sababu ukagawanya Kata, kaya baadhi za wananchi lakini inakata mashamba ya watu na Mheshimiwa Naibu Waziri alisema tutatoa fidia. Wananchi wale wamenituma sisi hatuna shida na fedha bali sisi tuna shida na ardhi yetu ambayo tumekaa nayo toka enzi za mababu. Hatuko tayari kuchukua fidia, kama ni mali yenu kwa nini mnatufidia sisi? Huwezi kutufidia, kama ni mali yako chukua, kama ni mali yetu usitufidie! Sisi hatuhitaji na wananchi wale wamenituma kwamba

sisi fidia hatuhitaji, tunachohitaji ni ardhi yetu na siyo eneo kubwa ni eneo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Serikali mwaka 2011 wanakuja kuweka *beacon*, wametumia fedha za umma, wanakuja kuweka 2014, wanakuja kuweka 2018 watu hao hao! Unajiuliza, wale waliofanya 2011 ni Serikali kutoka wapi, na hawa 2018 ni kutoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba pia ninakukaribisha katika Jimbo la Karatu, tutakwenda kwenye ile Kata, wananchi wale hawana shida, sisi tunaelewa kwa sababu tumekaa na hawa wanyama muda mrefu, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imeanzishwa mwaka 1959 sisi tunakaa nao? Pia, wananchi wale hawana shida na uhifadhi ni katika eneo lile linaloonekana wananchi wetu wananyang'anywa mali yao kwa nguvu kabisa. Kwa sababu 2011 waliweka *beacon,* 2014 waliweka *beacon* na 2018 wakasogeza wakaingia kwa wananchi. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, niko hapa Salome.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mheshimiwa Mbunge, muda wake ulikuwa umekwisha alikuwa anamalizia sentensi yake.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa nafasi lakini ninamuomba Mheshimiwa Waziri mwezi wa Saba karibu kwenye Jimbo langu tuweze kushusha ile *pressure*. Siku ile ulipotoa kauli katika eneo la Karatu wale *pressure* ilishuka. Nami ninaamini kwa jinsi ulivyofanya kule Tarime naamini kwamba kwa Karatu utaweza kuja kufanya vizuri, ninakushukuru na ninakukaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Tlemai, huyu ni mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu, ninaomba nitaje majina ambayo yataanza jioni. Kwanza ni Mheshimiwa Kwagilwa

Nhamanilo, Pili ni Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Felix Kavejuru Eliadory.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge kuna matangazo mawili kutoka kwa Katibu wa Bunge.

Tangazo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Bodi ya Filamu Tanzania chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia programu yake ya kurudisha utamaduni wa kuangalia filamu za Kitanzania kwenye kumbi za kisasa za sinema inawakaribisha Waheshimwa Wabunge wote leo Tarehe 05 Juni, 2023 kwenye onesho la filamu ya *The Green Tanzanite* iliyoandaliwa kwa kiwango cha hali ya juu kwa kushirikisha wacheza filamu kutoka Tanzania, India, China na Jamhuri ya Cech. Filamu hii itaoneshwa kwenye ukumbi wa sinema wa *Mysterious Cinematics* uliopo Kambarage *Tower* ghorofa ya pili kuanzia saa 2.30 Jioni na kiingilio ni shilingi 30,000. Mgeni Rasmi katika onesho hilo ni Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuunga mkono tasnia ya filamu nchini. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea na maonesho ya utalii katika Viwanja vya Bunge, hivyo, mnaombwa Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea maonesho hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nawatakia mchana mwema nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja Jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii adhimu ili na mimi nipate kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Handeni Mjini kwenye Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Uchaguzi ukurasa wa 11, ukisoma kile kipengere cha 67(a), sitakinukuu lakini nitataja kilichoelekezwa kwa sababu ya muda. Ilani inatuelekeza ifikapo 2025 tunatakiwa tuweze kuingiza fedha zinazotokana na Utalii dola za Kimarekani bilioni sita au fedha za Kitanzania karibia trilioni 14 ndani ya miaka mitano ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile Ilani inatuelekeza ifikapo mwaka huu wa 2025 nchi yetu iwe imepokea au imepata Watalii milioni tano. Hali ikoje kwa sasa? Hali ilivyo kwa sasa mpaka Aprili 14 taarifa ya Serikali inaonesha kwamba tulikuwa na watalii 1,412,719 pungufu ya lengo kwa 3,500,000. Wakati huohuo inaonyesha tulikuwa tumeoingiza fedha bilioni za Kitanzania 288 ambayo hiyo ni asilimia kidogo sana ukilinganisha na lengo la bilioni sita kwa maana ya trilioni 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zetu hizi wenzetu wa Maliasili hizi za kusema wanazo 1, 412,719 wanazipataje? Watalii wa Ndani kwenye hiyo 1,400,000 wako 718,299, watalii wa nje na hapa

nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake binafsi naomba mninukuu hilo vizuri kwa juhudi zake binafsi za kufanya tukio kubwa lile la *Royal Tour* na kuwavuta watalii kuja hapa Tanzania, watalii 694,420. Kwa hiyo, watalii 694,420 wameletwa na Mheshimiwa Rais kwa sababu ya *Royal Tour* hawa wa ndani 718,000 ndio nataka nizungumzia takwimu wanaziptaje hizi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana, eti hata mtu akipanda basi anatoka Arusha kupitia Momera kwenda vijijini anahesabiwa ni mtalii, akipanda basi kutoka Bagamoyo au gari binafsi kupitia Saadani, Pangani yaani mimi Kwagilwa naenda Handeni nataka nipite Tanga Mjini niende msibani nahesabiwa ni mtalii.

Mheshimiwa Spika, mtu akipanda basi kutoka Arusha akapita Serengeti Ngorongoro anaenda zake Musoma anaenda kuoa huko, anaenda zake Musoma anaenda kutibiwa, anaenda zake Tarime mahindi yake yameliwa na ng'ombe anawahi, anaenda zake Mwanza anahesabiwa ni mtalii, halafu tunakuja hapa tunasema tuna watalii 1,412,000! Nimesema nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwaleta hawa 694,420, ninyi mnafanya kazi gani watalii wa kwenu wako wapi? maana hao miongoni mwao ni wasafiri, ni watu wanatoka Dar es salaam wamepanda treni ya *TAZARA* wanapita Morogoro wanaenda zao Mbeya mnahesabu watalii.

Mheshimiwa Spika, mtalifikiaje lengo la watalii milioni tano, mtalifikiaje lengo! Mtalifikiaje lengo hilo? Sikilizeni niwaambie ni lazima mtekeleze wajibu wenu wa kumsaidia Mheshimiwa Rais, kwenye hii habari ya utalii lazima tufanye mambo yafuatayo badala ya kuwa mnakuja hapa na kutupa takwimu kwamba kuna watalii wa ndani laki saba kumbe mmehesabu na wafugaji ambao wanahamishwa kutoka Ngorongoro wanaenda Handeni wakipita getini mnawahesabu!

Jambo la kwanza la kufanya, ondoeni *VAT* kwenye *Airline Industry.* Sikilizeni niwaambie utalii ni *export,* tunafanya *export of service* ndiyo maana tunapata Dola katika kipindi ambacho dunia yote ina msukosuko kuhusu *forex* hatuna fedha za kigeni za

kutosha, utalii sisi ndiyo ulitakiwa utulinde tupate fedha za kigeni, acha kuhesabu mtu anakwenda mnadani kuuza kondoo amepita getini unamhesabu.

Mheshimiwa Spika, fanyeni jitihada sekta hii ituokoe, ondoeni *VAT* kwenye *Airline* maeneo yafuatayo:-

Kwanza; kwenye Ndege. Kwenye Injini za Ndege, hizi injini zinauzwa gharama kubwa sana ukitoza *VAT* unafanya hilo jambo linakuwa la anasa, Kwa hiyo matokeo yake *Airline Industry* ya kwetu iliyo ndani haiwezi ku-*compete regionally,* ondoeni *VAT* kwenye *spare parts* za ndege, ondoeni *VAT* kwenye *aircraft maintenance*.

Mheshimiwa Spika, hizi ndege zinasaidia wawindaji kupekewa watalii wao kwenye vituo vya kuwindia, zinasaidia watalii kutoka eneo moja kwenda jingine, sasa leo mtu amekubebea watu anakuletea unamgonga *VAT!* tutapata wapi mapato? Mtafikaje bilioni sita kwa mwaka? Mtafikaje watalii milioni tano?

Pili; ondoeni *VAT* kwenye ada za vitalu. Mtu anapokuwa amelipia kitalu kwa mwaka, amelipa ile ada ya kwanza anakuwa amekilipia kwa miaka kumi ninyi hata ile fedha ambayo anawalipa kwa miaka inayofuata mnaipiga *VAT 100 percent, that's wrong*! Ilani yetu ya Uchaguzi inasema nini? Tatizo hamsomi hiki kitabu kizuri. Ilani inasema fanyeni mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo (c) ukurasa wa 112, Sheria ya *VAT* siyo msahafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *Finance Bill,* nataka tu nitoe taarifa kwamba nitashika shilingi leo kama Serikali haitaweka *commitment* kwenye *Finance Bill* inayokuja hii ili kuondoa *VAT* kwenye haya mambo ninayoyazungumza hapa. Tunataka fedha za kigeni, hatuwezi tukafika mahala, tutafika mahala tutashindwa hata kuagiza mafuta kwa sababu hatuna Dola, tutafika mahala viwanda vyetu vitashindwa kununua *raw materials* kwa sababu hatuna Dola lakini tuna nchi ambayo imejaliwa tuna kazi ya kuhesabiana tu mtu kapita anaenda Ngorongoro, mtu kapita

anaenda msibani mnasema ni mtalii ameingiza nini cha *forex*. *(Makofi)*

Mwisho, watu wa mahoteli, watu wanaosafirisha kwenye *tourism industry* wanatozwa *VAT* mahala ambapo siyo sahihi kwa sababu tu ya ubovu wa sheria, ninyi watu wa maliasili na utalii hawa wanaondesha sekta ya utalii, *private sector* ni watu wenu, simameni muwatetee na ninyi msiwe sehemu ya kuungana kuwakandamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ondoeni *VAT* kwenye *deposit*. Sheria iliyopo ya *VAT* inasema hivi: *The Value Added Tax imposed on taxable supply shall become payable at the earlier of (A) the time when an invoice of supply is issued;* yaani mtu tu akipata mtalii kule nje akimwandikia tu *invoice* mnakuja mnataka *VAT* anaitoa wapi? Akakope? Halafu unasoma inasema: *the time when consideration of supply is made* yaani hata akilipa *advance* tu ambayo mtalii anakuja miezi sita baadae leo analipa kuwahi chumba analipa kuwahi ndege analipa, ninyi mnataka kodi *we cannot work like that!* Halafu *we are very comfortable* eti sheria iko hivyo! Sheria ni kitu gani kwani? Sheria inatungwa hapa! Kwa hiyo, tuondoeni hivi vitu. *(Makofi)*

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Asya.

**TAARIFA**

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kuhusiana na wadau wa utalii hasa hawa wawekezaji wa *tour industry*.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la hawa wadau kutozwa *VAT* kwa sababu wageni wanapokuwa nje ya nchi ni lazima wafanye *advance booking* kwenye mahoteli, hoteli Sheria ukiisoma ya Utalii, hawa watu wanalipa kodi (*VAT)* ni mwisho wa

mwaka siyo kipindi kile ambacho mgeni ana-*book,* kwa hiyo asipotoshe.

**SPIKA:** Mheshimiwa umepokea taarifa hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, anasema napotosha siipokei taarifa, nataka nimwambie nimesimama hapa nimesema nasimama kuongea kwa wananchi wa Handeni Mjini watu werevu kabisa wanaelewa ninachofanya hapa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufanye mapinduzi kwenye hii sekta ili tumuunge mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya jitihada kubwa sana *why are we lagging behind*?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu muda wake umeshaisha nilikuwa nasubiri amalize sentensi yake, ahsante sana. Mheshimiwa Kwagilwa muda wako umekwisha kengele ya pili ilishagonga, ahsante sana.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahasante sana. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa, Margaret Simwanza Sitta, ajiandae.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uzima. Nami nielekeze mchango wangu moja kwa moja bila kupoteza muda kwenye Wizara yetu hii ambayo ni muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na mimi kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa *Royal Tour* ambayo imefanya vizuri na imeongeza watalii wengi sana katika nchi yetu. Pia nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako

kwa kazi kubwa na nzuri ambazo mnazifanya katika nchi hii, katika kipindi kifupi nafikiri miezi mitatu na siku kadhaa tumeona mabadiliko makubwa na sisi tunaimani sana na wewe. Nikuambie Mheshimiwa Waziri nilipanga kushika shilingi leo lakini kwa namna ambavyo nakuamini nina imani yote ambayo umetuambia yatakwenda kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nataka kuboresha tu kwenye hotuba yako ili uweze kuona namna nzuri ya kutusaidia watu wa Mvomero. kwanza ni suala la Tembo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 nilichangia kwenye Wizara hii ya Maliasili kwenye upande wa tembo, mwaka 2022 nilichangia na leo 2023 hakukuwa na utekelezaji wa aina yoyote lakini nina imani kama nilivyosema sasa unakwenda kutusaidia na kutatua changamoto tulizo nazo katika Wilaya yetu ya Mvomero.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri sasa hivi tembo katika nchi hii wana thamani kuliko binadamu, wenzangu wengi waliochangia hapa wameeleza kwenye maeneo yao namna ambavyo tembo wanawasumbua wananchi. Mvomero tumepakana na Hifadhi ya Mikumi, mpaka nazungumza hapa Mheshimiwa Waziri, tembo wameshaua wananchi 37. Wananchi wameshapoteza Maisha 37 kwa kipindi kifupi tu, wiki mbili zilizopita tumetoka kumzika ndugu yetu pale Mkata ameuawa na tembo.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi ambao mashamba yao yameharibiwa na hawa wanyama ni zaidi ya 2,500, hakuna chochote walicholipwa. Tunajua hakuna fidia kuna kifuta machozi na kuna kifuta jasho ambacho kwanza ni kidogo sana, leo mwananchi shamba lake likiharibiwa na tembo anatakiwa ekari moja alipwe laki moja, tunafahamu gharama za kutayarisha shamba, gharama za kupanda, kulima, mpaka kuvuna, leo shamba likiharibiwa na tembo anatakiwa kulipwa kiasi kisichozidi laki moja.

Mheshimiwa Spika, pia mwananchi ambaye ameuawa na tembo familia yake inatakiwa kulipwa kifuta machozi kisichozidi milioni moja. Hizi ni kanuni zilizopitwa na wakati Mheshimiwa Waziri, tunawaumiza wananchi na hawa wananchi siyo kwamba

wanataka hizi fidia, siyo kwamba wanataka hiki kifuta machozi na kifuta jasho, wanataka kuishi kwa amani hawataki kuishi na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa naomba leo nizungumze kwa kawaida tu, hivi Serikali imeshindwa kweli kuwarudisha tembo na kuwapeleka kule kwenye hifadhi? Ina maana kwamba hawa watalii ambao wanakuja kwenye hizi hifadhi zetu hawariziki na wale tembo ambao wako mle kwenye zile hifadhi? Sasa hawa tembo ambao wako nje ya hifadhi wanafanya nini Mheshimiwa Waziri? Watu wanaisha, watu wanapotea na hawo ni Watanzania wenzetu! Kifuta machozi chenyewe na kifuta jasho ni kidogo na hawalipwi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mvomero toka mwaka 2019 mpaka leo hakuna mtu aliyelipwa, lakini inaonesha Serikali inathamini sana tembo kuliko binadamu. Niliona kwenye hotuba yako kwamba utakuja sasa na sheria mpya ambayo itaweza kuwasaidia wale wananchi ambao wanakutana na hii adha ya tembo na tuondokane sasa na haya mambo ya kikoloni, haya mambo ya kulipana laki moja na milioni moja yalishapitwa na wakati. Tembo akienda kufanya uhalibifu kwenye maeneo ya wananchi kuwe na sheria ya kumlipa mwananchi fidia siyo kifuta machozi na kifuta jasho kama vile hisani, kuwe na fidia ambayo atakwenda kulipwa huyo mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri, mimi nina ushauri na sidhani kama Serikali mnashindwa, hivi ile Hifadhi ya Mikumi, sisi tuna Kata Saba ambazo zimepakana na Hifadhi, wale tembo waliopo kwenye hizi Kata Saba kwenye hii Tarafa ya Mlali, hivi mkiwarudisha kule halafu mkaweka fensi kwenye ile hifadhi hata zile fensi za umeme ambazo mnazipa umeme baadae mnyama akitaka kwenda kugusa fensi anapigwa *shot* anarudi, hivi Serikali na yenyewe inashindwa kuweka hizi fensi?

Mheshimiwa Spika, mbona wananchi wa kawaida katika maeneo mengine wanaweka hizi fensi? Ama kuchimba mtaro mkubwa ili wanyama wasiweze kuvuka na lenyewe linashindikana hili? Wako wakulima wetu katika Tarafa hii ya Mlali wana mashamba lakini wamezungusha fensi wamechimba mifereji

hakuna mnyama anayeingia katika mashamba, sasa nashindwa kuelewa Serikali inashindwaje kuweka fensi hata ya waya wa umeme wa kuzuia wanyama hawa wasiende kwenye maeneo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tembo ni wengi sana, wananchi sasa hivi hawalimi Kata ya Doma pale Kijiji cha Doma kule Mahalaka hali mbaya, hakuna mwananchi anayelima na kule tunajua wananchi wetu wanajishughulisha na shughuli za kilimo, kuna kilimo cha biashara wanalima nyanya na kuna kilimo cha chakula, pale Msongozi, Mkata, Mangaye Kata nzima ile hakuna mwananchi analima, Merela hakuna mwananchi yeyote analima, Rubungo na Mlali yote kwa ujumla hakuna mwananchi anayelima. Sasa Mheshimiwa Waziri ninakuomba na kwa sababu ninakuamini na hata ulivyoteuliwa kwenye Wizara hii mimi nilinyoosha mikono juu na kumshukuru Mungu kwamba matatizo haya sasa yanakwenda kuisha. Nimeona kwenye hotuba yako umesema Tanzania kwa Afrika tumekuwa watu wa tatu kama sikosei kwa kuwa na tembo wengi, Kimataifa huko tuna sifa kubwa ya kuhifadhi tembo lakini hawa tembo ambao huko nje tuna sifa huku ndani wanaua wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, naomba shughulikia masuala haya ya tembo. Pia nikupongeze nilikuomba siku moja unisadie tuweze kukutana na watu wa *TAWA* na ukatoa maelekezo tukakutana na watu wa *TAWA* tukafanya kikao kama wiki tatu zilizopita. Kikao kile nina imani kama yale tuliokubaliana yatatekelezeka hii changamoto kama siyo kuisha inakwenda kupungua kwa kiasi kikubwa, ninakupongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri sisi Mvomero tuna hifadhi ya Wami Mbiki na kuna Hifadhi ya Msitu. Hifadhi hii ya Wami Mbiki ni hifadhi ambayo ina migogoro na wananchi wanaopakana na hii hifadhi kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema toka nimekuwa Mbunge na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais ile timu ya Mawaziri Nane, pamoja ya kwamba hii timu imekwenda kukagua yale maeneo na kuanza kupima. Mimi kama Mbunge sijui na wananchi hawajashirikishwa lakini tuna imani itakwenda kututendea haki,

nimeona kwenye hotuba yako ulisema utawaagiza Wakuu wa Mikoa haraka iwezekanavyo waende wakamalize haya matatizo ya mipaka katika hizi hifadhi. Mimi nina imani pale katika Hifadhi yetu ya Wami Mbiki tunakwenda sasa kumaliza yale matatizo ili wananchi wetu sasa waweze kulima kwa uhuru. Wamekuwa wakinyanyasika miaka yote, wamekuwa wakinyanyasika kila siku wanashindwa kujua hatma yao lakini kwa maelekezo yako nina imani mambo yanakwenda kukaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuna Hifadhi ya Msitu wa Magote, hii hifadhi ilianzishwa mwaka 1940. Wananchi wameishi ndani ya hii hifadhi katika kipindi chote, kuanzia mwaka 1940 mpaka leo wananchi wapo kwenye ile hifadhi na watu wamezikana mababu na mababu katika ile hifadhi. Leo Serikali inataka kuwaondoa hawa wananchi ili hifadhi hii sasa waanze kupanda miti watu wa *TFS,* wakati hifadhi hii eneo lote la hifadhi kuna shughuli za kijamii na watu wamejenga, watu wamezikana, hakuna eneo lililobakia. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri hifadhi hii ni hifadhi ndogo sana, ipo pale Jongoya. Ninaomba busara zako utusaidie hifadhi hii wapewe wananchi ili tuweze kuondokana na adha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia…

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge majina hapa yako mengi kuliko muda wa kuchangia uliopo, kwa hivyo ili tuweze kwenda vizuri Wabunge waliochangia mara chache ndiyo watakaopata nafasi. Wabunge waliochangia mara nyingi zaidi wataikosa hiyo nafasi. Kwa hiyo, Wabunge waliochangia mara moja mara mbili wakiisha hao kama muda wetu bado upo tutawafikia waliochangia mara tatu halafu wale wa mara nne tutamalizia akama muda utatosha. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Felix Kavejuru Eliadory ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini la pili nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mtalii na muongoza watalii namba moja. Vilevile, naomba nikupongeze wewe mwenyewe na kukushukuru sana, pia nakushangaa una nguvu za ajabu, unakaa Bungeni na sisi kama haupo kwenye kiti unamaliza majukumu yako yote mezani, mambo yetu yote yanaenda vizuri, hakika hutashindwa pia kuongoza hilo Bunge la Dunia. Hutashindwa kwa sababu uwezo wako ni mkubwa sana, tunakuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Ndugu yetu Mchengerwa pamoja na Naibu wake Ndugu yetu Mary Masanja, wakati huo huo nawapongeza Katibu Mkuu pamoja na timu yao yote siyo rahisi kumtaja kila mmoja sasa hivi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii. Kwa namna hiyo pia ninavipongeza vyombo vya habari bila vyombo vya habari mambo ya utalii kwa vyovyote vile yatadorora. Kwa hiyo, nawapongeza *Safari Channel* wa *TBC*, wanapongeza *Channel Ten,* nawapongeza *ITV* na vyombo vyote kwa kweli, *Azam Tv* na vyombo vyote ambavyo vinajihusisha katika kuhakikisha kwamba wanahamasisha utalii na hasa katika maeneo yale ambayo bado yapo nyuma ki utalii ikiwemo Wilaya yangu ya Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuungana na ndugu zangu kule Mwanza kufuatia kifo cha Mwanahabari Magreth Tengule ambaye alikuwa ni mpenzi sana wa uandishi katika nakala za afya na utalii, Mwenyezi Mungu amrehemu. Mheshimiwa Naibu Waziri kuna wakati alikua amekuja kwenye Wilaya yangu ya Nyasa na kule kulikuwa na mgogoro mkubwa sana kwenye Pori la Liparamba na jirani zao ambao ni vijiji vinavyozunguka lakini alivyoondoka alituahidi atalifanyia kazi na kwa kutumia kikundi kazi kilichoundwa cha Mawaziri leo mgogoro ule umeisha, mipaka imeshawekwa, imebakia sehemu moja tu kutokea Ndondo mpaka Liparamba ambayo ninaomba pia wakamalizie, naamini chini ya uongozi madhubuti ya Mheshimiwa Kaka yetu

Mchengerwa Mjukuu wa Bibi Titi, Mama yetu jambo hilo pia litaisha salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo pia nitoe taarifa ambayo siyo nzuri, mamba wetu wa maajabu ambaye tulikuwa tunampenda sana alikuwa mpole akiitwa anakuja, kwa bahati mbaya alinaswa kwenye nyavu na wale ndugu zangu wakamuona ni kitoweo basi hatuna naye tena. Kwa kweli tunashukuru tu kwamba alikuwa ameshakuwa na watoto basi ndiyo habari hiyo kwa sababu alikuwa anajulikana Dunia nzima ni maajabu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia kuhusu umuhimu wa kupanga maeneo ya ardhi yetu hasa katika Wilaya ya Nyasa. Sasa hivi Wilaya ya Nyasa inakua vizuri kiutalii, tumehamasisha kwa muda mrefu wadau wamekuwa hawajitokezi sana. Sasa hivi wametokea *TAWA* ambao wamechukua Mlima wa Mbamba *Bay*, Tumbi na Kile Kisiwa cha Lundo. Tunashukuru wameanza kazi nzuri na hivi juzi nimeambiwa tayari boti limeshaenda kwa ajili ya kuwapeleka watalii kule Kisiwa cha Lundo. Niwaombe sana Wizara kupita *TAWA* muendelee kuiangalia Wilaya ya Nyasa kwa sababu vivutio vyake ni vingi sana, vinahitaji uwekezaji. Sisi tunapata wivu sana tunaposikia Ngorongoro kuna jambo hili, Serengeti kuna jambo hili, sijui fukwe za wapi jambo hili na kule sisi kunabaki kumekaa kama vile hakuna wa kutumia hizo fukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jitihada zilizoanza tunaomba muendelee nazo na ninazidi kuwasihi wale wote ambao wanatabia ya kuvamia maeneo kwenda kuleta vurugu kusema kwamba mlima huu wanasema na wenyewe ni wa kwao lazima tufuate taratibu na sheria za nchi. Kwa hiyo, ninawaomba sana mtu yeyote anayetaka kuwekeza kwenye milima hiyo basi hii milima yote ambayo tayari imeshakabidhiwa kwa *TAWA* wahakikishe wanawasiliana nao ili taratibu zifuatwe na uwekezaji ufanyike bila migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka nilizungumzie ni kuhusu asali. Nimeona hapa katika taarifa zetu ukiangalia toka mwaka 2005 asali tulikuwa tunavuna kiasi cha tani 465 ambayo

thamani yake ilikuwa tu kama milioni 550. Sasa hivi asili katika miaka kuanzia 2017 mpaka 2022 imeendelea kuongezeka na hata pale ilipokuwa inapungua imekuwa bado thamani yake ni kubwa. Kwa hiyo, niwaombe Wizara kuendelea kulisaidia zao hili la asali pamoja na nta, kwa sababu zao hili linamgusa mwananchi mmoja mmoja ukiacha hayo mambo mengine ambayo fedha yake inaenda moja kwa moja kwenye mifuko mikubwa ya Kitaifa, lakini kwenye asali na nta inaenda moja kwa moja kwa wale wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, niwaombe sana kulitilia mkazo zao hili lakini pia linatusaidia sisi katika kuapata afya.

Mheshimiwa Spika, wakati ule ilikuwa ukienda sokoni unataka asali unapewa asali iko kwenye chupa ya konyagi tena hiyo chupa sijui imeokotwa vipi shida tupu na hupati wakati mwingine, lakini sasa hivi asali ni zao ambalo unalipata kiurahisi kila mahali na kwa kweli kwa namna ya kipekee kabisa inaandikwa kwenye historia Mheshimiwa Mzee Pinda, Waziri wetu Mkuu Awamu ya Nne anastahili pongezi katika mdudu huyu anayeitwa nyuki pamoja na asali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nazidi kuomba kwamba tuwe na utamaduni wa kuandika historia za watu. Kama ambavyo leo tunamuona Mama, Mheshimiwa Rais alivyohangaika na *Royal Tour* aandikwe historia yake vizuri kwa sababu anayetenda jema apongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nikiendelea katika hili suala la makumbusho, makumbusho ukiangalia ni kama vile eneo la utalii ambalo halipendezi pendezi hivi, lakini sisi wenyewe tunashuhudia kila wakati wanapokuja viongozi wa Kitaifa kutoka nchi mbalimbali sehemu wanayokimbilia kwenda ni kwenye makumbusho. Ina maana wanataka kujua historia yetu wanataka kujifunza mambo mbalimbali lakini pia kupitia historia kama hizo zinatoa kipimo namna gani watu wamepiga hatua za kimaendeleo kutokea wakati huo mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo nataka kufahamu Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba makumbusho haziishii tu ziwe za siku nyingi, kwa sababu kila siku zinazaliwa

historia nyingine. Wamejipanga vipi katika kuendeleza masuala ya kimakumbusho. Kuna mwongozo wowote ambao upo kwa ajili ya kuendelea makumbusho? Nasema hivyo kwa sababu hata *CAG* ameuliza swali hili. Kwa hiyo, nimeona na mimi niongeze mbele lakini pia hata nikifuatilia katika baadhi ya maeneo naona makumbusho ziko maeneo machache sana. Hapa Dodoma sijui lini sasa tutaijenga makumbusho kubwa kabisa ya Kitaifa. Kwa hiyo, niwaombe sana suala la makumbusho ni muhimu kwa sababu watu tunakuja, tunapita, vitu vinakuja vinapita, historia zetu zinakuja zinapita lakini tunapokuwa tumeziweka vizuri zinasaidia hata watoto wetu kujifunza hatua kwa hatua za mabadiliko na maendeleo yetu katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na suala la Makumbusho ya Taifa ninazidi kuwaomba kwamba katika makumbusho mojawapo ambayo ni ya Majimaji kule Songea bado pamoja na kwamba sasa hivi tunaona kila mwaka ina adhimishwa inapofikia tarehe 27 mwezi wa Pili lakini ile jitihada ya Serikali ya kuwekeza bado ni kidogo, ndiyo maana hata wenzetu wa kule Nandete Rufiji wanalalamika. Kumbe tungeunganishwa sasa hivi tukawa kama *circuit* moja, makumbusho kimsingi, kisheria, ikishakuwa imekaa zaidi ya miaka 100 *automatically* inakuwa imeshaingia kwenye kuwa ni Makumbusho ya Kitaifa. Sasa wale Nandete kwa nini kila siku wanakumbusha jambo hilo hilo? Kwa hiyo, mimi niwaombe sana Wizara katika suala hili la kuunganisha hizi historia zetu hizo hazitaki mjadala mrefu. Kinachotakiwa ni sisi kuhakikisha kwamba tunajipanga na kuona kwamba makumbusho hizo zinawekwa katika historia yake inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwamba, Wizara hii imepata viongozi vijana, kuna kufanikiwa katika wanayofanya, kuna kukosea kutokana na ujana wao na sisi kila siku tunasema kwamba vijana wapewe nafasi, basi pale wanapokuwa wameteleza tuwaelimishe kwa upole, tuwasaidie ili waendelee kufanya vizuri, hiyo itakuwa ndiyo Tanzania tunayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Felix Kavejuru Eliadory, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai lakini pia nawashukuru wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikano. Kabla sijaendelea naomba kwanza nikupongeze wewe mwenyewe umewapa akinamama moyo kwamba wanaweza kwa kuwa Spika lakini pia kwa kugombea nafasi kubwa ya Umoja wa Mabunge Duniani, hongera sana. Naamini kabisa watoto wa kike walioko shuleni tayari nao wanandoto kwamba siku moja wataiga mfano wa Mheshimiwa Spika wetu anaegombea nafasi kubwa sana Duniani. Mwenyezi Mungu akubariki nasi tujivune Tanzania kwamba tuna kiongozi mkubwa duniani.

**MBUNGE FULANI:** *Halleluya*! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali inayongozwa na Mama yetu mpenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli kazi wanayofanya ni kubwa na inaonekana jinsi ambavyo maendeleo yanapatikana katika nchi yetu. Nichuke nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Naibu wake, Wakuu wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara, kwa kweli kazi mnayo kubwa na mnaitendea haki Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa niaba ya wananchi wa Urambo na hasa ambao hoja hii inawagusa ambao ni Wananchi wa Kata ya Nsenda ambako ndani yake kuna vijiji vya Lunyeta, Lutenge na Mtakuja lakini pia Kata ya Ukondamoyo ambayo ndani yake vijiji vinavyohusika ni Ifuta, Tumaini na pia Utewe. Wananchi hawa nimeshawasemea suala lao mara nyingi hii siyo mara ya kwanza na nitaomba tu Wizara ikaangalie katika kumbukumbu zake kuna barua nyingi ambazo nimeandika kuhusiana na ombi ambalo nalileta rasmi hapa mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Urambo tunategemea sana zao la biashara tumbaku lakini zao la pili ni asali. Kwa kutegemea asali sasa, tuliomba msaada wa Wizara hii hii ya Maliasili na Utalii watusaidie kutupa mashine za kuchenjua asali ili na sisi tusafirishe nje ya nchi. Tukapata watu waliokuwa wanataka asali yetu wanaitwa *Follow The Honey*. Walikuja na tukakubaliana nao. Tukafanya umoja wa wananchi wafugaji wa nyuki, tukatengeneza mahali pa kukusanyia asali na Wizara tulipoiomba ije itusaidie walikuja, walimtuma Mkurugenzi akaja akaona na kweli akaahidi kwamba Wizara itatuunga mkono katika kuimarisha hili zao la asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika harakati zile zile za ahadi ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii Serikali ikaleta Azimio hapa la kuchukua Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla. Sisi tukashukuru kwa sababu pia nasi tunapata faida. Watu wetu wananufaika na misaada mbalimbali na tunakubaliana na wazo la kuhifadhi misitu kama hii. Tatizo lililojitokeza na naomba niliweke wazi hapa, hakukua na ushirikishwaji wa wananchi. Wananchi walishtukia tu siku yenyewe tayari kuanzia leo hamuingia hapa. Imekuaje na sisi tulikua tunaishi miaka yote hii? Marufuku hamruhisiwa kuingia humu. Watu wakashangaa lakini kuna historia yake nyuma mbaya ambayo wakawa wanaikumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, 2013/2014 hawa watu walilima mazao yao yakachomwa na Tume ikaundwa, kwa kweli bado walikuwa wana uchungu wao wa mwaka 2013/2014. Kwa hiyo walipokuja tena tukasema; Hee! hii Serikali yetu vipi? Hakuna kukaa pamoja walituchomea mazao yetu tunaambiwa tu kuanzia leo hamuuingii huku. Kwa hiyo, ikaleta taharauki.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kwamba wananchi wa Urambo tunaikubali hifadhi tunachoomba kwanza ni kushirikishwa, pili ni kuelimishwa, hifadhi maana yake nini? Halafu pia nashukuru Serikali hii hii ya nchi yetu ilimtuma Mheshimiwa Hasunga, akiwa Naibu Waziri alikuja akaona, kwamba mpaka wao wa zamani ulirudidshwa nyuma baada ya *TANAPA* kuja kuweka mipaka yao na wana namba zao 23, 22 na yeye mwenyewe Mheshimiwa yule pale alishangaa wanafukua kwa

mkono tu, wakaoneshwa kwamba jiwe letu 23, 22 mmeliruka mmeturudisha nyuma sisi lakini watu wameongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachomba, kwa heshima na taadhima Mheshimiwa Mchengerwa tunajua kazi yako ni nzuri ulipotoka, kwenye mabanda hayo tumekuta picha zako zimejaa mule, kazi uliifanya vizuri. Tunaomba wananchi wale washirikishwe, wanaomba kwa kupunguza eneo lao hawana mahali pa kuweka mizinga na alipokuja Mheshimiwa Rais Tarehe 30 mwaka jana Mwezi wa Tatu, hili pia aliliongea mbele ya Mheshimiwa Rais kwamba wanakubali kuwa na hifadhi lakini wanaomba waongezewe eneo la kuchungia mifugo yao na kuweka mizinga yao. Kwa sababu tayari tulishaweka mahali pa kukusanyia asali, walishaunda umoja wao na ninyi wenyewe kama Wizara mkamtuma Mkurugenzi akaja akaona akakubali, hasa mmetutoa tayari. Asali hatuwezi kupata tena kwa sababu mmetupungizia eneo, kwa hiyo mimi kwa sasa hivi natoa maombi tu kwako wewe ili Mheshimiwa Waziri ayachukue.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wananchi washirikishwe, maana ya hifadhi ni nini? Ina manufaa gani kwao? Kwa undani waelewe halafu tuombe pia kwa heshima na taadhima mtupe eneo warudishe mizinga. Hawawezi sasa hivi kuweka mizinga ili wale watu ambao tulikubaliana *Follow The Honey* waje tuendelee kuwapelekea asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo wanaomba pia, tuna *WMA* yaani kuna eneo ambalo wanakuja watu kuwinda, sasa kuna madai fulani ambayo wanayo wale wananchi wa Uyumbu, *WMA* ya Uyumbu wanaomba kuna malipo ambayo wanahitaji ya mwaka 2021/2022 ili kurudisha mahusiano.

Mheshimiwa Spika, hatukatai kuwa na hifadhi, tunawashukuru na hili ombi tulishapeleka, kile kikundi kilichoundwa cha Mawaziri Nane walikuja lakini ndiyo walituacha hoi. Jibu lililotolewa pale lilituacha hoi, lakini bado wanaimani na Serikali yao kwamba itawafikiria ili warudishiwe eneo kiasi ili na wao waendelee kuchunga ng’ombe lakini pia na kuendelea na mizinga yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kwa kifupi nasema tu kwamba ombi langu ni hilo, tunathamini sana hifadhi lakini bado tunaomba eneo. Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felix Kavejuru Eliadory atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Minza Simon Mjika ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia kwenye hoja ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mhifadhi namba moja na mtangazaji wa vivutio vya utalii namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ninampongeza Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango kwa juhudi kubwa na kazi kubwa anayoifanya ya kuhifadhi mazingira hapa nchini. Kipekee nishuke kwa Mheshimiwa Waziri nimpongeze rafiki yangu Mchengerwa mtu kazi pamoja na Dada Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbasi Said, Naibu Katibu Mkuu Anderson Mutatembwa kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja waliyoiandaa ambayo sasa tunaijadili kuna mikakati mikubwa sana. Katika mchango wangu nitachangia mambo mawili tu. Moja ni maombi kwenye sehemu mbili ambazo zina migogoro kule Mkoani Kigoma. Mgogoro wa kwanza lipo eneo ambalo lina itwa Kagerankanda iko Kasulu, eneo hilo ni tegemeo kwa kilimo cha mahindi na maharage kwa Wilaya karibu tatu za Kasulu, Buhigwe na Kigoma Kaskazini. Uko mgogoro ambao umedumu kwa muda mrefu kati ya *TFS* na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu chanzo chake ni *TFS*. Mvua zinapoanza kunyesha wakulima huruhusiwa kwa sababu hawajui mipaka na mipaka haijajulikana, *TFS* wanawaacha wanalima, wanapalilia, wanaweka mbolea ikifika wakati wa kuvuna kiangazi kama hiki, wanawazuia kuvuna mazao yao au wakienda kwa kujificha wanawanyang'anya mazao yao, hiyo ni dhuluma!

Ninakuomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mchengerwa mtu kazi ushuke pale ndani ya Wilaya ya Kasulu uwasikilize wakulima utatue mgogoro huo na mipaka iwekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa pili ni wa Kijiji cha Karirani kiko katika Wilaya ya Uvinza, kinapakana na Hifadhi ya Milima ya Mahale. Kijiji hiki kilisajiliwa mwaka 1995 na kina barua ya usajili ya tarehe 5 Juni, 1995 na kina usajili wa Namba 244. Kuna taharuki kubwa sasa hivi katika kijiji kile. Tarehe 13 Machi mliwapelekea barua kuwaonesha katika vitongoji vinne kati ya vitongoji vinne katika Kijiji cha Karirani vitongoji viwili mnasema viko kwenye sehemu ya hifadhi. Vitongoji hivyo ni Mahasa na Kabukuyungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitongoji hivi vina kaya 479 zenye idadi ya watu 1,721. Kuna taharuki kubwa, hawa ni Watanzania, wamekaa pale zaidi ya miaka 28. Eneo hilo ambalo mnarudisha kwenye hifadhi ya Milima ya Mahale lina Shule ya Msingi, lina makanisa sita, lina misikiti miwili na taasisi zingine za Kiserikali wana nyumba za kudumu. Mmepeleka barua mwezi wa Tatu tarehe 30 mnatuma Kamati ya Ulinzi na Usalama kuwajazisha fomu waondoke bila kuongea nao. Hiyo siyo halali, haikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani hifadhi yoyote ile *conservation is for human development* ni kwa ajili ya maendeleo ya watu. Ni lazima mshuke muwashirikishe wananchi. Hatukatai, tunajua mnayo programu ya kuhakikisha kwamba zile shoroba ambazo zilijengwa sasa ziwe wazi lakini muende kwa utaratibu wa kiutu. Tunataka fedha lakini hatutaki migogoro. Hatutaki kuona kila mwaka kwenye taarifa au kwenye ripoti kwamba askari wangapi wameuawa, au wananchi wangapi wameuawa. Hatutaki fedha tutakazozipata kutoka kwenye Wizara hii zingine ziwe zimeambatana na damu ya watu. Itakuwa ni dhuluma, hatuwezi kubarikiwa kama Taifa na hatuwezi kupata baraka. Ninakuomba sana ushuke pale Karirani uwasikilize wananchi wako, ni Watanzania uwasikilize muyaweke mambo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni ya ushauri. Nimesoma bajeti yako ukurasa ule wa 27 kuna biashara ya hewa ya ukaa, nami ninaenda kuungana na Mheshimiwa Reuben kwamba makusanyo yanayokusanywa na Wizara yako bado ni madogo. Sasa hivi kuna biashara ya hewa ya ukaa na nimeona mmeingia mkataba na kampuni mbili. Ipo Kampuni hii moja ya Singapore ambayo inaonekana tayari mmekwisha ingia mkataba na mmelipwa shilingi bilioni 8.4. Je, mmeshindanisha? Bado mmeingia tayari kwenye mkataba na Falme za Kiarabu kuna Kampuni hapo inaitwa *Carbon Cop;* je, mmeshindanisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii kwenye maliasili kwenye misitu tunayo misitu ambayo ni *natural forest* zaidi ya 452 na tunayo misitu ambayo iko chini ya Halmashauri ambayo inamilikiwa na Halmashauri 46 lakini inatia aibu mpaka sasa hivi katika nchi nyingi wenzetu majirani wa Kenya wanavuna fedha nyingi kutokana na biashara hii ya ukaa, sisi bado tuna misitu hii miwili. Je, mmekwisha fanya tathmini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii ya hewa ya ukaa imezungumzwa kwenye Wizara ya Mazingira na ninyi mmeizungumza. Je, fedha ambayo sasa mmepanga au kwenye mkataba huu ni Wizara ipi itakayohusika na makusanyo hayo? Ninaomba utakapokuja ku-*finalize* mtuelekeze ni Wizara gani hasa itakayohusika kwa sababu Wizara ya Mazingira ndiyo imetoa mwongozo namna gani hiyo biashara inaweza ikafanyika lakini tunaona tayari kwenye mikataba tayari iko ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii na tunaomba hawa *TFS* ambao wanatumia nguvu kubwa kupitia Askari Wanyamapori ambao wanatumia nguvu kubwa ya kuonea wananchi waumize kichwa sasa hivi wasaidie namna ya kuwashirikisha wananchi kwa sababu wananchi ndiyo wahifadhi namba moja. Hakuna usalama bila kushirikisha wananchi. Hao ndiyo wahifadhi namba moja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mimi ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja na ninakuombea sana kwenye lile jambo lako ambalo umeomba tunakuombea

ushindi wako itakuwa ni heshima kwetu. Uthubutu wako ni heshima kwetu na Mungu akutangulie na akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi kuweza kusimama kwenye Bunge lako pia kuchangia kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Ninamshukuru sana pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa yako hii iliyopo mezani pamoja na Naibu wako Waziri. Pia niwapongeze sana Watendaji wako wa Wizara kwa uandaaji mzuri na kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya ya kuifanya Wizara hii iwe Wizara nzuri ambayo inachangia Pato kubwa la Taifa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo lakini pia nitakuwa nimefanya makosa makubwa sana nisipompongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya hususan kwenye Wizara hii. Hatujawahi kuona tokea dunia iumbwe Rais kufanya kazi kubwa mno kwa kipindi kifupi hususan kwenye Wizara hii, Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa kweli Mheshimiwa Rais anahitaji pongezi kubwa mno na anahitaji kila pongezi, kila namna kwa namna ambavyo Rais alivyojitoa muhanga kuitangaza nchi yetu Kimataifa lakini ndani ya nchi kwenye Wizara hii ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, leo tumeona wimbi kubwa la wageni ambao wanatoka nje, *international* kuja nchini kwetu Tanzania. Miaka ya nyuma tumeshuhudia kipindi kama hichi mwezi wa tatu mpaka mwezi wa sita ni kipindi cha *low season* lakini leo hii tunaona ndege nyingi sana ambazo zinatua ndani ya nchi kana kwamba ni kipindi cha *high season.* Kwa kweli anastahiki kila pongezi Mheshimiwa Rais. Ameifanya *low season* sasa hivi kuwa *high season.* Ni *season* nzuri tuna wageni wengi sana sasa hivi nchini kwetu namna ambavyo tayari wanavyokuja, namna ambavyo mama alivyoitangaza nchi, namna ambavyo wageni ambavyo wanavyoingia ndani ya nchi kwa ajili ya kuja

kutembelea ndani ya nchi lakini pia kujifunza mambo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi nitajikita zaidi kwenye utalii wa fukwe. Ingawa nchini kwetu tuna fukwe nyingi lakini bado hatujazitumia vile ambavyo inatakiwa ukilinganisha na nchi nyingine. Utalii wa fukwe sasa hivi duniani ndiyo utalii ambao unatembelewa na wageni wengi nchini duniani. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara lazima tuweke mikakati madhubuti ili kuinua Wizara hii kwenye Sekta hii ya Utalii wa Fukwe. Mfano mzuri nilipoangalia kwenye mtandao wa *BBC* hivi karibuni wametoa taarifa yao 31 Machi, 2023, watalii wengi ambao wametembelea duniani ni watalii ambao wameenda kwenye fukwe ukilinganisha na maeneo mengine yoyote yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri nchi ya kwanza ambayo inaongoza kuwa na wageni wengi lakini wote wameenda kwenye fukwe ni nchi ya Brazil kwenye eneo la *beach* ambalo linaitwa Santos lakini pia nchi ya pili ambayo imeongoza pia kuwa na watalii wengi wameenda kutembelea kwenye fukwe ni Accra lakini pia kuna nchi ya Australia lakini kwenye tathmini yote *overall* Marekani ndiyo inaongoza kutembelewa na wageni wengi kwenye eneo la *beach*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni wazi sasa lazima tuweke mipango mikakati ili kuhakikisha sasa tunakuwa na utalii wa fukwe. Kwenye nchi zaidi ya 30 zilizotajwa kwenye ripoti ya *BBC* Zanzibar imetajwa kweye eneo la Nungwi na eneo la Nungwi ni eneo ambalo limeshamiri kwenye utalii wa fukwe. Ni fursa pekee sasa hivi lazima tuwekeze huko kwenye eneo la fukwe. Watalii wengi duniani ndiyo wanakuja kwenye eneo la fukwe ukilinganisha na maeneo mengine, yote ni mazuri hayo, yote ni mazuri lakini kwenye fukwe zaidi ndiyo wanapendelea zaidi, wanapendelea zaidi ku-*pleasure,* kustarehe, kutembelea *beach,* kuota jua na mambo mengine hali kadhalika ukilinganisha na maeneo hayo ya wanyamapori pamoja na milima. Kwa hiyo, naiomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa huku kwa upande wa bara ardhi upande wa *beach* kwenye fukwe wameachiwa wenzetu wa Halmashauri na Serikali za Mitaa. Naiomba sana Wizara mtumie *technique* yoyote ile ili kuhakikisha sasa Wizara ndiyo inahodhi maeneo yale na hii Halmashauri pamoja na Serikali za Mitaa mnaweza mkatengeneza sheria na utaratibu mzuri ili ziweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ikitengeneza Tume kwa ajili ya kuchukua maeneo ya *beach* na kuyaendesha basi tuhakikishe kwamba tunaweka sheria na kanuni za *Corporate Social Responsibility (CSR)* ili vijiji ambavyo vitatoa ardhi yao kwa matumaini kwamba watahisi Serikali itaweza kuwasaidia basi mahoteli yale au wawekezaji hao wawe wanakumbuka kutoa gawio la faida kwa vijiji ambavyo vipo karibu, vitapata faida ya kujengewa mahospitali, vitapata faida za kujengewa mashule lakini pia vitapata faida vya kujengewa *transportation*. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze sana baada ya kuzindua hiyo filamu yetu lakini pia tuna *tv* yetu inaitwa Safari ambayo hiyo inamilikiwa na Maliasili, kwa hiyo niwapongeze sana kwa hiyo, lakini pia niwaambie kitu kimoja, mbali na *tv* sasa hivi mambo yetu haya yamehamia kwenye mitandao ya kijamii sasa hivi, tunao vijana wetu ambao wanatangaza sana kwenye utalii na ninaamini tukiwatumia vizuri nina uhakika tunaweza tukaongeza mara dufu watalii kupitia nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao vijana wetu naomba uniruhusu niwataje, yupo kijana ambaye anaitwa Yasini Jamal ni kijana ambaye ukifungua kwenye mitandao ya kijamii ana *followers* wengi na anauwezo mkubwa sana wa kuitangaza Tanzania kwenye *issue* ya kiutalii. Pia tunaye kijana wetu anaitwa Ally Jape ni vijana ambao wote wana uwezo mzuri wa kuutangaza utalii. Kwa nini tusiwachukue vijana hawa tukawafanya kama mabalozi wa kuweza kuutangaza utalii wetu ndani ya nchi? Ninaamini tukiwapa fursa hawa vijana wataitangaza sana nchi yetu kwenye sekta ya kiutalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niende kwenye eneo la pili. Watalii wengi nao wanaokuja ndani ya nchi wanavutiwa na vyakula. Kwenye eneo la vyakula bado hatujaweka mikakati madhubuti ili watalii wengi wanaokuja nchini basi wa-*recognize* kwenye *issue* ya chakula. Mfano mzuri tuna nchi nyingi sana kama India, watalii wengi wanaoenda India wanafuatilia masuala ya chakula. Ukienda Japan watalii wengi nao wanaenda Japan kwa ajili ya kufuata *taste* ya chakula lakini pia kwa upande wa Zanzibar, watalii wengi wanaenda Zanzibar na wao pia mbali na *beach* lakini pia wanafuatilia masuala ya chakula. Kwa hiyo naamini tukiweka hasa utalii wa chakula tutafanikiwa kwa asilimia 100 na ndiyo fursa yenyewe pekee hiyo tunaweza tukaitengeneza watalii wakaja wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri leo hii Zanzibar kuna tamasha ambalo linaendeshwa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja anaitwa Ayoub Mahmud. Huyu anastahiki pongezi za hali ya juu, tarehe 25 Juni, kuna tamasha Zanzibar linaitwa Zanzibar *Seafood Festival.* Tunaanza na tamasha mwisho wa siku matamasha kama haya yanakuwa ni sehemu ya kichocheo cha kuvutia wageni wengi nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo nchi nyingi sana zimefanikiwa kwenye matamasha haya ya kiuchumi kwenye suala hili la vyakula. Kwa hiyo nawaomba sana, naiomba sana Wizara tuangalie kwenye suala la chakula. Leo hii kuna ma-*chef* wengi Afrika Mashariki wamekutana walikuja kushangaa Tanzania tunapika ndizi kwa nyama ambayo duniani kote hakuna. Tukilifanya hili jambo kama ni fursa ya kiutalii tumetengeneza uchumi wetu, tumetengeneza ajira kwa vijana wetu, pia kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Minza Simon Mjika atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Mwanakhamis Said ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia. Napenda kumshukuru Mungu kwa vile amenipatia nafasi nzuri na siku njema kama hii ya leo kuweza kusimama hapa na kuongea yale niliyonayo. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Rais wetu Mama Samia, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kufanya katika nchi yetu. Ni kweli amekuwa mama wa mfano kiongozi wa mfano Rais wetu, tuzidi kumuombea awe na afya njema na aweze kutimiza maono yake kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninakushukuru sana Spika wetu kwa kazi kubwa ambayo iko mbele yako, tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu asimame na uweze kushinda, hakika tunapoomba muda wote Mungu anasikia maombi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru Waziri Mchengerwa pamoja na Naibu wake, Katibu, Naibu Makatibu kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Nimeendelea kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kazi anayoifanya ni nzuri. Wizara hii ni nyeti sana, ina muingiliano mkubwa sana na ina ugomvi mkubwa sana, lakini Mungu awaongoze katika hilo mkubali kushauriwa na mkubali kubadilika mambo yenu yataenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yangu kwa kazi ambazo zinaendelea kwa sasa, Rais yetu Mama Samia *royal tours* imeleta mambo mazuri sana, tumeona wageni wengi wanaongezeka kila leo na tunapata fedha za kigeni tunashukuru kwa hilo. Pesa zile zimeingia katika maendeleo ya nchi tunapata barabara, tunajenga hospitali, tunajenga vituo vya afya na maendeleo mengine mengi nchini yanapatikana kulingana na hii ziara ya mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru wawekezaji wetu ambao wapo katika nchi yetu ambao wanakuja kwa ajili ya kutembelea na kutupatia fedha nyingi. Sitaki niongee zaidi kwa sababu naona muda wote ni mdogo nataka niseme habari ya Simiyu. Simiyu ina Wilaya Nne ambazo zinachangamoto kubwa sana ya tembo. Kuna Wilaya ya Busega, Bariadi, Itilima, Meatu.

Wilaya hizi zinazo changamoto kubwa sana kila leo wananchi wanauawa ni hakika nadhani hata wewe Waziri taarifa hizi unazipata.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba wananchi wa kule wamekuwa na tatizo kwa muda mrefu sana, kila siku wakinababa ni kulala nje kwa ajili ya kulinda tembo, tembo ni wengi kupita kiasi. Tembo wameleta madhara makubwa sana katika Mkoa wetu wa Simiyu, wameua akina baba, akina mama, watoto na wanafunzi wakati wanaenda shule, imefanya hata maendeleo ya baadhi ya wanafunzi kutokuwa mazuri kwa sababu hawaendi shule kwa ajili sababu ya tembo kuwa wengi kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, tembo hao wameleta madhara mengine ya kula chakula kikiwa shambani na kikiwa nyumbani. Tembo ni mnyama mwenye vurugu sana kwa kweli, ni ambaye kweli anavuta watalii wengi wanakuja kumuona hapa Tanzania lakini ni mnyama ambaye analeta madhara makubwa sana, amesababisha vifo vingi sana, ulemavu, ameleta njaa ameleta shida mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri napenda nikuambie kwamba katika Mkoa wa Simiyu kweli watu wengi wameuawa sana, lakini kumbuka kwamba katika Mkoa wetu wa Simiyu tunahangaika na hawa wanyama kwa muda mrefu sana. Mwaka jana tulisema walau mtupatie magari ya askari *game* hakuna hata gari katika Wilaya ya Meatu na Wilaya ya Bariadi lakini wanyama muda wote wapo wanaingia mpaka sokoni ni muda wa kukimbia tu kina wakimama, wakibaba hawapati amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanyama hawa wamekula sana mazao unakuta katika Wilaya zetu hizo kuna njaa kubwa sana kwa ajili ya ukosefu wa chakula kwa ambao wanakaa pembezoni mwa sehemu hizi zenye wanyama hawa. Tunaomba Serikali iweze kutusaidia hili, ninaamini kiongozi wetu Waziri wewe ni msikivu, nilikuambia hata siku moja kwamba jamani mjitahidi kuleta amani hata maandiko matakatifu yanasema katika "Waebrania 12 – 14 tafuteni kwa juhudi kuwa na amani na watu wote" tunapokuwa

na amani ni jambo ambalo ni jema hawa watu wanalala nje, akinamama wanabaki wenyewe nyumbani, watoto wanashindwa kwenda shule, lakini Waziri ukifika pale na Naibu Waziri wako mkawasaidia hawa watu ni jinsi gani hawa wanyama basi waweze kulindwa na watu ambao wamesomea yale mambo ili kwamba wale watu waweze kupata amani. Kweli imekuwa ni shida ni kukimbizana muda wote watu hawana hata kazi za kufanya. Mheshimiwa Waziri jitahidi kwa hilo, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge mmoja hapa amesema mimi hilo jambo kila siku nilikuwa nawaza akili kwangu, kwanini msijenge *fence* kwa ajili ya hawa wananyama wasiwe wanavuka kuingia kwenye makazi ya watu? Zijengwe *fence* kama vile yalivyo Magereza ya nchini Tanzania *fence* ndefu mnyama hawezi kuvuka ili tuleta amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, familia nyingi kule zinalia zimepoteza watoto kinababa wamefariki, kinamama wamefariki wengine wamepata ulemavu. Kwa hiyo, unakuta kwamba hata wale manyama watu wanawachukia kwa sababu ya changamoto kubwa kama zile. Waziri wetu jitahida sana kufatilia mambo kama haya. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hapa Jacquline Ngonyani Msongozi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacquline Ngonyani.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba, kutokana na kadhia hiyo kwamba watoto wanashindwa kwenda shuleni lakini pia hao tembo wameweza kufika mpaka majumbani wanavuna mazao na wakati mwingine wanachua vyakula mpaka vya nyumbani wanakula.

Mimi nilikuwa nadhani kwamba sasa hawa tembo wangevunwa ili kupunguza hiyo kadhia wabakizwe wachache, hawa wachache watakaobaki waendelee kuzaa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Nilikuwa naelekea kusema kwamba kwa mfano mfugaji anapofuga anakuwa na ng'ombe wengi sana, ng'ombe wanazidi inabidi awapunguze wengine aende kuwauza mnadani apate pesa afanyie shughuli zingine za maendeleo. Hata hawa tembo wamekuwa wengi mno na ndiyo maana wanatembea huku na huku, si wavunwe wauzwe basi tupate hata fedha za kigeni? Itakuwa ni jambo jema kuliko kutesa wananchi muda wote wanakimbizana kwa ajili ya tembo, kila leo unapigiwa simu tunaomba hela ya tochi, tunaomba hela ya turubai, tunaomba pesa ya nini?

Tunaomba Waziri Mchengerwa utusaidie na tunakuomba ufike katika Mkoa wetu wa Simiyu. Ufike katika Wilaya zile ambazo zinahangaishwa na hawa Wanyama, utaona heka heka ya kinababa ambao wanayo kule, hawalali nyumbani muda wote wako porini jamani hebu tuangalie hawa watu kweli? Kuna Mheshimiwa mmoja anapenda kusema kwamba changamoto ya akili, matatizo ya akili wale watu hawawezi wakawa na akili nzuri. Kwa sababu hawatulii majumbani kwao na weka zao na familia zao, muda wote wanalala porini je, watapata amani kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba wanyama hawa ndiyo hatarishi sana katika Mkoa wetu wa Simiyu, hakuna mnyama mwingine mwenye vurugu kama tembo. Tunaomba Serikali iangalie kama ni kuwavuna basi wavunwe, sasa hivi wameingia katika hizo Wilaya toka mwezi Novemba mwaka jana, mpaka sasa hivi wako kule wanakula chakula shambani, wanakuja nyumbani, hata akikuta ni kubinua tu lile bati anaanza kula huyo mnyama ni mnyama mwenye vurugu sana, lakini hakuna mtu anayeweza kupiga kwa sababu wananchi wanaogopa sheria. Tunaomba Serikali basi iweze kuwavuna wanyama hao na sisi wananchi wetu waweze kuishi kwa amani na waweze kuwa na amani kama wapo katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema juu ya hawa wawekezaji wetu, kwa mfano Mwiba. Nashukuru kwamba si

kwamba hawasaidii, wanasaidia katika maendeleo na ni wadau wa maendeleo pia. Kwa mfano, katika shule ya sekondari Paji, Mwiba ametoa baiskeli 200. Wanafunzi wamepata baiskeli ambazo zina thamani ya milioni 40 na kuendelea lakini pia wamejenga shule, wamejenga madarasa, tunawashukuru wale wawekezaji, si kwamba tunawachukia lakini kero ni kwa wale wanyama tu basi, ikitoka hiyo kero wala hatuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mwekezaji huyo tunapenda kumshukuru sana ameamua kuanzia mwezi wa Saba wanafunzi watakula shuleni muda wote. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa huo uwekezaji, wawekezaji wetu waliyopo hapa nchini kwa ajili ya kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mchengerwa ninazidi kukuomba Waziri wangu endelea kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Simiyu na Wabunge wengi hapa wanaongea wanalalamika hilo jambo, tafadhali mtusikilize ili familia za kule ziwe na amani ili familia za kule ziwe na furaha, wanapolima wapate chakula wasije wakawa ombaomba kwa sababu ya kufirisiwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema awali majina ni mengi sana hapa na kila mtu baada ya kusema waliyochangia mara nyingi hawatachangia, vikaratasi vimezidi hapa mbele. Kwa hivyo wanaochangia kuanzia sasa watachangia dakika sita ili tuvute wachangiaji wengi zaidi. Mheshimiwa Haji Amour Haji atafuatiwa na Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, kwanza kabla ya yote nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Pili nakupongeza wewe kwa namna ya unavyoweza kufanyakazi zako pia na namna ya *philosophy* ambazo

unazozitumia katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu nawapongeza, nampongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Wizara yetu hii ya Utalii pamoja na mambo ya *natural resource* mambo ya Maliasili na Utalii, lakini pamoja na yote, pamoja na kuwapongeza lakini pia nawapa pole. Kwa sababu asilimia kubwa ya Wabunge hapa wanawapongeza lakini wakati huo huo wanakuwa na kitu kama lawama kidogo na hasa kwa upande ule wa maliasili. Kwa hiyo, kwa upande ule kule mimi nawapa pole sana, kwa sababu hili jukumu la maliasili ni jukumu ambalo ni zito na kwa nini nazungumza kwamba ni suala zito? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya namna ambavyo ya uasili wake, na siku zote kitu ambacho ni cha asili maana yake siku zote kitakuwa na lawama na ulawama wa asili maana yake huja pale kwamba huna namna ya kuweza kubadilisha. Kwa sababu hapa katika Bunge letu hili utakuta kwamba Wabunge wengi wanalalamika juu ya tembo na mambo mengine kitu ambacho tembo kwa namna ya uasili wake inakuwa ni vigumu sana kuweza kubadilisha na huna namna. Naamini pengine nitakwambia kwamba muweze kukubaliana tu na hizo lawama mnazopewa kwa sababu ya ule uasili wa mambo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nadhani kwamba leo nijikite zaidi kwa upande wa utalii. Utalii wetu wa Tanzania ni utalii ambao ni wakimaumbile, kwa ufupi kwamba naweza kusema kwamba Tanzania hatujawa na ile *vision* ya moja kwa moja katika suala la utalii kwamba tunaelekea katika utalii wa aina gani?

Mheshimiwa Spika, utalii ni kitu ambacho ni kikubwa sana, na mimi kama ningekuwa natoa ushauri kwa namna ya ukubwa wa Wizara na namna ambavyo ilivyo kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii maana yake mimi nigeliweza kushauri tu kwamba huu utalii kutokana na namna ambavyo uwekezaji wake pengine mimi ningeshauri Serikali pengine suala na maliasili likabaki na upande wake na utalii ukabaki upande wake, na kwasababu utalii kwa namna yoyote ile ni sekta ambayo inayojitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia suala la utalii. Utalii ndiyo unaojenga kila kitu, tukiangalia hasa katika masuala ya *component* za utalii, utalii maana yake umejigawa katika *component* karibu sita, kuna suala la vivutio vya utalii. Vivutio vya utalii maana yake vinajenga pamoja na hizo rasilimali ambazo ndiyo tunazozungumza za misitu pamoja na vitu vingine. Sasa huo wote ni utalii. Tukizungumzia suala la *accessibility* maana yake yale mambo ambayo ambayo yaliyokuwemo katika ile nchi, maana yake tukiangalia suala la fukwe na mambo mengine, haya yote maana yake tunazungumzia suala la utalii.

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia suala la *accommodation* ambalo ni malazi ambayo nalo ni suala utalii. Tukizungumzia suala la *amenity* ambalo ni suala pengine la yale mahitaji yaliyomo katika nchi ni suala la kiutalii, pamoja tukizungumzia na *activity* zile shughuli zilizomo maana yake ni suala la tunazungumzia ni utalii. Sasa utalii ni kitu ambacho nachozungumza kwamba ni sekta moja ambayo ni muhimu sana na ndiyo ni sekta ambayo mama. Kwa sababu kwa nchi za wenzetu mara nyingi jina la utalii hutangulizwa mwanzo lakini sisi maana yake kwamba kama Tanzania tumetanguliza maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa maliasili na utalii lakini utakuta kwamba maliasili kwa upande wetu maana yake imebeba sehemu kubwa sana hasa katika masuala ya majadiliano, ukiangalia hata kwenye Bunge letu hili maana yake utalii unazungumzwa kama ni *component* ndogo sana. Wakati utalii ndiyo inayojenga hivyo vitu vingine, hata suala la utalii maana yake tukisema suala la utalii maana yake utalii unatakiwa iwe ni sekta mama, kwamba ni utalii ambao ni sekta ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale au Wizara ya Utalii na Maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii pengine mimi ningesema kwamba uwe unaanza mwanzo kisha baadaye ije maliasili, kwa sababu kwenye maliasili ni kitu ambacho kuna vivutio kule. Kwa sababu vivutio vile maana yake ndivyo vinavyoitengeneza hiyo sekta ya utalii katika masuala ya kibiashara, na biashara yetu maana yake tunategemea nini? Tunategemea hizo mbuga za wanyama, tunategemea nini? Tunategemea misitu, tunategemea nini? tunategemea hoteli, tunategemea nini? tunategemea fukwe,

tunategemea nini? tunategemea kila aina utamaduni wetu maana yake yote, maana yake ni moja ya utalii hasa utalii maana yake tukiwa tunauweka katika sehemu ndogo itakuwa kidogo tunaupa nafasi ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua kwamba unaniangalia kwa sababu ya dakika cha msingi niunge hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanakhamisi Kassim Said atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete na Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate ajiandae.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Wizara hii ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya jumatatu ni siku tukufu ni siku nzuri sana kwa hivyo nakuombea dua kwa Mwenyezi Mungu akujalie kwa jambo lako hilo unalokwenda kulifanya la huko Duniani ufanikiwe. Kufanikiwa kwako ni kufanikiwa watanzania, kufanikiwa kwako ni kufanikiwa Wabunge, kufanikiwa kwako ni kufanikiwa Wanawake hususani wa Jimbo lako la Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan bado kuendelea kupambana na nchi yake lakini kuiletea maendeleo nchi yake. Nimpongeze Dkt. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini nirudi kumpongeza Dkt. Hussein na Mama Samia Suluhu walivyotangaza *Royal Tour* walitangaza jambo hili kwa upendo mkubwa, kwa ukakamavu mkubwa na kwa kuwa na moyo wa dhati wa nchi zao au wa nchi yao ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi walitangaza utalii wa fukwe,

walianza huko wa Bahari halafu wakaja kwenye zetu za utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini jambo hili Viongozi wetu wa nchi kutangaza utalii? Kwa sababu hizi ni rasilimali za nchi yetu na ndizo tunazozitegemea na rasilimali zetu hizi ikifika miaka kumi, kumi na tano basi Mheshimiwa zitapotea. Kwa hivyo, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Mama Samia walisimama kidete kutangaza utalii wa nchi zetu mbili hizi iliyobaki Watanzania nasi lazima tuwaunge mkono Viongozi wetu waandamizi wa Nchi kwa juhudi kubwa waliyofanya kutangaza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kweli wanakazi kubwa sana kwa sababu Mheshimiwa kila aliyenyanyuka alimzungumza tembo. Sasa siye kama kazungumzwa tembo kwa kweli tunasema ni jambo kubwa sana hili kuzungumzwa tembo kama amekuwa anapiga watu sasa ni hatari! Namuomba Mheshimiwa Waziri hii tembo aidhibiti kwa nguvu zake zote pamoja na Naibu Waziri. Kwanza ana Naibu Waziri mkakamavu, muelewa, mchapakazi na Waziri umeingia kwenye Wizara ni Wizara ngumu sana, lakini Mungu atakusaidia. Kwa vyote anavyochakatwa huyo tembo lakini bado uendelee kupambana tembo wasiathiri wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwakweli ni hatari tena hii ni hatari kubwa sana, tembo wasiumize. Unao Askari wakakamavu, unao Kamati yako nzito, madhubuti na Waziri Mkuu anasaidia sana kutatua migogoro, sasa hii migogoro ya tembo sasa ataitatua vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwakweli Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi, Wizara hii ni Wizara ngumu, nzito sana ni Wizara iliyo na mambo mengi sana, lakini sisi tunasema unaweza, kwa sababu kule utamaduni ulifanya vizuri *Alhamdulillah*. Kwa hivyo na hapa tunataka uendelee kuchapa kazi, una Naibu Waziri ni Mwanamke lakini mwanamke shujaa sana, mtume Naibu wako Waziri anatumika usimuogope.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Askari wetu kwa kweli wanazungumzwa sana wao ni wanyonge, wamezaliwa kama sisi

kila mmoja mwenye mama yake naye anao mama yao. Leo askari imekuwa wapo kwenye matatizo makubwa sana, tunakuomba Mheshimiwa Waziri uwasaidie askari wetu, wapambane lakini uwasaidie kwa nguvu zako zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana, kengele imeisha gonga.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mhessimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kisha nikupongeze Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri unayoifanya ndani ya Bunge letu, hatimae sasa hivi unakwenda kugombea kule kwenye Mabunge ya Dunia kule. Wabunge Watanzania hatuna mashaka hata kidogo juu ya utendaji wako uliotukuka. Hakuna sehemu yoyote ile ambayo umeomba nafasi ukashindwa, kwa hiyo ndiyo maana sisi kama Watanzania tuna imani kubwa na wewe kilichobaki ni kitu kidogo tu, yaani ni nini? Ni kusema huyu ndie anaefaa kuliko wengine wote. Tunakupongeza na tunakutakia kila la kheri, *Allahuma Zidna I'liman Waruzuqna Fahma*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Waziri umeshapitia Wizara tatu sasa hivi, ndani ya Wizara hizo tatu hakuna Wizara hata moja ambayo imekushinda na hapa ndiyo umefunga kazi, tunakupongeza na tunakutakia kila la heri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtendaji mzuri, ni mtu msikivu ni mwanamama ambaye hajitanuitanui, ameshuka kuliko kawaida yake, hongera sana Mheshimiwa, tunampongeza pia vilevile Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na Watendaji wake wote. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kila aliyechangia amezungumzia masuala yanayohusu mnyama tembo. Mnyama tembo ni mnyama mzuri sana lakini mnyama tembo huyu, tembo ana tatizo. Tembo tunampenda huyu, tunampenda sana tembo kwa sababu tembo anatuletea kama nilivyosema pale mwanzo, pesa za kigeni. Lakini tembo huyu pamoja na uzuri wake huo mkubwa alionao, tembo huyo ana shida, tembo huyu siyo rafiki huyu kwa watu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa tumeambiwa ya kwamba tembo wameongezeka kwa kiasi kikubwa sana, tunaipongeza Serikali kwa kudhibiti majangili hatimaye kusababisha tembo kuongezeka kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kinachotokea tembo hawa wanaleta madhara kwa binadamu, ninachoomba kwa Wizara hii, yaani hapa watu wamnapiga makofi kweli kweli wakimaanisha ya kuwa lazima Serikali iweke mkakati madhubuti juu ya wanyama tembo. Mkakati madhubuti usipowekwa maana yake ni nini? tutabaki na tembo watu wataondoka, watu watakufa. Tutabaki na tembo peke yake, kweli kabisa hili siyo sawa sawa ni lazima tuliangalie kwa mapana yake makubwa. Inaonekana kama kichekesho lakini ni hatari kwa Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukiachana na Wanyama tembo ambao wanaua, mimi mfano hai Jimboni kwangu Mheshimiwa Waziri sasa hivi tembo wamejaa, sasa hivi wanasaidiana na wanyama wanaoitwa fisi, wanaua watu. Nataka nikueleze tukio la watu wanne waliojeruhiwa na fisi Tarehe 10 Mwezi wa Tano Mwaka 2023 ule usiku, mmoja ameuawa na fisi na wengine watatu wamejeruhiwa wapo hospitali ya Mkoa ya Sokoine, nilikwambia Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ni shuhuda juu ya jambo hili. Sasa si unaona wamewaambia tembo ngojea tupumzike tuwaache fisi, hii ni hatari.. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya tembo na kusema muweke mkakati madhubuti. Kumbe nimeambiwa nisitumie tembo, nitumie neno ndovu, ahsante, kule

kwetu wanaitwa tembo. Ahsante sana haya nitatumia neno ndovu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la linalohusiana na asali ya Tabora imeshika nafasi ya pili katika Bara la Afrika. Kwa kuwa, asali yetu imeshika nafasi ya pili katika Bara la Afrika, mkakati gani uliopo ili kuhakikisha asali yetu inashika nambari moja ndani ya Bara letu la Afrika, hili ni muhimu sana kwa sababu asali ni dawa na asali ni kila kitu lazima tutengeneze mkakati madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna suala la dinasoria au yule mnyama anayeitwa mjusi. Dinasoria anapatikana huku Kusini lakini anapatikana kwenye Jimbo la Mchinga. Kwa kuwa dinasoria huyu anapatijkana kwenye Jimbo la Mchinga, Wizara ya Maliasili na Utalii tunaipongeza sana, pale Kitomanga wameshaweka kituo cha kupatia habari na Lindi Mjini pale ukifika unamkuta huyo dinasoria mrefu kuliko wengine maana yake tunatangaza utalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *LNG*. *LNG* italeta mabilioni ya pesa na watakaoajiriwa kutokana na *LNG* au watakaopata fursa ni zaidi ya watu 15,000,000. Tunajipangaje kuhusu fukwe zetu, ikiwemo fukwe za Mchinga hili ni lazima tuweke mkakati madhubuti. Tukiweka mkakati madhubuti wale watalii watakwenda kule.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100 tujipange kwa ajili ya *LNG* ili watalii wasiende huko wabaki kwenye fukwe zetu zilizopo kusini na Jimbo la Mchinga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa John Pallangyo ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya ya kutangaza vivutio vyetu na tumeanza kuona faida kubwa ya *Royal Tour* ambayo imeanza kuleta watalii wengi na kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri sasa hivi hii ni Wizara ya tatu na kila ulikoenda kwa kweli uliendа na matumaini na uliacha matumaini na ninaamini Wizara hii ambayo imeleta makovu mengi, imeleta huzuni na masikitiko kwa watanzania sasa naamini imepata mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, tumeongelea suala la tembo, kwa kweli tembo tunawapenda na wanadamu tunawapenda, jambo hili Mheshimiwa Waziri lazima ujipange. Watu wamejeruhiwa, watu wameteseka muda mrefu sasa ni wakati wako kuleta majibu ambayo yanaenda kuponya haya majeraha ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapouliza hapa Bungeni wanakwambia tembo hawa ni njia yao walipita miaka 200, lakini jambo ambalo linasikitisha maeneo hayo ambayo yamevamiwa na tembo ni maeneo ambayo yametengwa kwenye vijiji kwa mujibu wa sheria. Wakati wanatenga haya maeneo Serikali haikujua hapa ni njia ya tembo? Kwa nini watenge haya maeneo wawapeleke wananchi, waende kuendeleza maeneo hayo, wana mashamba wamejenga nyumba. Kwa mfano, kule kwangu Kyerwa katika Kata ya Businde, Kata ya Bugara Kata ya Kibare wanaendelea maeneo mengi. Hawa tembo walikuja kama 20 sasa hivi wameshazidi 100, hivi Mheshimiwa Waziri kama mmeshindwa kuwafukuza hata mmeshindwa uzazi wa mpango? Leteni uzazi wa mpango wa hawa tembo, tembo hawa wanaua wananchi, wanatesa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi kwenye kitongoji kimoja wameondoka wananchi zaidi ya 200, walikuwa na mashamba walikuwa wanafanya kazi zao vizuri. Nyumba zao zote

zimeteketezwa halafu mnakuja mnasema kuna kifuta jasho. Mheshimiwa Waziri tunaomba hili uliangalie.

Mheshimiwa Spika, kifuta jasho mtu ana shamba zaidi ya heka 10, zaidi ya heka 20 ana migomba amejenga nyumba zaidi ya Shilingi milioni 20 unampa milioni moja, unampa 100,000 moja hiyo hela inamsaidia nini? Tumewafanya Watanzania kuwa maskini kwa sababu ya hawa tembo. Kwa hiyo ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri unapokuja hapa kumalizia bajeti hii unapojumuisha hapa utueleze ni mikakati ipi umekuja nayo ili kuhakikisha mnadhibiti hawa tembo, vinginevyo hali ni mbaya na wanazaliana sijui namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri niongelee jambo jingine kuhusu suala la mipaka ya hifadhi pamoja na wananchi. Tulisikia Serikali imeunda timu ya Mawaziri Nane, Mheshimiwa Waziri kama unataka kufanya hili jambo kwa ufanisi ile taarifa ya Mawaziri Nane usiende nayo. Jiridhishe wewe mwenyewe kwa sababu haiwezekani hawa Mawaziri Nane wanaenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, shida iko Kyerwa nyinyi mnaishia pale Bukoba Mjini. Haiwezekani! Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri jiridhishe na taarifa hii, lakini maeneo mengine walikuwa wanafika kwa vitisho kuwaambia hawa hapa hampati kitu lazima muondoke.

Mheshimiwa Spika, hawa wananchi mnaowafukuza kama siyo Watanzania hawa, hawa ndiyo ninaoamini wanaweza wakawa wahifadhi wazuri wa kulinda vivutio vyetu na kulinda maeneo yetu. Lakini mnavyowafukuza namna hii mnajenga chuki na uadui mkubwa. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili uliangalie na ulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri nilikuwa najaribu kuangalia bajeti za nchi nyingine hasa kwenye mambo ya utalii. Mungu ametujalia vivutio vingi katika Taifa letu, lakini hivi vivutio tumevitangaza namna gani? Tunaona ile *Royal Tour* kitu ilichokifanya lakini tuombe na sisi kama Serikali lazima tujipange kuhakikisha tunatenga bajeti kubwa ya kutosha. Ukiangalia niwasomee kidogo Waheshimiwa Wabunge muone nchi yetu ilivyo na bajeti za nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukienda Rwanda, Rwanda naona kama Mkoa wa Kagera. Rwanda bajeti yao ya utalii ni Dola Milioni 4.5. Ukienda Afrika Kusini Dola Mil. 75. Ukienda Kenya majirani zetu Dola Mil. 3.5. Ukienda Tanzania kwetu Dola 1.5, jamani hata Rwanda? Hata Rwanda kwa kweli, hii hapana! Kwa hiyo, niombe sana Serikali ijipange kuja na bajeti kubwa tutangaze hivi vivutio ambavyo Mwenyezi Mungu ametujalia ili Tanzania tupate pesa. Tunaanza kukimbizana na wafanyabiashara, tunakimbizana na watu wengine wakati tunavvyo vitega uchumi pesa iko nyingi. Tuitumie fursa hii ambayo Mungu ametujalia ili tuone tutakavyopata pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sijaelewa hapo umetaja Kagera halafu ukataja Rwanda ili nielewe vizuri mchango wako.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, yaani nilichokuwa nalinganisha ukiiangalia nchi ya Rwanda ni kama ina lingana lingana na Mkoa wa Kagera lakini wanatuzidi mara nne.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tunapowapongeza Waziri na Naibu Waziri kweli wanafanya kazi sana siyo kwamba tunawatania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naongea suala hilo hilo la tembo. Jimboni kwangu wananchi hawana raha, wananchi hawana furaha, matatizo ya tembo kwenye Jimbo la Same Mashariki naomba tafadhali haya makabrasha mawili haya yaje mbele yako apelekewe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu gani? Kama miaka mitatu hivi madhara yaliyofika mashambani kwa wananchi wangu, mpunga, mahindi, miaka mitatu, takribani miaka mitatu

hata hicho mnachokiita kifuta jasho wananchi hawajapewa, sasa nianze upande wa vifo.

Mheshimiwa Spika, kabrasha hili linazungumzia vifo. Naanzia Muheza, Kenneth Edward Mazengo - Muheza, huyu alijeruhiwa tangu tarehe 24 Julai, 2022, wala Serikali haijamuangalia. Rayson Eminiel Mjema wa Kijiji cha Muheza alijeruhiwa na tembo tangu tarehe 26 Januari 2022, wala Serikali hamjampa hata senti tano. Ally Mhina Mbogo Makokane aliuawa tarehe 9 Julai, 2022 na tembo lakini Mheshimiwa Waziri mambo makubwa kama haya Serikali hamjawaona wananchi, na Zuhura Mapande wa Kijiji cha Muheza aliuawa tangu tarehe 17 Agosti, 2022 aliuawa na tembo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwepo mwenyewe Jimboni niliona aibu kwenda kumuona yule mama alivyochanwachanwa na tembo lakini Serikali hamjaona watu kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili kabrasha lote nililoshika mkononi hapa ni mazao ya wananchi wa Jimbo la Same Mashariki. Mimi ninahisi Mheshimiwa Waziri nisikilize vizuri, hawa tembo wangekuwa kule ndani ya *National Parks* wana maji ya kutosha, wasingekuja kwa wananchi huku, wangekuwa wana chakula cha kutosha wasingezunguka na kula mpaka wali uliopikwa na wananchi, angalieni vizuri ndani ya *National Parks* kuna hali gani?

Mheshimiwa Spika, naomba nikwambie. Naanza upande wa uharibifu wa mazao ya wananchi. Twende Kata ya Maore Kijiji cha Maore tembo wameharibu ekari 74.5 hapa ni kaya 67 zote wananchi hawakuvuna kitu, njaa. Kata hiyo hiyo ya Maore nenda Kijiji cha Mpirani ekari 21 mpunga na mahindi hapa ni kaya 21 wananchi hawakuvuna kitu. Kata hiyo hiyo ya Maore Kijiji cha Mheza kaya 367 ekari takribani 512, ekari zote hizi wananchi hawakuvuna kitu. Kijiji cha Kadando takribani kaya 54 ekeri 66, wananchi hawakuvuna kitu, tembo.

Mheshimiwa Spika, twende Kata ya Kalemawe, Kijiji cha Kalemawe kaya tisa na ekari tisa za mahindi wananchi hawakuvuna kitu. Twende Kijiji cha Makokane kaya 132, ekari 143 za mpunga na mahindi wananchi hawakuvuna hata hindi moja. Kijiji cha Karamba kaya 30, ekeri 31 mahindi, maharage, mboga

za majani hawakuvuna kitu wananchi. Kata ya Nungu Kijiji cha Misufini kaya 95 ekari 145 wananchi hawakuvuna kitu. Kijiji cha Nungu kaya 33 ekari takribani 35 hawakuvuna kitu.

Mheshimiwa Spika, nikianza Kijiji kwa Kijiji kwangu ni taabu. Jimbo la Same Mashariki ni shida, nakuomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja miaka miwili iliyopita, kote huku nilimpeleka hakuna kitu kimefanyika mpaka leo. Juzi nasikia Diwani anaiambia Mheshimiwa Waziri ametuma watu wake wamekuja kuona mahali pa kujenga Kituo cha Askari mimi wala hilo silipokei, wamekwenda kuona je, wamejenga? Huko ni kuona wananchi wangu wanakufa kila siku, wananchi wangu hawana mazao, hawana chakula, wana njaa, tembo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono hoja, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu anawafanyia nini wananchi wangu kuhusu tatizo la tembo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye bajeti hii ya Maliasili na Utalii, Wizara ambayo kwa kweli ni nyeti, ambayo inachangia *percent* 25 ya fedha zote za kigeni pia *percent* 17.5 Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, Naibu wake, Mheshimiwa Mary Masanja pia na Naibu Katibu Mkuu na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya Wizarani pamoja na watumishi wote ambao kwa kweli wote wanachangia katika kazi nzuri ambazo zinafanywa na Wizara hii, ikiwa ni pamoja na Wakuu wa Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kutembea wakati wa ziara za Kamati kukagua miradi, tulikwenda Ngorongoro, tulikwenda *TANAPA* kule Mkomazi, tulikwenda *TANAPA* Rubondo. Kwa kweli kazi zinazofanyika ni za uhakika. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo mnafanya, wewe tunakufahamu, ni mtu mwema pia ni mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye Hifadhi ya Arusha. Hii hifadhi ilianzishwa mwaka 1960, mwaka mmoja kabla hatujapata Uhuru wetu. Nimekuwa nashangaa kwamba ni kwa nini hii hifadhi ilitwa Arusha mpaka leo inaitwa Arusha, lakini kumbe hifadhi yenyewe ni sehemu ya Msitu wa Mlima Meru. Watalii wengi wanakuja wanapanda ule Mlima, nikaona heri leo nishauri Mheshimiwa Waziri ile hifadhi badala ya kuiita Arusha *National Park,* kuanzia leo ibadilike uiite Hifadhi ya Taifa ya *Mount Meru (Mount Meru National Park)*. Nakuomba ikiwezekana leo wakati wa kuhitimisha hapa utangaze kwa Watanzania kwamba sasa ile hifadhi itakuwa ni Hifadhi ya Taifa ya Mlima Meru.

Mheshimiwa Spika, kwenye ile hifadhi kuna mgogoro. Niliwahi kufika kwenye ofisi ya Waziri nikamwambia kwamba tupange angalau tende kule Jimboni aende azungumze na wananchi, bahati mbaya ile timu ya Mawaziri Nane ambayo ilizunguka nchi nzima haikuweza kufika pale hifadhini iweze kuzungumza na wananchi. Kwa hiyo nakuomba ile agenda ya kwenda Momela ukazungumze na wananchi wa kile kitongiji usiiache. Upange twende ukazungumze na wale wananchi kwa sababu ule mgogoro ulianza siku nyingi na ulitokana na mashamba mawili, Na. 40 na Na. 41 kutwaliwa na Serikali ambayo mashamba haya yalikuwa yanamilikiwa na wawekezaji, mwekezaji wa kwanza akafa, akachukua mwingine baadaye yakamshinda akaya-*abandon* akayaacha pale.

Mheshimiwa Spika, wakati ulipokuja mpango wa vijiji na vijiji vya ujamaa, wananchi waambiwa wajipange kule wajikimu na kufanya kazi za kilimo na ufugaji. Mwaka 2017 Serikali iliwatoa kwa nguvu na baada ya pale hakuna kilichofanyika, wananchi wale wameachwa wanateseka wametupwa kwenye lindi la umaskini, niseme ukweli kwamba Serikali ina haki ya kuchukua ardhi yake kwa sababu ndiyo yenye mamlaka, lakini inavyotoa wananchi

bila kujua wanawapeleka wapi, kidogo hiyo haiko sawa. Naamini kabisa kwamba Serikali ina nia njema, haiko hapa ku-*displace* wananchi wake lakini inapaswa ifanye *relocation*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuamini wewe ni mtu mwema hili tatizo nina uhakika utalimaliza.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani nilishawahi kuzungumza tena hapa kuhusu *cable cars.* Wakati unabadilisha jina la ile hifadhi uweke pia na *cable car* pale kwenye lango la kuingia hifadhini ambayo itakwenda mpaka Miliakamba. Nakuhakikishia ukiweka hiyo *cable car* idadi ya watalii wa ndani itaongezeka mara dufu. Nakuomba uliweke kwenye mpango ili tuweke huo mpango wa *cable car.*

Mheshimiwa Spika, naona unataka kunisemesha, basi niseme tu kwamba nakushukuru sana kwa muda huu mfupi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, angalau ni nafasi ndogo lakini naweza nikaongea machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri kwa hotuba nzuri inayohusiana na mambo ambayo yapo mbele yetu. Pili ninapenda niongelee sekta ya misitu. Sekta ya utalii kwa kuanzia tunaona kwamba ina mchango mkubwa wa asilimia karibu 17 kwenye Pato la Taifa. Sekta hii ya misitu inaonekana kama ni sekta ambayo mchango wake ni mdogo sana, lakini mimi nataka leo niseme bahati mbaya muda ni mfupi, nitaongea mbele ya safari. Niseme kwamba sekta ya misitu ina uwezo mkubwa wa kuchangia kwenye uchumi wa Taifa tukiweka mikakati mizuri. *In fact,* sekta ya utalii ni *very fragile,* ni tete, ikitokea shida kidogo tu inatetereka. Imekuja *COVID* hapa ikaporomoka, ikitokea vita inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya misitu ndiyo sekta ambayo Wizara inatakiwa iiangalie kwa makini sana ili iwe sekta ambayo itaitegemea, ni sekta himilivu, ni sekta jumuishi, ina watu wengi, inatoa ajira kwa watu wengi, kwa hiyo wawe na mikakati mikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nami nataka kusema kuwa kuna mambo matatu au manne ambayo wakiyafanya sekta hii katika kipindi cha miaka mitatu kwenda minne tutaona mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tubadilishe mtazamo na fikra. Hivi ni nani aliyesema kwamba samani, milango fremu, lazima ziwe za mninga, mvule au mpodo, nani alisema? Kuna uwezekano mkubwa tukawa na samani nzuri sana zinazotumia mbao laini.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema wengi tumetembea hapa, tumekwenda sehemu nyingi, tumekwenda kwenye mahoteli, nitajie hoteli moja tu ambayo utakuta mlango wa mninga, hakuna! Sekta hii tupende kusema, lazima tuanzie kwanza kwenye mchakato mzima wa Serikali wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, tuweke *permissive provision* inayosema kama *soft wood* ina-*meet* kiwango na yenyewe iwe *included* kama sehemu ya mambo ambayo yanaweza yakatumika. Serikali ita-*create demand* na iki-*create demand* itaendelea kukua na kukua na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala zima la *technology* kwenye sekta hii. Tukiangalia, sisi tukivuna mti wa mbao kutoka kwenye gogo tunatumia asilimia 30 tu, iliyobaki yote inapotea. Ukiangalia tuna viwanda vingi vya kuchakata, katika viwanda asilimia 70 vyote ni mbao tupu.

Mheshimiwa Spika, kule Njombe kwa mwaka kuna *semi-trailers* karibu 40,000 zinazoondoka. Kwa siku kuna *semi-trailers* karibu 39, ni mbao tu. Tufike mahali sasa kama nchi tufanye maamuzi ya kuongeza thamani kwenye mbao, kwenye mnyororo mzima wa mazao ya misitu, tutafanyaje, tutafanya kwa kuingiza kitu tunakiita *EWP* (uhandisi katika mazao ya mbao).

Mheshimiwa Spika, nipende kusema tuna *products* nyingi sana, siyo mbao tu, tuna *veneers*, tuna *plywood*, tuna *MDF*, tuna boriti zile ambazo zinakuwa *treated*, zote hizi ni *products* ambazo tunaweza tukileta *technology* nzuri kwenye soko la mbao au kwenye *industry* ya mbao tutaweza kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kusema *technology* ambayo tunaiongelea hapa ni ile ya *second level,* tutoe vivutio, kwanza kabisa kama Mbunge mmoja alivyosema hapa, tuangalie uwezekano wa ku-*zero rate* mashine zote ambazo zinakuja kwenye sekta ya mbao, hakuna hasara kwa Serikali, *medium term, long term,* Serikali itapata fedha zaidi, tuta-*create employment* zaidi katika sekta hii ya mbao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tunaweza kufanya ni kuendelea kuiangalia hii sekta kuiondolea vikwazo na kuangalia ada na tozo mbalimbali ambazo zipo kwenye sekta. Bado kuna tozo nyingi sana kwenye hii sekta, *GN* Na. 59 tuiangalie kwa makini. Lakini kule Njombe kwa mfano…

**SPIKA:** Malizia sentensi Mheshimiwa.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, upande wa vibali watu wetu wanaosafirisha mbao wanapata taabu sana humu njiani, unatakiwa u-*scan document* unapoondoka, upite una-*scan document* mpaka unafika, vituo zaidi ya 15 kwenye *destination*. Kwa nini tusi-*scan* pale mwanzo ili biashara iendelee waka-*scan* mwisho kwenye *destination*? Kwa hiyo kwenye upande wa vibali tuliangalie kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ukisafirisha mbao unatakiwa upate kibali unapotoka, lakini ukapate kibali unapouza. Kwa nini kuwe na vibali viwili? Na tunapoteza muda, tunapoteza mapato, tunapoteza ajira. Niombe sana tuiangalie sekta hii kwa makini sana na tuiongezee fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami kwa utamaduni, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara yetu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, pia nakuponggeza na kukuombea kwa Mwenyezi Mungu wewe binafsi ambaye unaomba nafasi ya Urais wa *IPU,* nakuombea kwa Mwenyezi Mungu akusimamie na utashinda nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Namtumbo ni wahifadhi, na nimekuwa nikisema ni wahifadhi na wakulima. Kwa miaka yote tumekuwa ni watu wa aina hiyo. Ni sisi wenyewe pia tulifika mahali tuliamua kwamba tuanzishe maeneo ya uhifadhi kwenye maeneo yetu ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, tulianzisha *Wildlife Management Areas (WMAs)* ambazo jumuiya hizi tulianzisha kwa kusini mwa Selous wakati ule mwaka 2007, ilikuwa inaitwa Mbalang'andu Kaskazini, na Kusini tuna Kisengue na Kimbande. Jumuiya hizi tulikubaliana hapo awali kwamba baada ya miaka 10 tutakuja kuwa na mapitio kwa ajili ya matumizi ya ardhi kwa sababu ile ilikuwa ni ardhi ya kijiji tuliiweka kwa ajili ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, miaka 10 ilishapita mwaka 2017 na wanavijiji wamekuwa wakiomba kufanyika mapitio ya ardhi kwa sababu wanahitaji ile ardhi kiasi, siyo yote kwa ajili ya kilimo. Lakini kumekuwa na danadana wasifanye yale mapitio na kuna sehemu wamefanya mapitio lakini majawabu hayaji. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali lazima tuishauri kwamba twendeni tukawaelewe wananchi mahitaji yao, ardhi yao ile waliitoa kwenye uhifadhi sasa wanahitaji kiasi kwa ajili ya kilimo. Lakini sasa hivi wanaonekana wananchi wale wa Namtumbo katika vijiji vile vyenye uhifadhi kana kwamba wao ndiyo wanataka kuvamia maeneo ya uhifadhi, kwa hiyo nguvu kubwa sana inatumika ili kuhakikisha kwamba wasiingie.

Mheshimiwa Spika, kama mtarudi mkazungumza nao kama mlivyowashawishi mwanzo, kuwapa elimu mwanzo na kukubali kufanya uhifadhi, tunaomba sana mrudi tena kuzungumza nao ili kuona ni kiasi gani na kufanya mapitio wapewe wananchi wale waweze kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tufahamu Maafisa wa Hifadhi pia, tufahamu sisi sote ni binadamu, na binadamu hasa wa vijijini kule wanategemea mapato yao ni kilimo, ndicho kinachofanya wanakidhi maisha yao kuishi katika dunia yetu hii. Kwa hiyo, lazima tufikirie hilo pia, pamoja na uhifadhi. Kwa hiyo, ushauri wangu ulikuwa huo, naomba sana tunapokwenda kule tuwasikilize wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu utalii. Balozi zetu na *consuls* kuu zetu zinafanya kazi kubwa ya kutangaza utalii, lakini kwenye bajeti zao Balozi na *consuls* kuu hakuna vifungu maalum vya kutangaza utalii, wanatumia *OC* zao. Siyo vibaya, lakini kutumia *OC* zao zile za kawaida inawawia ugumu sana kufikia malengo ya kuutangaza utalii wa nchi yetu. Kuna Ubalozi una nchi saba, lakini unahitaji usafiri uende ukatangaze maeneo hayo, hawana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna uhitaji wa kutangaza, fedha zinakuwa hazitoshi. Kwa hiyo, tunashauri Wizara mtenge fedha kwa ajili ya balozi zetu kuchapisha matangazo, majarida kwa lugha za kule, lakini kufanya matagazo kwenye televisheni pia. Ni muhimu sana kwenye hili kuzisaidia Balozi zetu. Hakuna fedha mahsusi zinazotumika kwa ajili ya utalii. Mimi naamini hili litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuutangaza utalii wetu. Nilipata bahati alikuja Spika wa India, Lok Sabha Om Birla. Uliniteua niwe mmoja wa watakaompokea na kuwa naye, lakini ulinipa kazi ya ziada kwenda Serengeti. Tulipokwenda Serengeti kule walihitaji kuona wale *Big Five,* waliwaona kweli, walibahatika wote, faru, *a pride of 18 Alliance* waliwaona kwa mara moja. Na Spika yule alishangaa kabisa, alisema katika maisha yake mpaka utu uzima hajawahi kuona simba zaidi ya mmoja, alikuwa ameona simba wale 18 *live*.

Mheshimiwa Spika, pia waliona nyumbu wengi, toka asubuhi wanaona nyumbu mpaka wakati wanapovuka. Wakasema walikuwa wanajua hawa nyumbu wako upande wa nchi ya pili kule, wenzetu kule wanatangaza sana, wao wanafahamu upande ule wa pili, lakini kumbe eneo kubwa la nyumbu hawa liko huku Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wahindi nao hawakuwa wanafahamu kama Serengeti ndiyo ina wanayama wengi na wale wanyama nyumbu wanakuwa wengi upande huu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tukazane sana kwenye eneo hili na hili ni pekee kwa kuwezesha Balozi zetu wazitangaze vizuri kule. Kwa hiyo ile timu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaj)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Maliazia sentensi.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ile timu ya Spika wa Lok Sabha ndiyo imekwenda kutusaidia kututangazia kule. Kwa hiyo, tuongeze nguvu ya fedha kwenye Balozi zetu kutangaza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nije kwenye suala la pongezi. Pongezi nyingi sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi aliyoionesha na dhamira ya dhati kabisa ya kuutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara. Lakini kwa niaba ya wananchi wa Buchosa naomba nitoe shukrani sana kwa Wizara kwa kutujengea vizimba viwili kuzuia wananchi wetu wasiliwe na mamba.

Mheshimiwa Spika, hapa ndani leo imekuwa ni suala la ndovu kila kona, lakini napenda niwaongezee suala la mamba. Kule ninapotoka mimi wananchi, hasa akina mama, wanaliwa sana na mamba, na kimekuwa kilio changu sana kwenye Wizara. Ombi langu kwa Wizara ituongezee vizimba vingine vya kuzuia watu wasiliwe na mamba hasa maeneo ya kuchota maji na maeneo ambayo watu wetu wengi wanakwenda kuoga nyakati za jioni. Hayo ndiyo mambo ambayo wananchi wa Buchosa wamenituma.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni maeneo ya hifadhi. Tunacho Kisiwa cha Maisome ambacho wananchi walikuwepo baadaye tukaja kupima eneo tukasema hii ni hifadhi, idadi ya watu imeongezeka, wananchi wanaomba kukatiwa kipande kidogo kwenye eneo la hifadhi ili waweze kupata maeneo ya kufuga mifugo yao na hata maeneo ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo kwenye Kisiwa cha Kome, na kwenyewe kuna tatizo hilo. Wananchi wanalalamika eneo la hifadhi lipo, idadi ya watu imeongezeka lakini hawana sehemu ya kujenga na pia kulisha mifugo yao. Kwa hiyo kila siku ng'ombe wanakamatwa wanapigwa faini 100,000 kwa ng'ombe, kwa hiyo naiomba Serikali hii sikivu, Mheshimiwa Waziri tulishazungumza, nikuombe sana suala hili uzingatie na ninakukaribisha Buchosa uje ujionee mwenyewe, umeniahidi kuja wananchi wanasikia, nakukaribisha sana Buchosa uje ujionee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Wizara hii ni suala la biashara kabisa asilimia 100. Uhifadhi, lakini tunawezaje kupata fedha kutoka kwenye uhifadhi, tunawezaje kugeuza Hifadhi zetu za Serengeti, Ngorongoro, Mlima Kilimanjaro, wanyama kama tembo, simba waweze kuwa fedha. Hilo ndilo jambo ninalotamani kuliona. Nataka kuona fedha katika nchi hii ili ziweze kusaidia juhudi za maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti kidogo na nimegundua kabisa ya kwamba kila unapo-*double* juhudi za kutangaza biashara ya utalii mapato yanaongezeka. Sasa, nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri nikakutana na maandishi yanasema kama ifuatavyo: -

"Bila kutangaza sana bado tumeweza kufikia kiasi cha pato la Taifa asilimia 21 kutokana na utalii." Bila kutangaza sana, bila *promotion* hii ni bahati kubwa sana, haitokei mahali popote duniani, yaani kwenye ulimwengu huu tulio nao wa leo unasema bila kutangaza sana tumefanikiwa. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba kama Waziri angetangaza sana, mapato yangeweza kuongezeka na hicho ndio kimenisimamisha hapa kuongea leo.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba siridhishwi kabisa na *investment* iliyofanyika kwenye suala zima la kutangaza utalii wetu. Tanzania katika dunia ni Nchi ya pili kwa vivutio vya asili ikiongozwa na Brazil. Tanzania ni Nchi ya kwanza Afrika kwa vivutio vya kiasili, nchi ya kwanza lakini angalia mapato yake. Mapato yake ni kidogo sana. Kama Taifa tunaweza kusema bado *GDP ratio* inaturuhusu kukopa. Tuna asilimia 40 tu, wenzetu wana asilimia 77, lakini je, tutegemee mikopo kila mara na utajiri huu tulionao? Ningetamani siku moja nchi yangu isikope, iweze kutumia zawadi ambazo Mungu ametupa kuendesha nchi yetu na inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikusomee *data* moja hapa, *data* moja rahisi tu. Baraza la Utalii Duniani *(WTTC)* mwaka 2019 lilisema maneno yafuatayo, Idara ya Utalii Tanzania iliingiza dola bilioni 6.7 mwaka 2019, bila kutangaza tunaingiza fedha hizi tuki-*double* itakuwa bilioni 13. Fedha hizo ukizijumlisha kwa ujumla wake ni trilioni 16. Shilingi trilioni 16 hiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, namalizia. Shilingi trilioni 16 hiyo *deficit* kwenye bajeti yetu sisi ni shilingi trilioni 10 ingeweza kuziba *debt*…tusikope. Ombi langu juhudi za

kutangaza ziongezeke, tusiridhike na mambo ya bila kutangaza tumefanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuata Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Dennis Londo ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi. Niungane na wenzangu kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wamefanya katika kuifufua Sekta hii ya Utalii ambayo ilikuwa imeathirika kwa kiwango kikubwa sana kutokana na *Covid-19*. Sote tunajua kwamba mwaka 2019/2020 watalii walishuka mpaka chini ya 600,000 lakini jitihada kubwa zimefanyika ambazo zimepelekea idadi ya watalii imeongezeka mpaka kufikia 1,500,000 mwaka 2021 na taarifa ya sasa hivi inaonesha wamefika milioni 3.8. Ni hatua kubwa Serikali wamefanya wakiongozwa na Rais wetu mpendwa mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kweli hongera sana kwa kazi hiyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtalii ni nani? Mtalii ni mtu yeyote anayeweza kusafiri kutoka sehemu anakoishi akaenda sehemu nyingine kwa lengo la kupata burudani, kwa lengo la kwenda kujifunza, kwa malengo mengine. Unaenda sehemu nyingine kwenda kula Maisha, huo ndio utalii. Kwa hiyo tunahitaji tuwe na mikakati ya kuwawezesha watalii waka-*enjoy,* wakale maisha. Tunahitaji utalii wa wanyamapori, jitihadi lazima zifanyike idadi ya watalii wa wanyamapori iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii wa milima pia uongezeke, nchi yetu ina milima mingi. Utalii wa miamba kama vile *Olduvai Gorge* lazima watalii waongezeke, tunayo miamba mingi nchi hii. Utalii wa mikutano mbalimbali inayofanyika katika nchi hii, lazima tuwekeze ili tuwe na mikutano ya aina mbalimbali kuvutia watalii. Tunahitaji utalii wa misitu, utalii wa matibabu, hospitali mbalimbali ambazo sasa hivi tunaboresha huduma tutapata watalii kutoka nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji vilevile watalii wa vyuo kuja kusoma na kuja kujifunza. Tunahitaji utalii wa fukwe na utalii wa mambo mengine mengi. Wote huu ni utalii, lakini maana ya utalii tunaupima kwa kuangalia idadi ya watu waliokuja wa ndani na wale wa kutoka nje, lakini na kiasi cha fedha killichoingia katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kupata fedha za kutosha tunahitaji kuwekeza, lazima tuwekeze vya kutosha. Tuwekeze kwenye kujenga hoteli, kujenga kumbi za kitalii, kumbi zitakazovutia watu mbalimbali kuja kufanya mikutano hapa. Tunahitaji kuwekeza kwenye miundombinu, tunahitaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali kuvutia watalii kutoka nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ili tufanikiwe tunahitaji kuboresha huduma. Sasa hivi huduma zetu katika meneo mengi ya utalii kwenye mahoteli bado hazijawa vizuri. Ni wajibu wa Wizara kuhakikisha inaboresha haya ili tuvutie watalii walio wengi. Tumeona kulikuwa na programu ile ya kuboresha utalii kusini ili kuhakikisha nchi yetu inapata katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na programu ya *REGROW* ambayo ilikuwa na dola za Marekani 150. Toka wakati ule mpaka leo ile programu bado haijafanikiwa. Kule kusini hatujatangaza ipasavyo vivutio na maliasili tulizonazo. Kule Mbozi tuna kimondo kizuri, hapo Iringa tuna Ruaha, tuna Mikumi, tuna Rungwe tuna milima, tuna wanyama, tuna kila aina ya vivutio. Lazima tuwekeze ili tuhakikishe kwa kweli na huko zinapatikana fedha zitakazotoa mchango mkubwa katika kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Ruaha kule, kuna maeneo mengine Rungwe kule kuna mlima na kuna kamto fulani kamuhimu sana, kana historia nzuri sana, kuna utamaduni. Kwa utajiri mkubwa huu tulionao nchi yetu tunahitaji kuwekeza. Tukiwekeza sekta zikajipanga vizuri nchi hii tutapiga hatua kubwa na tutapata maendeleo makubwa sana. Kwa hiyo, kazi ya Wizara ni kuhakikisha ina-*coordinate* sekta zote hizi tuwekeze. Tufanye kazi kwa pamoja ili nchi iende mbele na sisi tuone manufaa ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuwekeza zaidi, angalia *royal tour*. Tumetangaza kwa *royal tour* imeleta *impact,* je, tukitangaza? Sasa Wizara wajiongeze basi, waende sasa wakatangaze na maeneo mengine. *Royal tour* ni moja, je, maeneo mengine tumeyatangazaje? Mheshimiwa Rais ametuonesha mfano, sasa na wao wachukue pale alipoishia twende mbele tutangaze nchi hii tufanikiwe. Nina imani tutafanikiwa sana na tutafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tunaomba Wakala wa Misitu ibadilishwe iwe sasa ni Mamlaka ya Kusimamia Misitu yote Nchini. Misitu ni uhai, misitu ni maisha, misitu ni maisha yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni hii ya leo. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Naomba nianze na pongezi kubwa, niungane na wachangiaji wote waliompongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutangaza utalii kwa kupitia *Royal Tour*. Pia niungane na wote ambao wamekuwa wakikuombea wewe kugombea Urais katika Mabunge na nina imani kabisa kwamba hiyo nafasi utakayoigombea tunakuja kuweka historia katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Mchengerwa ambaye kwa kweli kwa kipindi tu kifupi ameweza kuonesha kwamba Wizara hii inaanza kubadilika na inaleta maendeleo mazuri. Pia nimpongeze Naibu

Waziri, wifi yangu ambaye pia amefanya kazi nzuri sana katika Wizara hii, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu Mradi wa *REGROW;* kusema kweli kabisa Mradi *REGROW* kama walivyosema wenzetu wote waliochangia asubuhi na sasa hivi, ni mradi ambao tulikuwa tunategemea sasa utakuza utalii katika Mikoa yote ya Kusini lakini tunaona bado mradi huu unasuasua. Toka ulipoanza mwaka 2019 sasa hivi tuna miaka mitano, lakini bado tunaona hakuna chochote kinachowekezwa katika Mkoa wa Iringa, maana yake tuliambiwa kungejengwa kituo kikubwa cha maonesho ya utalii wa kimataifa katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, pia walisema wangejenga ofisi ya kanda, lakini tunaona mpaka leo hii bado. Je, ni lini sasa vitu hivi vitajengwa, lakini pia nataka kujua je, wananchi wameandaliwa kiasi gani kuupokea huu mradi, kwa sababu tunategemea huu mradi sasa watajiajiri kwa kutumia utalii kama ilivyo kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea pesa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege. Tunategemea huu uwanja wa ndege pia utahamasisha sana utalii katika Mkoa wetu wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini, lakini sasa tulikuwa tunaomba pamoja na huu ujenzi bado wanatakiwa wajenge ile barabara inayokwenda katika mbuga za Wanyama, *Ruaha National Park* kwa sababu kukiwepo tu na huu uwanja bila kujengwa ile barabara bado tutakuwa hatujafanya chochote.

Mheshimiwa Spika, tunategemea hata utalii wa ndani utaongezeka, lakini vilevile tunaomba pia katika lile lango pale Idodi kijengwe kituo kikubwa cha polisi kwa ajili ya usalama wa watalii kwa sababu tumeona kuna kontena tu ambapo sio vizuri. Pia wangesaidia hata ujangili ambao unatokea pale, kituo kile kitasaidia, wapewe na gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Iringa lipo eneo ambalo tunaomba Serikali ibadilishe matumizi ili gereza lile liondolewe eneo hilo litumike kama kivutio cha utalii. Eneo la Kihesa Mgagawa ambalo lipo katika Wilaya ya Kilolo, Mkoani

kwetu Iringa. Hili eneo lilitumika na wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika, walilala pale akina Mandela, walikuwepo akina Sam Nujoma, walikuwepo Walter Sisulu, Thabo Mbeki. Hawa watu ni maarufu sana sasa kuweka gereza sidhani kama tunawatendea haki, na hiki ni kivutio ambacho kingeweza kuwavuta watu wote katika nchi zao waje waone wapigania uhuru walikuwa katika maeneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Balozi aliishawahi kuja kutembelea lile eneo alisikitika sana kukuta kwamba kuna gereza. Nashauri ni bora hata kijengwe chuo cha utalii lakini pia hayo maeneo yatumike kwa utalii ili tuweze kutengeneza pesa. Pia itasaidia hata wananchi ambao wapo Kihesa Mgagao kujiajiri kwa kutumia utalii na barabara nyingi za pale zingetengenezwa. Hao watu ambao marais wao walikuwa wamekaa katika kile kituo wangekuwa wanakuja kutalii na ingesaidia kuongeza pato la utalii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niungane na wale wote waliozungumzia kuhusiana na tatizo la ndovu. Katika Mkoa wetu wa Iringa ndovu pia wamekuwa wakileta uharibifu mkubwa. Yapo maeneo ambayo yameathirika na tembo na haya maeneo mengi ni yale ambayo yamezungukwa na Ruaha *National Park*. Katika Jimbo la Isimani kuna Kata ya Idodi, Mlowa, Pawaga, Unyinga na kadhalika. Pia katika Jimbo letu la Kilolo kuna Mahenge, Nyanzwa na Ruaha Mbuyuni na changamoto kubwa kabisa ya hawa watu ni fidia ambayo wanapewa fidia kidogo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Malizia sentensi kengele imeshagonga.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba, pengine sasa hawa watu ambao wapo katika haya maeneo waweze kupatiwa hata miradi midogo midogo kama ufugaji wa nyuki ili waweze kusaidia. Tumesikia kwamba nyuki huwa wanasaidia kufufukuza tembo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nikushuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu kwa Taifa lakini pia kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuungana na wenzangu ambao wamemshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake katika kuhamasisha utalii, lakini pia Mradi wa *REGROW* ambao wenzangu wameuzungumzia ni mradi ambao ni wa matumaini makubwa sana katika Sekta ya Utalii katika uwanda wa kusini mwa nchi yetu. Mradi huu ulitupa hamasa sana na ulitupa matumaini mkubwa lakini utekelezaji wake unasuasua sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo wakati Waziri akifanya majumuisho tunaomba atoe msimamo wa Serikali, nini hatma ya huu mradi wa *REGROW* hasa kwa wananchi ambao wamejikita katika Sekta hii ya Utalii. Sekta ya Utalii ni muhimu sana katika uhai wa Taifa lolote lile. Ajira za vijana, lakini uhifadhi endelevu wa mazingira unategemea sana shughuli za kiutalii endelevu. Naomba niungane na wenzangu ambao wanazungumza kwamba pamoja na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kwa idadi kubwa ya watalii katika nchi yetu, bado kuna nguvu kubwa tunapaswa kuwekeza katika suala la kutangaza vivutio vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili la kutangaza, haitoshi tu kuongeza bajeti lakini suala zima la ushirikishwaji wa wadau ni muhimu sana. Huu ni mchango wangu wa nne kwenye sekta hii na kwenye Wizara hii ya utalii. Nilizungumza kabla na naomba nirudie tena, Balozi zetu Mwanadiplomasia wa Kitanzania ndio mwanadiplomasia pekee ambaye anapaswa kujibu hoja za *CAG*, anapaswa kutafuta wawekezaji, anapaswa kutafuta watalii, anapaswa kuboresha mahusiano ya nchi. Hatuwezi kufika

kwa sababu wanadiplomasia hawa hawajafundishwa *marketing*, hawajafundishwa utalii, *customer care* na si kazi yao ambayo imewapeleka katika vituo vya kazi huko nje.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza, wakati umefika wa Serikali kuona namna bora ya kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo zinajikita kwenye utalii, ku-*station* watu wao kwa gharama zao lakini wakapata nafasi katika balozi zetu, watu waliosomea utalii, kwa ajili ya kushughulika ku-*promote* utalii katika balozi zetu. Ukiuliza kwa nini tunashindwa wanakwambia sababu za kiusalama, sababu za kiusalama kwa nini wao wamekaa kwenye hizo ofisi?

Mheshimiwa Spika, hivi ni nini ambacho kinampa huyu Afisa wa Serikali ambaye ameajiriwa hadhi ya ziada kwamba usalama wa nchi uko salama kwa sababu yeye ameajiriwa? Kwa sababu yeye analipwa na Hazina? Kitu gani ambacho kinawafanya kuamini kwamba sekta binafsi sio wazalendo na kuwakaribisha ndani ya balozi zetu ku-*promote* utalii wetu kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi?

Mheshimiwa Spika, lazima tufike mahali tuaminiane. Lazima tufike mahali tuamini kwamba hata hawa ambao wako kwenye sekta binafsi wangeweza kufanya kazi kwenye sekta ya umma lakini kwa sababu sekta ya umma haiwezi kuajiri kila mtu ndio maana wameamua kujiajiri katika sekta binafsi. Mchango wao lazima uheshimike na lazima tuwape nafasi katika mawanda ambayo Serikali inaweza kuruhusu.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa katika utekelezaji wa shughuli za kiutalii, sawasawa na biashara nyingine, kodi ni nyingi sana. *Compliance* ambazo anatakiwa ku-*comply* mtu ambaye anajikita kwenye utalii ni nyingi mno kiasi ambacho haichochei watu hawa ku-*comply* na sheria zetu. Matokeo yake wanasuasua, matokeo yake mitaji yao inakufa na utalii wetu unashuka.

Mheshimiwa Spika, nina mfano hai utalii pale Mikumi hali ni mbaya, wafanyabiashara wanafunga ofisi zao, lakini wakati wanafunga ofisi zao tunaona idadi ya ndege zinazoshuka Mikumi

inaongezeka kila siku, lakini watalii hao ambao wanashuka pale Mikumi hawaji mjini, hawakai mjini, hawaji kuangalia vivutio pale mjini. Hakuna *package* ambayo inawakalisha pale Mikumi. Matokeo yake Serikali inapata fedha nyingi kutoka kwa watalii, lakini wananchi na hasa wafanyabiashara ambao wanajikita kwenye shughuli za kiutalii wanakufa kiuchumi na wanaondoka kwenye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jikumu la Serikali kuona namna bora ya kulinda wafanyabiashara wetu ambao wanajikita katika shughuli za kiutalii kama tunavyoweza kuwawezesha wakulima wengine vijana kwenye *block farming* na maeneo mengine. Ni muhimu sasa tukajikita kungalia namna bora ya kuwawezesha vijana ambao wamesomea utalii, shughuli za kiutalii namna ya kuwapa mtaji, namna ya kuwawezesha ili waboreshe huduma zao kwa ajili ya kuangalia ni jinsi gani wanaweza kuchangia katika shughuli za kiutalii.

Mheshimiwa Spika, siwezi kumaliza mchango wangu bila kuzungumzia migogoro kati ya hifadhi na wananchi. Wenzangu wamezungumza na naomba nilikazie. Tatizo la mipaka kati ya hifadhi na wananchi limekuwa kubwa kiasi ambacho mwananchi haoni kwamba anawajibu wa kulinda hifadhi zetu na hawa ndio walinzi namba moja. Pale Mikumi tuna changamoto katika Misitu ya Palaulanga, Mkwiva, Mbeleselo na maeneo mengine. Kule Kielezo na Kitete Msindazi katika Kata ya ulenge.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza sana, wakati umefika sasa Serikali kuona kilio cha wananchi na kilio chao ni kimoja tu wanakwambia kwamba kuna *GN* zaidi ya tatu ambazo zina *identify* mipaka kati ya hifadhi na kijiji. Ni mamlaka gani ambazo zinatoa hizi *GN*? Ni kwa nini hizi *GN* zimekuwa chanzo cha migogoro kati ya wananchi na Serikali yao?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kero ya ndovu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, malizia sentensi yako, kengele imeshagonga.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.”

Mheshimiwa Spika, pamoja na programu ya kutunza maliasili zetu, Serikali iweke usimamizi wa msitu hasa ya asili, ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya nishati. Katika kupangilia matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara zote zinazosimamia Maliasili, Ardhi, Kilimo, Wizara za Maji na pia Wizara inayosimamia Mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi mazingira yetu na kuwepo msukumo zaidi kwenye kuboresha mazingiara.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua zinazochukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala. Kuna mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma, Kata ya Inyala. Kutokana na mgogoro huu kuchukua muda mrefu na kusababisha hata uvunjifu wa amani, kuna ahadi ya mwaka 2015 alitoa Mheshimiwa Hayati Magufuli na kumwelekeza Waziri wa Ardhi na pia Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo kupitia upya mipaka ili wananchi wa kata za Inyala, hususani Kijiji cha Mwashoma waachiwe maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye mgogoro ni mashamba ya wananchi na wamekuwa walinzi wazuri wa misitu na vyanzo vya maji, ni imani yangu wakiachiwa hayo maeneo yanayogombewa na *TFS,* kuna maslahi mapana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Serikali kuweka umuhimu wa kipekee na kupewa kipaumbele kwa sekta ya utalii ili iendelee kuchangia pato la Taifa, uhifadhi wa mazingira, na ustawi wa jamii kupitia fursa za matumizi endelevu ya rasilimali za utalii. Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele kutangaza utalii kwa kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo Programu ya *Tanzania - The Royal Tour* ambapo kwa mwaka 2022, idadi ya watalii imeongezeka kwa asilimia 58 kufikia watalii 1,454,920. Kwa mwaka 2022 mapato yatokanayo na watalii yameongezeka kwa asilimia 93 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,527.72.

Mheshimiwa Spika, mchango huu wa sekta ya utalii bado ni mdogo sana kulinganisha na nchi shindani na hata kulingana na maoteo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(FYDP III 2021/2022-2025/2026)* umeelekeza kufikia idadi ya watalii wapatao milioni tano na kukusanya mapato ya kiasi cha dola za Kimarekani bilioni sita kufikia mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya utalii unakabiliwa na changamoto ya ushindani mkubwa katika soko la utalii wa

kimataifa hasa kutokana na miundombinu na hata mazingira ambayo siyo rafiki kwa wawekezaji ikiwemo utitiri wa tozo. Biashara ya utalii ni sawa na biashara zingine za nje zinazotegemewa katika mapato ya fedha za kigeni, lakini inakabiliwa na utitiri wa tozo katika mnyororo mzima na kupelekea kuwa mzigo mkubwa kupambana na ushindani wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, watalii kama ilivyo kwa biashara zingine wanaangalia sana ubora wa huduma pamoja na gharama katika mnyororo mzima wa utalii. Pamoja na nchi yetu kubarikiwa utajiri wa vivutio vya aina mbalimbali, inatakiwa kuwepo na mkakati madhubuti wa kuhakikisha uendelezaji wa vivutio ili kuongeza wigo wa shughuli za utalii na hata kuondoa tozo ambazo ni mzigo kibiashara. Serikali iangalie kuondoa kodi zote ambazo hazotozwi na nchi shindani na pia mnyororo wa biashara ya utalii ichukuliwe kama biashara ya nje *(export)*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa maandalizi ya hotuba nzuri, lakini zaidi kwa kuwa *open minded,* nimepata wasaa wa kuzungumza na Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu kuhusu sekta ya misitu na kwa kweli walinisikiliza na kupokea mawazo yangu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya misitu ni mtambuka kwa kiasi fulani, jana tumepitisha bajeti ya Wizara ya Nishati, moja ya mkakati wao ni kufikisha umeme vitongoji 15 kwa kila jimbo, lakini pia kuna miradi ya *REA III,* Awamu ya Pili, miradi ya ujazilizi wao wanaita 2A, 2B,2C na kadhalika na miradi ya *TANESCO,* yote hii inategemea kwa sehemu kutumia nguzo zinazotoka katika sekta ya misitu, lakini pia ujenzi wa miradi mbalimbali ya Serikali kuanzia majengo ya shule, zahanati, vituo vya afya na hospital za wilaya, ujenzi wake kwa sehemu unatumia mazao ya misitu kuanzia milunda, mbao, *plywood* na kadhalika. Hata Mji wa Serikali Mtumba, majengo mengi kama sio yote yanatumia bidhaa zinazotokana na misitu.

Kwa hiyo, sekta hii ni muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa, hata takwimu kwamba sekta hii inachangia 3% sio sahihi kwa sababu takwimu hii inaangalia tu mti/gogo, mara baada ya kuvunwa, bidhaa inayofuatia inaonekana sio msitu tena. Kwa hiyo, kwa ufupi sekta hii ni muhimu na tuendelee kuitizama na hasa katika suala zima la *EWP,* nashauri kongamano tulilofanya mwaka 2021 tuendelee nalo kila mwaka kwa nia ya kunyanyua sekta hii na hasa suala zima la *EWP*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *REGROW* mradi huu ambao ni mkopo wa Benki ya Dunia umekuwa unatekelezwa kwa kusuasua sana, huu ndio ukweli, mradi huu ukitekelezwa kwa kasi utasaidia sana kukuza utalii Kusini, utaboresha mazingira ya utalii na hivyo kuvutia wawekezaji zaidi. Mheshimiwa Rais ametufanyia kazi kubwa katika kututangazia utalii kupitia *Royal Tour,* kwa hiyo *REGROW* itasaidia sana kuendana na kasi ya kuongezeka kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa watu ambao nimeusemea sana mradi huu, nashauri tuongeze kasi ya kuutekeleza, ninaamini kwa kasi ambayo Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wake walionesha kwenye sekta ya michezo, wataitumia kusukuma mradi huu, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba mzigo mzito mtwishe Mndengereko, basi mimi namtwisha mzigo huu ili twende kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, ndege ndogo; kuna gharama kubwa sana ya usafiri wa anga kutembelea mbuga zetu, ushauri, kaeni ndani ya Serikali tupate ndege za *ability* ya kati ya watu nane hadi 14 ambazo zitaweza kutua mbugani, na hizi ziwe za *ATC,* kwa kuanza hata mbili zitafaa kuwa zina *shuttle* kati ya Dar es Salaam, *KIA* na mbuga zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa kushauri yafuatayo; kwanza Wizara ifanye utafiti wa kutosha kubaini chanzo cha tembo kwa nini wameamua kuhamia kwenye maeneo ya binadamu, tuondoe dhana ya ushoroba kuwa ndio chanzo cha kadhia hii. Je, huko

nyuma miaka minne iliyo pita shoroba hizi hazikuwepo? Mbona migogoro haikuwa mingi hivi? Kuja na majibu mepesi wakati watu wanauawa na tembo kila siku hakuisaidii Serikali. Tembo wamebadili tabia hawataki tena kukaa hifadhini na hata ulaji pia hawataki tena majani ya porini wanatamani mazao ya wakulima ndio maana tunasumbuana nao kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, kufanyike utafiti kubaini hizo zinazoitwa shoroba ili kuzibaini na kujua idadi na kuona namna gani ya kuzilinda ili kila kwenye shoroba kuwe na kituo cha askari wa wanyamapori ili kulinda shoroba husika

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wananchi kwenye uhifadhi ni mdogo sana na haulingani na nguvu zinazotumika kwani kufanya kazi ya uhifadhi kwa kutumia nguvu bila ushirikishwaji haiwezi kuleta matunda yanayotarajiwa. Hivyo basi Wizara ione namna ya kuelimisha jamii umuhimu wa hifadhi badala ya kupiga watu kila kukicha. Kitendo hiki kinakuza chuki baina ya wahifadhi na wanajamii.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Wizari hii walio wengi wanafanyakazi kwa mazoea na kukomoana ndio maana hata Waziri akija na malengo mazuri kwenye Wizara hii hawezi kukaa kwani atakuWa anakwaza maslahi yao binafsi na hivyo wanamhujumu makusudi na hatimae ataonekana hafai. Uwajibikaji wa pamoja kwenye Wizara hii ni msamiati mgumu sana na ndio maana migogoro haiishi ndani ya Wizara hii.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kiuchumi, kiplomasia, kisiasa na mshikamano wa Taifa letu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na kutatua changamoto nyingi sana

zinazowakabili wananchi hususan utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020-2025 kwa kila sekta, Mwenyezi awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mohamed Mchegerwa, Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Masanja na watendaji wakuu wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa jinsi wanavyotumikia nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson - Spika wetu, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, Wajumbe wa Kamati hii, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Bunge kutokana na mipango yao mizuri ya kufanikisha maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa kupitia hotuba ya mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya Maliasili na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuchimba mabwawa ya maji katika hifadhi zetu au kujenga mabwawa kwenye mito ndani ya hifadhi zetu, kwa sababu dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tibianchi na ukame mkubwa hivyo basi tatizo la ukosefu wa upatikanaji wa maji katika hifadhi zetu siyo suala litakalopungua kwa haraka bali litazidi kuongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iajiri Maafisa Wanyamapori katika Halmashauri zote nchini ambazo zinapakana na Hifadhi za Taifa. Kwa kuwa kumeongezeka tatizo la wanyama wakali na waharibifu kutoka ndani ya hifadhi zetu na kwenda kwenye maeneo ya makazi ya watu na kupoteza maisha na kuharibu mali za wananchi, hali hii imekuwepo katika Halmashauri ya Mbulu Mji, ninaomba tupatiwe mtumishi huyu muhimu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutowepo kwa mahusiano mazuri kati ya wananchi na askari wa hifadhi zetu hali inayosababisha athari nyingi ikiwemo vifo na kupoteza mali, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwepo kwa ratiba ya vikao vya ujirani mwema kila robo mwaka kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi zetu nchini kwa kuunganishwa na

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na sisi Wabunge tushiriki kwa maslahi mapana ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya uhalisia wa sheria za fidia na kifuta machozi kwa wananchi wanaoathiriwa na wanyama wakali na waharibifu wa mazao yaliyoko mashambani na kwenye maghala yao hali ambayo imesababisha umaskini mkubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii iangalie uwezekano wa kuwepo kwa kitengo cha kuratibu, kubaini na kutangaza vivutio kwenye tovuti za halmashauri ili kukuza na kuchochea utalii wa ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara iangalie utaratibu mzuri wa kutoa michango ya miradi ya maendeleo kwa jamii katika huduma za sekta kwenye maeneo hayo ya hifadhi ambayo yanapakana na wananchi wetu ili kuongeza mahusiano na hamasa ya kuthamini uendelevu wa hifadhi za taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbushia umuhimu mkubwa sana wa ziara ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri katika jimbo langu la Mbulu Mjini kwenye Kata za Gehandu, Bargish, Daudi na Marangw ambazo zinapakana na hifadhi ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Msitu wa Marang kwa ajili ya kufanya mikutano ya hadhara ya ujirani mwema na ufafanuzi wa sheria za hifadhi na kuhamasisha jamii kuwa sehemu ya walinzi na wahifadhi wa rasilimali hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Francis Masanja na wataalam wa Wizara, taasisi zilizo chini ya Wizara na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye changamoto ya magugu vamizi katika mbuga zetu za wanyamapori na maeneo ya akiba, udahili wa wanafunzi kutoka nje katika Chuo cha Wanyamapori Mweka na fursa za utalii zilizopo katika jimbo la Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ripoti za kiutafiti zilizofanyika katika Mbuga za Serengeti, Ngorongoro, Mapori Tengefu zimeonesha kwamba magugu vamizi yamesambaa katika maeneo mengi ya hifadhi za wanyamapori na mapori ya akiba yaliyoko nchini.

Mheshimiwa Spika, aina ya magugu vamizi hayo yaliyoko katika baadhi ya maeneo nimeayaorodhesha. Magugu vamizi yaliyoko Ngorongoro ni *Azolla filiculoides (red water fern), Argemone mexicana (Mexican poppy), Datura stramonium (jimsonweed), Gutenbergia cordifolia, Acacia mearsii* na *Parthenium hysterophorus (famine weed);* huko Serengeti magugu vamizi yaliyoonekana huko ni *Parthenium hysterophorus, Opuntia stricta, Tithonia diversifolia, Lantana camara, Chromolaena odorata* na *Prosopis juliflora;* huko mbuga ya wanyama ya Burigi Chato magugu vamizi yaliyopo ni *Tegetes minuta* na *Argemone Mexicana;* na huko *Mahale Mountains National Park* mmea uitwao *Senna spectabilis (Caesalpiniaceae)* umekuwa ni gugu vamizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uvamizi wa magugu yaliyotajwa hapo juu, maisha ya wanyamapori katika maeneo mengi ya Hifadhi za Taifa yapo hatarini kwani uwepo wa magugu haya umesababisha athari nyingi, kubwa ikiwa ni kuua majani na mimea mingine inayoota karibu yake.

Mheshimiwa Spika, magugu vamizi hayo yana tabia inayoonesha kwamba yanapoota hakustawi kitu kingine kwa kuwa hufunika eneo lote na kusababisha kutoweka kwa nyasi na kuathiri malisho ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, hata ripoti moja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali *(CAG)* ilionesha kuwepo kwa magugu vamizi katika Hifadhi ya Ngorongoro ambayo inahatarisha uwepo wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo hivi sasa kunatakiwa kuwe na mikakati dhabiti ili kudhibiti magugu haya kwani yanasambaa kwa kasi kubwa sana katika mbuga mbalimbali na maeneo ya akiba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iwe na mpango kazi maalum na iwekeze kikamilifu kwenye kudhibiti magugu vamizi ili kulinda ikolojia ya mbuga zetu ziweze kutoa huduma ya kuwapatia wanyama chakula.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka hutoa mafunzo ya usimamizi wa wanyamapori na utalii. Ni chuo kimojawapo pekee chenye hadhi kubwa hapa Barani Afrika. Chuo hiki hutoa Shahada, Stashahada na Astashahada katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, chuo hiki hupokea idadi kubwa ya wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali Afrika. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya kupokea wanafunzi kutoka katika baadhi ya mataifa ya Afrika kama Kenya na Msumbiji. Vigezo vilivyowekwa na *NACTE* vimekuwa vinazuia wanafunzi kutoka mataifa haya kujiunga na Chuo cha Mweka.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Wizara ikae na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na *NACTE* ili waangalie upya vigezo vya kujiunga na Chuo cha Mweka ili tuwe na muundo wa kuwasaidia wanafunzi kutoka nchi hizi wapate elimu kama walivyotumwa na nchi zao. Haifurahishi kuona mtu anatumwa na nchi yake kusoma shahada, na akifika ananyimwa fursa na kuambiwa asome stashahada. Jambo hili limekuwa siyo rafiki, na limepunguza idadi ya wanafunzi kutoka nje na kutunyima fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro ni mdau muhimu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninasema hivyo kwa sababu Mlima Kilimanjaro na viunga vyake ni moja ya vivutio muhimu vya utalii ambavyo vimeipatia Tanzania heshima kubwa kimataifa. Ndani ya Mlima Kilimanjaro na maeneo yanayouzunguka mlima kuna vivutio vya aina mbalimbali vya kitalii.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Rais wetu alishiriki kikamilifu kwenye filamu ya *Royal Tour* iliyokuwa na kipengele cha kutangaza utalii ukiwepo Mlima Kilimanjaro. Kutokana na hili, ni vyema tukachukua tahadhari mapema ili watalii watakapoanza kumiminika kuja kutalii Kilimanjaro kama ambavyo imeanza kujitokeza wakutane na mazingira mazuri. Tusipofanya hivyo, watalii wakija wakikumbana na changamoto watapeleka sifa mbaya kuhusiana na eneo letu, na kuathiri idadi ya wageni watakaotembelea Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kwenye suala la vivutio vya Mlima Kilimanjaro na umuhimu wa kutatua changamoto za vivutio hivyo ili kuwezesha watalii kufika maeneo hayo kirahisi na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni imegundulika kwamba mti mrefu kuliko yote Barani Afrika ujulikanao kama Mkukusi umepatikana katika Kijiji cha Tema, Kata ya Mbokomu, Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoani Kilimanjaro. Mti huo ambao una urefu wa mita 81.5 upo ndani ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro *(KINAPA)*. Ugunduzi huo umeonesha pia huu ni mti wenye miaka mingi zaidi duniani kwa aina hii ya mti kwani una miaka 600.

Mheshimiwa Spika, mti huu umeupa heshima Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa jumla. Kugundulika kwa mti huo kumeongeza chachu ya watalii kupanda Mlima Kilimanjaro na wengine kwenda kushuhudia mti huo. Licha ya mti huu kuwa kivutio ambacho kinaweza kuiingizia Serikali fedha za kigeni, lakini changamoto iliyopo ni ugumu wa kuufikia mti huo. Ili kufika katika eneo la Mrusungu ambapo ndipo ulipo mti huo mrefu zaidi, ni safari ya kutembea kwa mguu kwa takribani muda wa saa nne kwenda na kurudi kwa kupita katika milima, mabonde, mito na makorongo.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hii, ninaishauri Serikali iboreshe miundombinu ya barabara ili kuweza kuufikia mti huo iwapo watalii watataka kwenda kuuona. Barabara ya kufika kwenye mti huu ni mbaya sana, na hii ni changamoto inayowafanya watalii wasitembelee eneo hili. Tunaiomba *TANAPA*

isaidie ujenzi wa hii barabara katika mipango yao ya mwaka 2023/2024. Katika mwaka ujao wa fedha, *TANAPA* ina programu ya kujenga barabara mpya zenye urefu wa kilometa 500, na kukarabati kilometa 10,500. Katika hizo barabara, tunaomba tusisahau barabara inayokwenda kwenye huu mti mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa eneo hili linaendelezwa ili liwe na hadhi ya kuwa sehemu ya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro. Vilevile ninaishauri Serikali itengeneze utaratibu wa kuhakikisha wanaokwenda kuuona mti wanalipa ada.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili utahusu maporomoko ya maji Materuni au kwa jina lingine *Mnambe Waterfalls.* Maporomoko haya ni moja ya maporomoko ya maji katika Mto Mware, Kata ya Uru Mashariki, Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro. Maporomoko haya yanapatikana katika Kijiji cha Materuni pembezoni mwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Maporomoko haya yana urefu wa zaidi ya mita 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kivutio cha maporomoko ya maji, eneo hili la utalii limekuwa maarufu kwani watalii wanaokwenda kuona maporomoko hupata fursa ya kutembelea shamba la kahawa na kujifunza jinsi kahawa inakuzwa, kuvunwa na kusindikwa. Watalii hupata fursa ya kujaribu kwa mkono yao kuchoma na kuandaa kikombe cha kahawa kwa kutumia njia asili ya Wachagga.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayokabili eneo hili ni ubovu wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometa 15 kutoka Mjini Moshi. Kutokana na ubovu wa barabara, watalii hupata shida kufika katika eneo hili. Changamoto za barabara katika maeneo yanayopeleka watalii kwenye vivutio vya Mlima Kilimanjaro zinatakiwa zipewe kipaumbele cha pekee na Wizara ya Maliasili na Utalii kwani wao ni wanufaika wakuu.

Ninaishauri Serikali iachane na kuzitegemea *TARURA* na *TANROADS* kwani mitandao yao ya barabara ni mingi, na hawajatoa kipaumbele kikubwa kwa barabara za jimbo langu kama zile za kupeleka watalii kupitia *Umbwe Gate, Kidia VIP*

*Route, Materuni Waterfalls,* Mti Mtefu Kijiji cha Tema huko Mbokomu, Kanisa la Kibosho Singa, na maeneo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, huu ni wakati wa kutumia michango ya *Corporate Social Responsibility (CSR)* unaotokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro kutengeneza miundombinu ya barabara katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kukuza utalii wa fukwe hasa katika Mkoa wa Mtwara, fukwe za Bahari ya Hindi ambazo ni nzuri na bado hazijachafuliwa lakini uwekezaji wake upo duni sana. Hali hii inanyima fursa mbalimbli katika mkoa wetu. Pale Msimbati kuna fursa kubwa ya uwekezaji katika utalii, Serikali inasema nini?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanyika, nashauri yafuatayo; kwanza, miundombinu kuelekea kwenye vivutio vya utalii ni mibovu sana kiasi cha kukatisha tamaa watalii kuvitembelea; pili, Ukerewe kuna vivutio vingi kama jiwe linalocheza la Nyabulebeka, fukwe za Rubya, mapango ya Handebezyo na vingine vingi, lakini hakuna mfumo maalum uliopo kwa ajili ya kuvitangaza.

Mheshimiwa Spika, nashauri wataalam wa Wizara watembelee Ukerewe na kukaa na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ili wapate masada wa kitaalamu katika sekta ya utalii ili vivutio hivi vilinufaishe Taifa na jamii ya wananchi wa Ukerewe.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii Kanda ya Kusini *(REGROW)*, utekelezaji wa mradi huu umesaidia kuboresha miundombinu katika hifadhi na utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa ya kukuza utalii na maliasili zetu. Pongeza pia za kipekee zimuendee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa mchango wake binafsi katika kuendeleza Wizara hii kupitia *Royal Tour.*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika kujenga kituo cha Utalii Kusini chini ya *REGROW* kiitwacho Kihesa-Kilolo ambacho kinatakiwa kujengwa katika Manispaa ya Iringa ambalo ni lango la utalii Kusini. Umuhimu wa vituo hivi vya kitalii duniani ni kutoa taarifa na elimu kwa watalii kuhusiana na mwelekeo au ramani ya eneo husika ambalo mtalii anatakiwa kutembelea, kutoa taarifa ya huduma zilizoko katika eneo hilo la utalii, ni sehemu inayomuunganisha mtalii na eneo la utalii. Hivyo basi, ni lazima tukubaliane kuwa pamoja na uboresha mbalimbali unaofanyika kwenye mbuga na hifadhi zetu, bado tujue ni muhimu sana kuwa na kituo cha utalii au *information centre* ambacho ni Kihesa Kilolo.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kitatakiwa kutoa taarifa za Utalii Kusini yote, sio Iringa pekee yake. Utafiti unaonesha ili tufikie lengo la Ilani yetu ya kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025; basi ni muhimu kujenga kituo hiki. Sababu ni kwamba huwezi kupeleka watalii wote hawa Kaskazini, utaharibu kabisa ikolojia ya utalii wenyewe Kaskazini. Tabia za watalii hutaka kupata taarifa mapema kutoka kwenye vituo hivi kabla hawajaanza safari ya kutembelea eneo husika. Sasa kwa wale wanaotaka kuja Kusini wanapata taarifa wapi?

Mheshimiwa Waziri, msiseme tu muda unaturuhusu mpaka mwaka 2025, utakuwa unaenda kinyume na Mpango wa Miaka Mitano na Ilani ya CCM, inayotutaka tuongeze pato la Taifa. Mchango wangu namba mbili, moja ya sababu kubwa inayowafanya watalii kutorudi nchini ni kukosekana kwa huduma bora muhimu ikiwepo, kupatikana kwa fedha za kigeni. Mheshimiwa Waziri fanya jitihada zako binafsi bila kuwategemea Wizara ya Fedha kuhakikisha, maduka ya fedha za kigeni yanarudishwa nchini, hasa maeneo ya utalii. Pigania Wizara ya Fedha kupitia *BOT* waondoe masharti yasiyokuwa rafiki yanayosababisha maduka ya kubadilishwa fedha za kigeni yasiwepo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Iringa Mjini kama lango au *reception* ya Utalii Kusini, lazima sasa tukuombe Mheshimiwa Waziri kuweka msukumo mahsusi wa kuwaandaa watu wa Iringa kuwa wakitalii. Mamlaka za Iringa kuwa kitalii, mazingira ya Iringa kuwa kitalii ikiwemo kuhakikisha misitu ya asili inalindwa kwa kushirikia na programu za *TFS,* kama kupanda miti, kutunza miti ya asili, kutoa mizinga ya nyuki ili kupunguza ukataji wa miti hovyo kuifanya Iringa kwa *Southern Geneva);* ikiwemo kuanzisha *zoo,* hili mimi mwenyewe naweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapo *wind-up* atoe kauli thabiti amejipanga vipi kuwafanya watu, viongozi, mji wa Iringa, mazingira ya Iringa kuwa ya kitalii *(Southern Geneva of Africa).* Naunga mkono hoja naomba kuwasilisha.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kutujalia uzima. Nikupongeze wewe kwa usimamizi na uendeshaji mzuri wa Bunge letu tukufu. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake imara na dhamira yake ya dhati ya kuleta mabadiliko makubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa, Naibu wake Dada yangu, Mary Masanja na timu yao kwa kazi kubwa na nzuri wanaoiyafanya kwenye Wizara hii. Hii ni miongoni mwa Wizara muhimu kwenye uchumi na ukuaji wa uchumi wetu. Kama Taifa linaloendelea, tunahitaji kuwa na sekta imara ya utalii na ninyi ni watu sahihi kwa sababu mnaifanya kazi hiyo kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sikuweza kupata nafasi ya kusimama kuchangia, lakini naomba nifikishe mawazo yangu kwa maandishi ili kusaidiana na kaka yangu Mchengerwa na dada yangu Mary kueleza mambo machache.

Mheshimiwa Spika, nianze na utalii; nipongeze jitihada kubwa zinazofanyika katika kuvutia watalii nchini. Kwa takwimu za Wizara ni kwamba zaidi ya watalii milioni 1.4 wametembelea

hifadhi na mbuga zetu za wanyama. Haya ni mafanikio makubwa sana, lakini nadhani bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuongeza tija zaidi. Natambua yapo maeneo mengi ambayo kama tutaweka mkakati wa kuyafikia basi tunaweza kuwa na idadi kubwa zaidi ya tuliyonayo sasa. Kwa mfano, Mkoani kwangu Singida tuna ardhi nzuri na hali ya hewa rafiki kwa watalii, uwepo wa Ziwa Singidani lenye ndege adimu, lakini nyumba za utamaduni (tembe, vibuyu na vipeyu). Hili ni eneo ambalo linaweza kuongeza tija kwa watalii kwa kuwa sio kila mtalii anakuja nchini kuangalia wanyama, wengine hufuata kujifunza tamaduni, mbali na hilo Singida ni mkoa ambao uko katikati ya nchi hivyo kutangazia dunia kuwa ukiwa hapa ndio utakuwa katikati kabisa mwa Tanzania kila mtalii atatamani kuona Singida inafanana vipi.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Singida kuna mlango wa mkondo wa bonde la ufa katika Kijiji cha Kinyamwenda, lakini bado hakuna jitihada za makusudi kulihifadhi eneo hilo ama kulitangaza kwa nguvu katika kuvutia utalii.

Kuhusu mapori ya akiba; mkoani kwangu kuna mapori ya akiba ya Mgori na Rungwa ambayo ni muhimu kwa ustawi wa Taifa letu. Mapori haya ni sifa na fahari kwa wananchi wa Singida. Lakini kuna mambo ambayo kama Serikali tunapaswa kuyapa kipaumbele. Wanawake wa Singida bado ni masikini hivyo, naomba uwepo wa mapori haya ukawe na baraka kwao. Wengi walikuwa wakihemea kuni kwenye maeneo ya jirani nje ya mapori, lakini kwa sasa wanakutana na vitendo viovu. Itoshe kusema basi ukatili huu dhidi ya wanawake ukomeshwe na Wizara ione umuhimu wa kusaidiana na jamii kwa kuwapa wanawake hawa majiko ya gesi ili wawe mabalozi wazuri wa kulinda mazingira ya ndani na nje ya mapori haya. Kwenye maeneo mengine yanayohusika na Hifadhi za Taifa kama Ngorongoro, mamlaka imekuwa mstari wa mbele kushirikiana na jamii kupitia *CSR,* basi na huku ikawe hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuomba Wizara ya Maliasili na Utalii itenganishwe kuwe na Wizara ya Utalii na kuwe na Wizara ya Maliasili na Mambo ya Kale. Kwa nini nasema hivyo Wizara ya Maliasili na

Utalii imekuwa ikitumia muda mwingi kushughulikia migogoro ambayo inatokea kwenye mapori ya hifadhi badala ya kutumia muda huo kutafuta namna bora ya kutangaza vivutio vyetu na kuutangaza utalii wetu ambao una vivutio vingi ambavyo bado hatujavitangaza vizuri.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima. Nitumie fursa hii kumpongezaza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujitoa yeye mwenyewe kwa kucheza filamu ya *Royal Tour* ambayo imeinua sekta ya utalii hapa nchini. Nipongeze pia uongozi wa Wizara kwa kazi za kutumikia Watanzania kwa moyo na bidii kubwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwakumbusha kuwa Wizara hii imepewa jukumu kubwa la uhifadhi wa maliasili zetu. Uhifadhi huu ni kwa aijili ya matumizi na manufaa kwa Watanzania. Tungependa kuona kuwa uhifadhi huu unawasaidia Watanzania na usiwe kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pale Kilwa Kisiwani kumetangazwa kuwa ni sehemu ya urithi wa dunia na Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori *(TAWA)* imepewa jukumu la usimamizi wa eneo hili la utalii ambapo Serikali imeboresha miundombinu ili iwe rafiki kwa aijili ya watalii wanaokuja Kilwa kujionea historia ya Kilwa Kisiwani mji ambao ulikuwa wa kwanza katika Pwani ya Afrika Mashariki kujitengenezea fedha zake yenyewe. Tunachokumbusha hapa ni kwamba Serikali itimize wajibu wake wa kutoa *CSR* kwa Wana-Kilwa Kisiwani kwa kuwajengea miundombinu ya shule ya msingi na zahanati kama ambavyo tumetarajia.

Mheshimiwa Spika, Kilwa Kivinje ni miongoni mwa maeneo yenye historia kubwa hapa nchini; Kilwa Kivinje ndipo palipokuwa na soko la watumwa; Kilwa Kivinje ndipo palipokuwa ni njia ya kusafirisha watumwa; na Kilwa Kivinje ndipo palipokuwa makazi ya Waarabu na baadae Makao ya Wajerumani. Serikali ichukue hatua ya kukarabati soko lile lililokuwa la watumwa ili liendelee

kubaki katika uhalisia wake kulinda historia. Pia Serikali ikarabati na kuhifadhi magofu ya Kilwa Kivinje ili kulinda historia na kuifanya Kilwa Kivinje kuwa ni sehemu ya utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika Kijiji cha Mchakama, Mavuji, kuna msitu wa hifadhi unaosimamiwa na *TFS* kwa upande wa Kusini Mashariki mwa kijiji. Kwa upande wa Kusini-Magharibi, kijiji kimepitiwa na Mto Mavuji ambao ni chanzo cha maji na tunachoendelea kukihifadhi kwa kuzingatia sheria ya kutoingilia eneo la mita 60 kutoka ukingo wa mto. Kwa muktadha huo, kijiji kimebakiwa na eneo dogo la makazi na taasisi za pale kijijini. Wananchi wanakosa eneo la kufanya shughuli za kiuchumi. Wananchi wangu kutoka Mchakama walituma uwakilishi wao mwaka jana kuja Dodoma kukutana na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa lengo la kuomba wapatiwe sehemu ya hifadhi ya msitu kwa ajili wa shughuli za kiuchumi. Niliongozana na uwakilishi huo hadi ofisini kwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja na kukabidhi barua ya maombi yetu yakiambatana na muhtasari wa kijiji.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa bado Wana-Mchakama hawajajibiwa ombi lao na hatujaona hatua ya Wizara ya kugawa eneo la hifadhi ili wanakijiji wapate kufanya shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo bila kukiuka sheria. Tunakumbusha hapa, maombi yetu yafanyiwe kazi ili wananchi wale wapate eneo kufanyia shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri wanazofanya katika sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni muhimu Mheshimiwa Waziri atambue kwamba jeshi letu la askari wa wanyama pori linahitaji

kufanyiwa tathmini ya kina ili lifanye kazi kwa weledi mkubwa na kufuata misingi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za wananchi kuingia hifadhini, lakini baadhi ya askari hawa wamekuwa wakiua watu, wakijeruhi watu na wakipora mifugo ya watu kiholela. Kwa kweli mwananchi anayeishi karibu na hifadhi mimi naamini ndio wahifadhi wa kwanza kama mahusiano yatakuwa mazuri. Kwa sasa wananchi ni bora akutane na chui au simba ataweza kujiokoa kuliko kukutana na askari wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, jeshi hili kwa jinsi linavyokiuka utawala wa sheria na kunyanyasa sana wananchi. Haikubaliki na haipendezi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni wanyama kuvamia makazi ya watu hususani tembo. Hili tatizo linaendelea kukua kwa kasi sana na wanyama hawa wakivamia maeneo ya wananchi wanasababisha uharibifu mkubwa wa mazao, lakini wazee na watoto wanapoteza maisha na fidia kwa matukio haya kwanza hayaendani na hali iliyopo ya uhalisia kwa sasa, lakini pia hayatolewi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Wizara hii iweke mkakati madhubuti kuweza kushughulikia matatizo makubwa wanayokumbana nayo wananchi waishio pembezoni mwa hifadhi hizi, wananchi hawakupenda kuzaliwa wala kuishi pembezoni mwa hifadhi, ila wamejikuta wamezaliwa karibu na hifadhi. Tunaomba muwasaidie, Mheshimiwa Waziri Mchengerwa nakuamini. rekebisha hii sekta, okoa wananchi walioteseka kwa muda mrefu, angalia kwa jicho la ziada jeshi hili, wananchi wa maeneo haya mioyo yao inavuja damu kwa mateso makali, rudisha mshikamano na umoja wa jeshi hili na wananchi. Nashauri watumie nguvu hizo kupambana na majangiri na sio wananchi ambao makosa yao yanarekebishika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii

iliyotolewa siku ya Ijumaa tarehe 2 Juni, 2023 kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuitangaza nchi yetu ya Tanzania kupitia filamu ya *Royal Tour* hali iliyopelekea watalii wengi kuja Tanzania kutembelea vivutio via utalii.

Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Waziri wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii pamoja na timu nzima ya Wizara yake kwa usimamizi wa Wizara hii. Pamoja na mambo mengi mazuri yanayotekelezwa na Wizara hii naomba kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo; kwanza malikale na maadhimisho; napenda kuishauri Serikali iweze kuyapa *GN* Maadhimisho ya Majimaji ya Nandete Kilwa mkoani Lindi ili yaweze kuingia katika urithi wa Taifa. Pia itenge bajeti kila mwaka kuanzia mwaka 2023/2024 na kupangiwa taasisi simamizi smbamba na kujenga miundombinu muhimu ya kutunzia kumbukizi muhimu zilizotumika wakati wa vita hivi vilivyopiganwa chini ya wakoloni wa Kijerumani kuanzia mwaka 1905 hadi 1907.

Mheshimiwa Spika, maboresho katika kumbukizi hii yataboresha na kuongeza mapato ya Serikali na kuinua uchumi hapa nchini kwa kuwa kumbukizi hizi zipo karibu na vivutio vingi vya utalii kama vile pango kubwa kuliko yote Afrika Mashariki la Nang'oma lililopo Kijiji cha Nandembo. Boma la wakoloni wa Kijerumani la Kibata, ziwa lenye viboko wengi la Maliwe lililopo katika Kijiji cha Ngea, magofu ya kale ya Kilwa Kisiwani, Songomnara na Kivinje, viboko albino waliopo katika Mto Nyange, Jiwe la Jahazi Kilwa Kisiwani na Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu urejeshaji wa malikale zilizochukuliwa na wakoloni, naishauri Serikali ifanye jitihada za dhati ili kuhakikisha malikale mbalimbali zilizochukuliwa na wakoloni ziweze kurejeshwa kama vile kurejeshwa kwa mjusi mkubwa *(dinosaur)* ambaye alichukuliwa katika Kijiji cha Tendeguru Wilayani Lindi mkoani Lindi na urejeshaji wa mafuvu ya machifu na kadhalika.

Kuhusu malipo ya fidia zinazotokana na athari za vita vya Majimaji, naishauri Serikali isimamie na kuweka mkakati wa kulipwa fidia za vita ya Majimaji kwa kuwashirikisha wananchi wa

jamii zilizohusika na vita hivyo. Naishauri Serikali ianzishe mchakato wa kudai fedha hizo ili zikipatikana ziweze kutumika kwa kujenga miundombinu ya kijamii kama hospitali, shule na barabara.

Mheshimiwa Spika, uwepo mpango *(succession plan)* kwa watumishi wa Idara ya Makumbusho kwa kuanzia na makumbusho mbili za Dkt. Livingstone za Tabora Kwihala, Tabora na Kigoma Ujiji; Tabora Kwihala kuna Mzee wa miaka 73 anaendelea kuhudumu na Kigoma Ujiji kuna Mzee wa miaka 69 anahudumu pale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda ajiandae. Hawa wote watachangia dakika tatu kila mmoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika ni nyota wa mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi ni kwamba ameanza na mkakati wa *Royal Tour* mkakati unaokwenda vizuri na majibu tunayaona. Ameingia na mkakati wa kuhamasisha katika michezo ikiwa ni sehemu ya utalii na mkakati wa hamasa ya michezo umejibu na matokeo tumeyaona Algeria, timu yetu na vijana wetu wamefanya vizuri. Tunawapongeza sana, hatuna tunachowadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge inayohusu suala zima linalohusianisha juu ya mifugo na hifadhi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumejipanga vema. Moja katika mipango yetu ni kuhakikisha *ranch* zetu za *NARCO* tutazitumia vema. wale wafugaji ambao wamekuwa wakihangaika sasa tunakwenda kuziboresha na tunaanza na pale Mkata ili wale wafugaji wanaoondoka katika Bonde la Mto Kilombero tutakwenda kuwapa eneo pale, ili ile mifugo isiadhirike zaidi, iweze kuingia katika eneo hili na iendelee kutoa mchango katika pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatoka hapo tutakwenda na maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba wafugaji wetu waweze kuwa na maeneo na ndio kitakuwa kipaumbele chetu cha kwanza kwa ajili ya aeneo hili la Serikali kwa maana ya *ranch* zetu.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni jambo maalum ambalo limezungumzwa hapa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusiana na Msomela. Msomela inakwenda vizuri mno, hivi sasa tunavyozungumza tumejenga kituo kizuri cha maziwa na ili kuhakikisha kituo kile kiwe na tija tumehakikisha tumeunda ushirika wa wafugaji na ushirika ule tutakwenda kuwapa ng'ombe bora ili waweze sasa kupiganisha na ng'ombe walioko pale na kusudio letu waweze kukilisha kituo chetu lita 5,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, vile vile tumeenda kuwafunza namna ya kuwa na mashamba ya malisho yanakwenda vizuri mno. Tatu, tumeimarisha eneo la majosho na mabwawa ya kunyweshea mifugo. Tunayo mabwawa mawili; moja linajengwa na Wizara ya Maji na lingine tunajenga Wizara ya Mifugo na Uvuvi, yanakwenda vizuri na tutahakikisha kwamba yanakamilika ili kusudi watu wote wanaotoka Ngorongoro wanakuja pale Msomela waweze kufanya shughuli zao za uzalishaji wa mifugo kwa usalama. Vile vile, kwa hakika kinakwenda kuwa kituo cha biashara ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, atafuatiwa na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda na Mheshimiwa Mary Francis Masanja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuanza kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mary Masanja.

Mheshimiwa Spika, kiukweli Mheshimiwa Waziri Mchengerwa anafanya kazi nzuri kama vile Mayele alivyofanya kwa timu ya Dar es Salaam *Young Africans. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikiliza hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na wengi walikuwa wakizungumzia maeneo yenye migogoro ya ardhi kati ya hifadhi, vijiji na vitongoji mbalimbali hapa nchini. Vilevile…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Ndejembi, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nampa tu taarifa Mheshimiwa Ndejembi kwamba kule Algeria aliyeleta kaushindi kale kagoli moja alikuwa ni Juma sio Mayele. Kwa hiyo, lile goli moja sio la Mayele ni la Juma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Ndejembi, unapokea taaria hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, sipokei taarifa hiyo kwa sababu niliposema Mheshimiwa Mchengerwa ni kama Mayele ni kwa sababu Mayele ndio *top scorer* katika mashindano yale, kwa maana ndio nyota wa mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zilizungumzwa hoja za Kamati ile ya Mawaziri Nane. Katika maeneo ambapo timu ile ya Mawaziri Nane ilipopita kuna maeneo ambayo hakuna migogoro kabisa na tayari taarifa ile ilikuwa imekwishapelekwa katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa. sasa nitumie Bunge lako hili kuwataka Wakuu wa Mikoa wote waliopelekewa taarifa ya migogoro yote ambayo imekwishatatuliwa waweze kwenda *site (field)*. Kwa sababu tumesikia taarifa hapa Wabunge wakisema wanabaki kule mikoani na hawapeleki taarifa hizi kwa wananchi. Basi, hawa Wakuu wa Mikoa waende kule *field* kwa ajili ya kupeleka taarifa

ya utatuzi wa migogoro ile kwa wananchi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kulizungumzia jioni hii ya leo ni suala la uanzishaji wa maeneo mapya ya kiutawala. Hili ndilo limekuwa chanzo kikubwa cha migogoro. Kuna vitongoji na vijiji vinaanzishwa katika hifadhi. Sasa sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, safari hii tutahakikisha hatuanzishi maeneo mapya ya utawala bila *consultation* ya Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili na Utalii lakini vile vile Wizara ya Ardhi, kuhakikisha kwamba maeneo yanayosajiliwa hayatokuja kuwa na migogoro siku za usoni. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tumeona hiyo imekuwa ni changamoto sana. Kwa kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Francis Masanja na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kweli kama alivyotangulia kuzungumza Mheshimiwa Ndejembi hapa, Wizara ya Ardhi ni kiungo kati ya Wizara zile za Kimkakati katika kutatua migogoro mbalimbali hapa nchini. Katika mazingira ya kawaida Serikali iliona umuhimu wa kuwa na Timu Maalum ya Mawaziri Nane kupita katika maeneo yote ya migogoro nchini na ilitoa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, yale maeneo machache ambayo yamebaki, tunaendelea kuhangaika nayo kwa ajili ya kutatua ile migogoro. Niwape tu *comfort* wananchi kwamba wawe watulivu katika kipindi hiki cha kutatua hii migogoro ambayo kimsingi

inakwenda kumalizika hasa kwenye hii mipaka ya hifadhi na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kawaida yale maoni yote ambayo nimesikia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge yanayohusu hii migogoro ni maelekezo kimsingi tunayapokea kwa mikono miwili na tutatoa ushirikiano mkubwa sana kwa sababu maeneo mengi Wabunge wanasema hatushirikishwi, hatushirikishwi. Tunapokwenda uwandani hatuwapi taarifa lakini ukweli wana majukumu mengi sana ambayo wakati mwingine yanawatenga na zile shughuli za kiutendaji. Hata hivyo, ahadi tunayoitoa Wizara ya Ardhi…

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pinda, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwijage.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Pinda. Jukumu muhimu la Mbunge ni maslahi ya wananchi, hakuna kazi yoyote ninayoweza kupewa na mtu yeyote zaidi ya kazi ya wapigakura wangu. Wawe wanatujulisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine mnakuwa hapa Dodoma na Kamati zenu zimepewa na Spika, mnashindwa kwenda majimboni Serikali inapokuwa inakwenda huko. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba sio kila Mbunge anakuwa sehemu ambayo Waziri yupo. Waziri anakwenda anafanya kazi yake, lakini hoja ya Msingi ni Mbunge kutaarifiwa ili hata yeye asipokuwepo awepo mwakilishi wake aweze kumpa mrejesho. Hata hivyo, hakuna uhalisia wa kufikiri kwamba kila Waziri anapokwenda kwenye ziara Mbunge atakuwepo, hakuna huo uhalisia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hiyo malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana huko ndiko nilikuwa naelekea. Nataka tu kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, wakati wote wa zoezi hili tutawarifu Waheshimiwa Wabunge na watuwie radhi kama huko nyuma walikuwa hawaarifiwi. Nia yetu ni kuongeza mshikamano katika kutatua migogoro ambayo inatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo kwa kweli tumwachie mtoa hoja ili aweze kwenda kufanya majumusiho ya mwisho kabisa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Francis Masanja, mtoa hoja ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hajaanza kuzungumza. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni familia yake wakiongozwa na Abdul Hafidh Ameir ambaye ni shemeji yake, sijui amekaa upande gani? Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 151 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge, ambao ni Walimu na wanafunzi wa *Baobab Secondary* kutoka Mkoa wa Pwani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe, ambaye ni Diwani Kata ya Mwamanyili, Halmashauri ya Busega. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko kutoka Kitunguroma, Mkoa wa Mara. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo wanafunzi 73 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mary Francis Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameendelea kutulinda hadi ameweza kutufikisha siku hii ya leo ambapo tunakwenda kuhitimisha Bajeti yetu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele wa kuhakikisha kwamba uhifadhi na dhamira yake kuu ya kuendeleza utalii inazingatiwa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuipigania sekta hii ukizingatia kwenye masuala mazima ya uhifadhi wa mazingira, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba migogoro mbalimbali iliyokuwa kwenye sekta yetu hii ameendelea kuisimamia na kuitatua kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipokupongeza wewe kwa uthubutu ambao umeuonesha kama mwanamke mwenzetu.  Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu kwa harakati hii unayoiendea, tuna imani na wewe na tunaamini ushindi unarudi Tanzania. Tunakuombea sana na Mwenyezi Mungu akakufanikishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na nimpongeze kwa namna ambavyo ameipokea Wizara lakini kwa jinsi ambavyo ameipokea Wizara lakini kwa jinsi ambavyo ameichukua kwa muda mfupi na kuielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ina changamoto nyingi sana, lakini kwa muda mfupi tayari tumekwishaanza kuiona nuru na Waheshimiwa Wabunge tayari wameonesha kwamba wanakwenda kushirikiana na sisi kwa nguvu zote. Niendelee kumuahidi Bosi wangu kwamba tutashirikiana vizuri na nitampa

ushikiano wa kutosha kuhakikisha kwamba Wizara hii tunaipigania na kuivusha hapa ilipo na tunaipeleka mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge lakini niwapongeze sana kwa namna ambavyo wametupa ushauri, kwa namna ambavyo wametupa maelekezo, lakini kikubwa wametuonesha wapi tulipo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa nini? Unapokuwa umevaa nguo yako unaweza ukaona umevaa vizuri na umependeza, lakini ukikutana na mwenzio akakwambia hapa kuna doa huyo anakupenda sana. Vile vile, sisi tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wametuonesha ni namna gani tunapaswa kwenda. Niwaahidi kabisa kwa moyo wa dhati kwamba, yale yote ambayo wametuelekeza, wametushauri na yale ambayo wametupatia kama mapendekezo tumepokea na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya uhifadhi na hususani kulinda rasilimali za Taifa ni kazi kubwa sana na inahitaji ushirikiano wa kutosha. Kuna milima na mabonde, hizi rasilimali tulizonazo tunazozilinda, tunazitunza si rasilimali za mzaha. Tunakutana na milima, mabonde na changamoto nyingi, lakini tunaamini kwa maelekezo waliyotupatia Waheshimiwa Wabunge na kwa namna tunavyokwenda kushirikiana na wananchi kuzungumza, kushuka nao huko chini ili tukae nao kwa pamoja tutahakikisha kwamba migogoro mingi tunakwenda kuipunguza ama kuimaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta yetu hii inategemewa na sekta nyingi. Ukiangalia katika maliasili hatuhifadhi wanyamapori peke yake. Hatuhifadhi kwa ajili ya utalii, lakini ndani ya sekta hii kuna sekta nyingi zinaitegemea. Sekta ya nishati, usipokuwa na eneo maalum ulilohifadhi vyanzo vya maji na kadhalika hakika sekta ya nishati haiwezi kuendelea. Vilevile tuna sekta ya mifugo, sekta ya kilimo, tuna maji, mazingira na kwenye mazao pia tuna uchavushaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunatunza haya maeno sio kwa ajili ya kuendeleza utalii peke yake ni kwa sababu tunaishi na uhai wetu unategemea sana maeneo hayo. Kwa hiyo, ningependa hili tulielewe sisi kama wawakilishi wa wananchi kwamba maeneo haya tunayatunza kwa ajili ya Watanzania wote, ni kwa ajili ya maslahi yetu wote ni kwa ajili ya uhai wetu wote Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la migogoro Waheshimiwa wameliongelea. Natambua kwamba Mheshimiwa Waziri atalifafanua, lakini pia kwa yale yote ambayo wametuelekeza tutaendelea kuyafanyia kazi na tunatamani sana migogoro hii iishe. Niendelee kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, uthubutu huu wa kutatua migogoro hii ni mwanamke jasiri na wa kwanza aliyeamua kutekeleza wazo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukikumbuka migogoro hii imekuwa na historia ndefu sana. Iliundwa Kamati ya Mawaziri Nane ikaingia uwandani ikaanza kuibua migogoro. Hata hivyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa unyenyekevu mkubwa ameingia ndani akaamua yeye mwenye kuitekeleza. Ndani ya miaka miwili sasa hivi tunaelekea kutatua migogoro yote.

Mheshimiwa Spika, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais ndani ya mwaka mmoja tumezunguka na tumekwenda mkoa kwa mkoa, tumezungumza na wananchi, lakini hatuwezi kukataa mapungufu yapo, lakini tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna amabavyo anaendelea kutuelekeza na sisi tunaendelea kuahidi kwamba kwa ile migogoro ambayo bado ipo, tutashuka na tutakwenda kuzungumza na wananchi na kuhakikisha kwamba migogoro hii inakwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mikakati mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuifafanua na kuielekeza katika Wizara yetu ya Maliasili na Utalii, tumeipokea. Kuna suala zima la kuimarisha Utalii wa Fukwe. Kwa sasa Wizara imejipanga kuanisha maeneo ambayo yanaweza kuwa mahususi kwa ajili ya fukwe. Tumeainisha fukwe hizi katika Mkoa wa Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Pwani na Tanga, lakini pia tunakwenda kuangalia

maeneo ya Kanda ya Ziwa ili fukwe hizi sasa ziweze kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo kama walivyopendekeza Waheshimiwa Wabunge kwamba fukwe hizi zikimilikiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii basi itakuwa ni rahisi sana kwenye utekelezaji wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuna wazo lingine limetolewa la Kiberenge (Utalii huu wa *cable car*). Kwa sasa hivi Wizara imeshaweka mshauri mwelekezi ambaye ameshaanza kufanya upembuzi, kupata mawazo ya wadau mbalimbali na kuangalia namna ya masuala mazima ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kupokea mawazo na ushauri kutoka kwa wadau. Muda wa utekelezaji ukifika na wadau watakapokuwa wameshatupatia mawazo ya kutosha, zao hili la utalii la *cable car* litakwenda kutekelezwa kwa nguvu zote. Tunaamini kwamba kwa sasa hivi asilimia 80 ya utalii tunategemea sana utalii wa hifadhi kwa maana ya wanyamapori. Kwa hiyo sasa hivi tunajikita sana katika kutanua wigo katika mazao mengine ya utalii ikiwemo utalii huu wa kiberenge *(cable car)*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tumepata maoni mengi kutoka kwa Wabunge hususani suala zima la mali kale. Kwenye suala hili la malikale tumeanza kujitanua na hivi sasa ukienda hata Kilwa tumeshaanzisha utalii wa meli na sasa hivi tunapata watalii wengine kutoka nje ya nchi. Hii yote ni kuboresha maeneo mbalimbali ya kihistoria lakini wakati huo huo tunatanua wigo wa utalii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na suala la utalii tumeendelea kuhamasisha masuala mazima ya uwekezaji. Kama ambavyo tumesikia kwamba sasa hivi Tanzania tuna vitanda 132,676. Hiki ni kiwango kidogo sana kwenye masuala mazima ya uwekezaji ukilinganisha na mataifa mengine. Kwa hiyo, tumekwishazindua *investment forum* lakini pia tumeendelea kuhamasisha wawekezaji mbalimbali na hata humu ndani wawekezaji wamo. Tunaendelea kuwahamasisha tujenge *Hotel,*

*lodge,* tujenge maeneo ambayo watafikia watalii wetu ili tuweze kupanua wigo wa namna ya kuwahudumia wageni wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu miundombinu. Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana suala la miudombinu wezeshi ambayo inaweza ikasaidia utalii kufikika maeneo mbalimbali. Tumeshaanza kuboresha miundombinu hii ukizingatia tulikuwa tuna Hifadhi 16 za Taifa na sasa hivi tuna Hifadhi 22, maeneo haya yote tumeshaanza kutengeneza miundombinu ya barabara lakini pia tunaweka uwekezaji ndani yake ikiwemo kujenga *lodges* na *hotels* na hii ni maandalizi mazuri sana ya mapokezi ya wageni wanaoweza kuja katika hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na suala zima la misitu hususani upandaji wa miti, lakini pia tumeanzisha mpango kabambe unaitwa "Achia Shoka Kamata Mzinga." Huu ni mpango mahususi wa kuwezesha wenzetu wote ambao wanashughulika na suala zima la ufugaji nyuki wahakikshe kwamba ukataji wa miti tunaukomesha lakini tunafuga nyuki kwa kuachia shoka halafu tunakamata mzinga. Lengo ni kuhakikisha kwamba zao hili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** …na mazao mengine yanayotokana na nyuki yaweze kuboreshwa ama kulimwa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri aliweza kuzindua mpango huo…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, mtoa hoja aje ahitimise hoja ya Wizara yake ya Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada usiku wa deni haukawii kukucha." Baada ya siku mbili za michango mizuri sana ya Kamati na Waheshimiwa Wabunge, nianze hitimisho langu kwa kuahidi kuwa ingawa hapa nitajibu kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya masuala yaliyoibuliwa, lakini nikuahidi kwamba michango mingi ina tija na tunaandaa utaratibu ili tuweze kuijibu kwa maandishi michango yote ambayo imeulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba nichukue pia fursa hii niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, nitajenga matumaini katika mioyo ya Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waniruhusu niingie katika vifua vyao ili nipunguze mazito waliyoyabeba ya changamoto mbalimbali za migogoro ya aina mbalimbali inayohusu Wizara yetu. Natambua kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa amezungumza kuhusu changamoto, ndovu akataja kwa jina lingine watu wakacheka kidogo, lakini nikuthibitishie, nitaingia katika mioyo ya kila Mbunge, kwa sababu natambua kwamba Waheshimiwa Wabunge hawa wanafanya kazi kubwa ya kuzungumzia maslahi ya wananchi wetu katika maeneo yao. Kwa hiyo niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niseme tu mambo yafuatayo kwamba wananchi wetu waliotupa heshima ya kuwa katika Bunge hili Tukufu sisi pamoja na Chama chetu Tawala, yako mambo wanayoyahitaji sisi kama Serikali tuyafanye. Kwa muda mrefu Wizara yetu hii Wizara ya Maliasili na Utalii kwa miongo mingi sana wamepita Waheshimiwa Mawaziri wengi sana na kila nyakati ambazo Waheshimiwa Mawaziri wakisimama nyakati hizi za bajeti mambo mengi yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge imekuwa ni changamoto changamoto, changamoto kila siku ni changamoto katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hata yale mambo ambayo yanatuletea tija katika Utalii Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyasahau hawayazungumzi kwa mapana yake, kwa sababu Wizara hii toka nyakati za Baba wa Taifa mwaka 1961 mpaka nyakati hizi za Rais wetu wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumekuwa na changamoto, changamoto, changamoto. Sasa nadhani wakati umefika na lazima tuseme kwamba wakati ni sasa kuhakikisha kwamba sisi kama Wizara tunajipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba tunazimaliza changamoto zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumza ili tutakapokutana hapa mwakani tusizungumze tena changamoto, tuzungumze namna tutakavyoweza kukuza utalii wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge nikushukuru sana wewe, niwashukuru Maafisa pamoja na Wenyeviti wote wa Kiti chako kwa kusimamia vyema mijadala hii kuhusu Wizara hii kwa siku hizi zote mbili. Niendelee kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, mdogo wangu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea na kuchambua michango kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, lakini pia tumechambua michango ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia 57 na Mheshimiwa Mbunge mmoja amechangia kwa maandishi, jumla michango 58 tumeipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujielekeza kqwenye baadhi ya hoja, chambilecho wahenga, "mcheza kwao hutuzwa". Napenda kusema hapa nakuunga mkono Watanzania wenzangu kuipongeza Timu ya Yanga, lakini vile vile nimpongeze sana Rais wa Yanga, *Engineer* Hersi Said kwa kuendelea kuitangaza vyema nchi yetu nje ya mipaka ya Tanzania na dunia kwa ujumla kwa kushika nafasi ya pili kwenye Fainali za Kombe la Shirikisho Barani Afrika sambamba na kutoa Mfungaji Bora na Golikipa Bora wa mashindano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeiwezesha *brand* ya Tanzania kuzidi kujulikana katika mataifa mbalimbali na hivyo kuchochea hamasa za watalii na kutoa mataifa mbalimbali kwenye vivutio vyetu Tanzania. Kwa ushindi huo Wizara yangu inatoa *offer*, inatoa *offer* kwa wachezaji na viongozi wa klabu ya *Young African* baada ya kazi hiyo ngumu tutaratibu pamoja na viongozi wao kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Hifadhi ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu tutaufanya watakapokuwa mapumziko. Sambamba na hilo, naomba nichukue fursa hii kuwakaribisha mashabiki wote wa Yanga kwenda kujumuika pamoja na wachezaji wao katika safari hiyo katika tarehe itakayotangazwa na utaratibu utakaowekwa ziara hiyo tunaomba ipendekezwe iitwe kwa jina la *The CAf Finalist Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi na shukrani maalum ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kujitoa kwake tumeeleza humu jinsi filamu ya Tanzania *the Royal Tour* ilivyoleta mafanikio lukuki hapa nchini, lakini siyo tu kwa watalii kuongezeka lakini pia nchi yetu sasa ni kivutio cha mastaa mbalimbali na watu mashuhuri duniani wamekuwa wakija hapa nchini na wanaendelea kujakutokana na juhudi hizi za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wageni wetu hawa wanapenda faragha yao na tunazingatia hilo mara zote lakini wapo ambao wameridhia jamii yetu iweze kutambua Tanzania kutuunga mkono kwa kupitia filamu ya *Royal Tour,* hivi ninavyozungumza leo hii naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi juzi tumepokea wageni kutoka nchini Marekani; mtoto wa aliyekuwa Rais wa Marekani, mtoto wake na familia yake wapo hapa nchini Tanzania, bwana Donald Trump Junior yupo hapa nchini Tanzania amekuja kuunga mkono jitihada za Serikali na atakuwepo nchini kwa mapumziko ya siku kadhaa na nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aridhie ili kesho niweze kukutana naye kuzungumza ni namna gani wanaweza kutuendeleza katika biashara hii ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hoja za Kamati na Wabunge; Kamati yako lakini na Wabunge wengi zaidi ya 14 wakiwemo Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Tecla Mohamedi Ungele, Jacqueline Ngonyani Msongozi, Jeremiah Mrimi Amsabi, Simon Songe, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Deus Clement Sangu.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Waziri, hawa ni akina nani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, hawa ni Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwenye baadhi ya maeneo.

**SPIKA:** Kanuni zetu haziruhusu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tunao Wabunge wengi waliochangia kwenye baadhi ya hoja na wamechangia kwa hisia sana. Nichukue fursa hii kwanza kabisa kusema mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi zetu, *TANAPA, TAWA*, Ngorongoro, pamoja na *TFS* zinaongozwa na Jeshi la Uhifadhi, Jeshi Usu. Jeshi hili la Uhifadhi ni Jeshi ambalo limepewa mafunzo ya kutosha, Jeshi hili la Uhifadhi ukiangalia utaratibu wa kijeshi na Waziri wa Ulinzi angekuwepo hapa angenisaidia, ni jeshi la pili baada ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kama sijakosea.

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili lina mafunzo ya kutosha, kwanza niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao pengine wanaweza kujaribu ku-*undermine* uwezo wa jeshi hili basi watambue kwamba jeshi hili ni jeshi ambalo lina mafunzo ya kutosha na kwa kuwa jeshi hili lina mafunzo ya kutosha, kero za Wabunge hapa kila aliyekuwa anasimama anazungumzia kuhusu ndovu.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi kwamba kila panapotokea wafugaji wameingia ndani ya Hifadhi, wenzetu wa Jeshi la Uhifadhi wanachukua hatua za haraka sana na kila ambapo pengine wananchi wananingia kwenye Hifadhi, Jeshi la Uhifadhi linachukua hatua za haraka sana, lakini kelele zote za Waheshimiwa Wabunge hapa ndani ya Bunge kuhusu wanyama

hawa wakali kuingia kwenye maeneo ya wananchi, lazima tukiri kwamba hatua za haraka zinachelewa kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa na kwa bahati nzuri sana Jeshi la Uhifadhi chini ya *TANAPA, TAWA*, Ngorongoro linaongozwa na Majenerali wa Jeshi ambao walifanya kazi kubwa sana kwenye Taifa hili, kazi nzito sana kwenye Taifa hili, tunatambua tuna kazi kubwa ya kufanya kuendelea kuliimarisha jeshi hili, lakini naomba nitoe maelekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nimekwishakaa na Viongozi wa maeneo haya wa Ngorongoro *TAWA, TANAPA* na *TFS* lakini pia nimeshawakutanisha na viongozi mbalimbali wa Chama Tawala wanaotoka kwenye maeneo ya wananchi, tumekwishakubaliana kwamba Kiongozi yoyote wa Uhifadhi katika eneo lake iwapo Waheshimiwa Wabunge wataendelea kupiga kelele kwenye maeneo hayo na kiongozi huyo akaendelea kubaki ofisini, maana yake ni kwamba yule Kiongozi wa Taasisi ile mimi nitashughulika naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwishakubalina, kila mmoja wetu afanye kazi zake, kama tunaweza kuchukua hatua za haraka dhidi ya wafugaji wanaoingia ndani ya Hifadhi vilevile tuchukue hatua za haraka kuwaondoa wanyama wakali katika maeneo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo *zone* zetu za kila Hifadhi na tumekwisha kufanya kikao. Nikuthibitishie mimi ni tofauti kidogo na ninaposema namaanisha, kiongozi yoyote wa Uhifadhi ambaye yupo kwenye eneo lake na kunakuwepo na kelele za wananchi yeye kushindwa kushuka kwa wananchi kukaa na kuzungumza nao, maana yake huyo hanifai katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nichukue fursa hii kwanza kutoa pole kwa wananchi wote ambao wamepata madhara mbalimbali katika maeneo yote na ndio maana ningetamani sana hata kuwataja Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wamezungumza kwa uchungu sana, kila Mheshimiwa Mbunge kwa namna alivyozungumza na hatuna sababu ya kuwa na changamoto hizi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tunavyo vitengo vyetu mbalimbali tunatambua panapokuwepo na changamoto mara nyingi Wizara ya Maliasili na Utalii ndio inayoguswa lakini tunajipanga vizuri na wenzetu wa TAMISEMI kwa sababu katika kila Wilaya nchi hii tunao Maafisa Wanyamapori, lakini swali la kujiuliza ni kwamba hawa Maafisa Wanyamapori kila wilaya wanafanya kazi gani? Kwa sababu hata tukiwauliza Waheshimiwa Wabunge hapa pengine hata hawawajui Maafisa Wanyamapori kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo misingi ambayo Baba wa Taifa aliianzisha. Katika nyakati za Uhuru tulikuwa na Afisa Wanyamapori kila Kata na kwenye vijiji, lakini hapo katikati mambo kidogo yakabadilika na leo hii hatuna Maafisa Wanyamapori kwenye vijiji na kwenye Kata na kwenye Tarafa, lakini hili tumekwishalizungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishatuagiza ili tuandae mpango mkakati ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kupata Maafisa Wanyamapori katika meneo yetu hayo ya vijiji na maeneo ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosisitiza hapa, tutamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na wenzetu tutakaa ili tuweze kuzungumza, kuona uwezekano hawa Maafisa Wanyamapori wa Wilaya warudishwe kwenye Wizara hii ili niweze kuwashughulikia vizuri katika maeneo yao. Tunatambua yako maeneo Maafisa Wanyamapori wanafanya kazi nzuri sana, kwa mfano kule Tunduru aliyekuwepo Afisa Wanyamapori akifanya kazi nzuri sana lakini baadaye wakamhamisha, Mbunge wa Tunduru analalamika, sababu za kumhamisha mambo tu ya hovyohovyo ambayo hayaeleweki. Tumemwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naye ameridhia kuhakikisha kwamba Afisa yule aliyehamishwa kutoka Tunduru, arudi Tunduru akafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba changamoto hii imeleta vilio kwa wananchi katika baadhi ya maeneo na hata leo tunapozungumza kule Bariadi kuna mwananchi amekanyagwa na tembo muda tunapozungumza kule Bariadi. Kwa hiyo tunatoa pole kwa wananchi, lakini pia tunatambua kwamba changamoto hii ya wanyama wakali inaleta changamoto pia

hata mpaka kwetu. Hivi karibuni wiki mbili zilizopita askari wetu kule Ngorongoro amechomwa na ndovu na kufariki. Kwa hiyo ni changamoto ambayo ipo pande zote mbili, lakini tumeandaa mpango mkakati wa kuona ni namna gani tunakwenda kumaliza changamoto hizi, mpango wa miaka kumi (2020 mpaka 2024).

Mheshimiwa Spika, mpango huu mkakati umeainisha hatua za muda mfupi na hatua za muda mrefu ambazo tutakwenda kupambana ili kuweza kuhakikisha kwamba changamoto hizi tumezimaliza. Aidha nichukue fursa hii kama ambavyo nimesema kuwaomba wenzangu wakati huu utakuwa mgumu kidogo katika Wizara hii, tunataka kila mmoja wetu afanye kazi kwa uweledi. Kila mmoja wetu afanye kazi kwa uweledi huku tukitanguliza ubinadamu mbele, nadhani hii lugha imeeleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaombe Maafisa wetu katika maeneo mbalimbali tufanye kazi kwa uweledi tufanye kazi usiku na mchana na kauli yangu hapa ni kwamba hawa ni Askari Jeshi, maana yake tunataka kuona wakifanya kazi usiku na mchana, wakifanya kazi wakati wa jua, wakifanya kazi wakati wa mvua kuhakikisha kwamba wamekwenda kumaliza tatizo na migogoro mbalimbali ya wanyama wakali kuingia katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo lingine lenye migogoro, kati ya maeneo ya Hifadhi. Suala hili pia limegusiwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza jambo hili. Wewe mwenyewe ni shahidi kwamba Baraza la Mawaziri liliwateua Waheshimiwa Mawaziri Nane kwenda kuzunguka na kupita katika maeneo mbalimbali. Nakiri kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge hapa wamezungumza, yako maeneo ambapo pengine tunapaswa kuendelea kupita zaidi ili tuzungumze na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu, Baraza la Mawaziri ni kikao cha juu kabisa cha Serikali cha maamuzi. Sasa wapo Waheshimiwa Wabunge hapa wamelalamika kwamba yapo maeneo ambapo hakuna migogoro, wananchi wameridhia yale maamuzi ya Baraza la Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amekwishasema hapa,

sasa kama maamuzi yamefanywa na Baraza la Mawaziri na kuna watendaji katika Serikali kule chini ambao walipaswa kutoa matamko na mpaka leo hii hawajatoa matamko, maana yake wanakinzana na maamuzi yaliyofanywa na Baraza la Mawaziri ambalo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais. Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ni Mheshimiwa Rais mwenyewe, maamuzi haya yamekwishafanywa, yako maeneo ambapo hakuna migogoro, ni jukumu la wale watendaji waliokasimiwa mamlaka na Mheshimiwa Rais, kutoa matamko katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tumetoa mpaka tarehe 28 Mwezi wa Sita ili Waheshimiwa wanaohusika kwenye maeneo yao, yale yasiokuwa na migogoro kutoa matamko mara moja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amekwishalizungumza hili. Yako maeneo ambapo Baraza la Mawaziri limerejesha maeneo kwa wananchi. Kwa hiyo, sababu hii tunawataka wale wanaohusika watoe maelekezo ili yale matamko yaende yakawasaidie wananchi kwa sababu Mheshimiwa Rais ameridhia kwenda kuwagawia maeneo yale wananchi. Kwa hiyo, niwaombe waliokasimiwa mamlaka maeneo hayo kuhakikisha kwamba wamelitekeleza eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni tuhuma za askari wa uhifadhi kutumia nguvu na ubabe na mabavu. Baadhi ya Wabunge walizungumza hili, wamechangia katika eneo hili, naomba nisiwataje kwa misingi ya kanuni, wameeleza malalamiko kuhusu eneo hili na niwathibitishie tumekubaliana kufanya kazi kwa uweledi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ngoja nikuweke huru, ukiorodhesha ndio kanuni inakatakaza, kama unamjibu Mbunge na hoja yake mahususi huyo uliyemchagua inaruhusiwa, yaani vile ulivyokuwa unaorodhesha Wabunge waliochangia ndio kanuni inakataza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumza hivi kwamba kuna matumizi ya mabavu lakini nichukue fursa hii kama ambavyo nimesema, ndani ya hifadhi zetu kuna mengi. Tunao pia wafugaji ambao

wanaingia ndani ya hifadhi na silaha za moto, lakini pia tunao watu wanaoingia na silaha za moto ndani ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mambo mengine uridhie tu nisiyazungumze hapa, lakini nimepokea hoja hii ambayo imezungumzwa na Mheshimiwa Kasheku Musukuma pamoja na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, akituomba twende kufanya mapitio ya Sheria ya Uanzishwaji la Jeshi la Uhifadhi na nimtaarifu kwamba Wizara yetu inaendelea kufanya *reform* kubwa sana. Tunaendelea kufanya mapinduzi makubwa sana kwenye sekta zetu zote na nimtaarifu tu kwamba hakuna mlango utakaobaki bila kufunguliwa katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwishaanza kufanya mapitio ya sheria mbalimbali, tumekwishaanza kufanya mapitio ya kanuni mbalimbali, zipo kanuni ambazo zinaingiliana, zipo kanuni ambazo zinakinzana, lakini zipo kanuni ambazo hazitoi tafsiri sahihi iliyotolewa na sheria. Kwa hiyo, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili tutakwenda kulipitia na niko tayari baada ya Bunge hili nitakaa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi pamoja na Mheshimiwa Ally Juma Makoa pamoja na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ili niweze kupata ushahidi wa yale mambo ambayo wameyazungumza kuhusu askari ambao wanafanya vitendo kinyume na utaratibu wa Jeshi la Uhifadhi na iwapo nitapokea ushahidi huo tutachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutachukua hatua pale ambapo tunaona kabisa kuna vitendo vya hovyo vya uonevu, tutachukua hatua dhidi ya askari wote ambao wanafanya vitendo hivyo. Pia nilitaarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba tunaendelea na vikao na pengine tarehe 11, 12 tutafanya vikao na Wenyeviti wa Bodi *TANAPA,* Ngorongoro, *TAWA* pamoja na *TFS;* ili tuweze kujadiliana kwa pamoja kuhusu mchakato wa uanzishwaji wa jeshi hili la uhifadhi. Ili tuweze kujiridhisha katika maeneo yenye mapungufu na tuweze kuyarekebisha katika maeneo hayo. Niwaahidi tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tutakapokutana hapa mwakani haya mapungufu yote itakuwa ni makofi tu na furaha

kwa kweli. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifugo kutaifishwa na kutozwa faini. Kwa hotuba yangu kuu nilinukuu kauli ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akitoa hotuba ya *Arusha Manifesto* ambapo alisisitiza kwamba uhifadhi ni lazima tuamue. Sisi kama Taifa ni lazima tuamue na lazima tuseme ukweli kwamba kuna haja ya kulinda hifadhi zetu. Mheshimiwa Baba wa Taifa alisema kwamba, Taifa lolote bila uhifadhi si Taifa na akayaomba Mataifa mbalimbali kuhakikisha kwamba tunashirikiana nao katika uhifadhi. Hivyo, naomba nisisitize kwamba tuna kila sababu ya kulinda hifadhi zetu kwa ajili ya vizazi vya leo na vizazi vya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutambue tu kwamba hifadhi zetu zinachangia katika pato la kigeni zaidi ya asilimia 25 pamoja na kwamba kiasi hiki ni kidogo sana lakini lazima tukiri kwamba kwenye mchango katika Pato la Taifa ni karibu asilimia 21 na kwenye fedha za kigeni ni asilimia 25 naomba nirekebishe hilo kidogo. Kwa hiyo, tuna kila sababu ni kwa nini tuzilinde hifadhi hizi na niwaombe Waheshimiwa Wabunge pale ambapo tunajadili kuhusu uhifadhi basi kila mmoja wetu arejee kwenye kauli ya Baba wa Taifa aliyoitoa wakati ule wa Arusha akitoa hotuba yake kwenye Arusha *Manifesto*.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize hapa tena, kama Taifa ni lazima tukubali kwamba tunazo sheria, tunazo kanuni na sheria hizi kwa mfano sheria kuhusu *TANAPA* zimetoa miongozo za kutaifisha mifugo baada ya maamuzi ya Mahakama na kama kuna ushahidi wowote kwamba kuna afisa yeyote anataifisha mifugo bila uamuzi wa Mahakama, basi nipewe taarifa hizo ili tuweze kuzifanyia kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kwamba Mahakama ndio hutoa maamuzi wakati wa utaifishaji wa mifugo kwa mujibu wa sheria hizi. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kama wana vielelezo vya ziada, basi waweze kunipatia ili tuweze kuona ni namna gani tutaweza kuchukua hatua katika maeneo ambapo watendaji wetu

wamekuwa wakitenda mambo ambayo ni ya utovu wa nidhamu na ukiukwaji wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*TAWA*) na sheria nyingine suala hili pia limechangiwa na Kamati pamoja na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. Nitoe tu taarifa kuwa marekebisho ya utungaji wa sheria mpya hizi za kuzipa mamlaka zaidi taasisi hizi, zimefika hatua nzuri. Tunaendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwa na subira kwa sababu tunaendelea kufanya mapitio na hivi karibuni tutawashirikisha wadau ili tuweze kukamilisha urekebishwaji wa sheria hizi ili kuweza kutoa mamlaka lakini pia sheria ambazo zitaenda kusaidia katika uhifadhi wa eneo letu la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kukamilishwa kwa zoezi la Ngorongoro; nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati, lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye eneo hili. Jukumu la Serikali kwa misingi ya Ibara ya nane ni ustawi wa wananchi lakini kama inavyofahamika kwamba Serikali inafanya kazi pia kwa kupita utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ibara ya 67 imezungumzia kwa kina sana kuhusu uhifadhi, lakini namna ambavyo tuna kazi kubwa ya kuustawisha ustawi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba, suala la Ngorongoro limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge lakini nataka niwaahidi hapa kwamba wakati natoa hoja hapa Bungeni siku ya Ijumaa nilizungumza hili kwa kina kabisa na sisi kama Serikali hatutarudi nyuma, tunatambua kwamba tunao baadhi yetu wakishirikiana na vijana wengine wa Mataifa ya nje. Tena vijana hawa wa Mataifa ya nje ndio wamekuwa wengi sana. Wakienda huko wakizunguka zunguka kwenye baadhi ya maeneo mbalimbali, Mahakama za nje ya Nchi, Mahakama za Ulaya na maeneo mengine wakijaribu kututekenya. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu hatutarudi nyuma kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Watanzania wa Ngorongoro ambao wameridhia wenyewe kuhama kwa hiari kutoka Ngorongoro na kwenda kwenye maeneo mengine. Sisi kama Wizara tutaendelea kupitia maelekezo ambayo Kamati imetoa. Tutaendelea kutekeleza maelekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wametushauri kwenye Bunge hili Tukufu ili tuhakikishe kwamba utekelezaji wa jambo hili unatekelezwa, lakini tunatambua kwamba tunaendelea kufanya mashauriano na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba jambo hili tumelitekeleza kama ambavyo tumeahidi mbele ya Bunge Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mikakati ya kutangaza utalii. Kamati ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza sana kwa kina jambo hili, lakini pia katika hotuba yangu ya awali niliweka hadharani mikakati 10 ya kutangaza utalii ikiwa ni pamoja na ubunifu na teknolojia, ambavyo vitaongoza katika mchakato huu wa kutangaza utalii.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumza sana kuhusu hifadhi, lakini hatujazungumzia sana kuhusu utalii. Nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye mwenyewe kwa kulianza jambo hili. Niwashukuru Watanzania, niwashukuru pia wadau mbalimbali wa utalii ambao kwa kipindi kirefu sana wamefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana ya kutangaza utalii nje ya mipaka ya Tanzania lakini sisi kama Serikali sasa tumekwishalianza jambo hili. Nichukue fursa hii kuwaomba wawakilishi, Mabalozi wetu waliopo katika maeneo mbalimbali kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa, tunazipongeza Balozi mbalimbali ambazo zinafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana. Balozi wetu kila Nchini, Balozi wetu Nchini Afrika ya Kusini na maeneo mengine wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa, kama jambo hili likishikwa na kila Mtanzania, kila mwananchi wa Tanzania akitoka akazungumza mazuri kuhusu utalii, kuzungumza mazuri kuhusu Nchi yetu, Baba wa Taifa ameturithisha mambo makubwa, mambo mazuri amani na utulivu, lakini Taifa letu lipo katika eneo

jiografia ambayo hakuna popote Afrika. Tunaamini kabisa Mwenyezi Mungu ametupa akili, ametupa na uwezo wakati ni sasa, kila Mtanzania kutoka kuzungumzia mazuri kuhusu Taifa letu. Sisi kama Wizara pia tayari tumekwishaanza mazungumzo na wenzetu ta *Tripadvisor* tipo advisor wenzetu wa *Expedia* lakini pia tunaendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali ambao wao wana mchango mkubwa sana katika Sekta hii ya Utalii. Pia tunaendelea kuwakaribisha wadau katika Sekta ya Utalii walioko kwenye Mataifa mbalimbali duniani ambao tayari wamekwishaanza kuja kutoka China na maeneo mengine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nikuombe hotuba yangu hii iingie kwenye *Hansard* ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya vizazi vya leo na vizazi vya kesho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufafanuzi nilioutoa pamoja na maelezo mengi ambayo nimeyazungumza na kwa sababu ya muda, naomba sasa baadhi ya hoja nitaziwasilisha kwa ufafanuzi wa hoja nyingine kwa maandishi, lakini natambua hapa kwamba wapo Wabunge wakiwemo Wabunge wa Mbarali, Ngorongoro, Serengeti, Mheshimiwa Kakunda na wengine wote waliomba tufike kwenye maeneo yao na wengine ambao sijawataja kule Nachingwea kule kwa ndugu zangu Kusini na maeneo mengine, kote nitafika kwa ajili ya kupitia na kuzungumza na wananchi ili tuweze kufanya kazi hii ambayo tumekabidhiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ufafanuzi huo na majibu yote ya hoja niliyowasilisha na mengine nitakayowasilisha kwa maandishi, naomba yaingie kwenye *Hansard* ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Tukae**.**

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi inaanza na Kitabu cha Pili, Fungu 69, Wizara ya Maliasili na Utalii, ukurasa 570, katika kishikwambi ni ukurasa wa 569.

**MWENYEKITI:** Katibu tunaenda kwenye mafungu.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*........................................Sh.5,321,671,190
Kifungu 1002 - *Finance and Account Unit* ................Sh.1,262,095,924
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....................Sh.1,492,473,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*......Sh.505,004,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit* ..................................Sh.597,580,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*..........Sh.912,374,808
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit* ................................Sh.622,802,240
Kifungu 1008 - *Management Information System Unit*……….............………......Sh.1,068,709,000
Kifungu 1009 - *Research and Training Unit* .............Sh.17,519,509,100
Kifungu 1010 - *Paramilitary Coordination Unit*..........Sh.1,062,793,000
Kifungu 2001 - *Wildlife Development*....................Sh. 378,495,652,596
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*................Sh. 39,314,739,096
Kifungu 4001 - *Tourism* .............................................Sh.16,093,188,084
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit* ................................. Sh.10,232,856,962

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI**: Kitabu cha Nne Fungu 69 ukurasa wa 207.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit* ..................Sh.145,750,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* .................Sh.41,877,638,496
Kifungu 1008 – *Management Information System Unit* ...............Sh. 0
Kifungu 1009 – *Research and Training Unit* ..................................Sh. 0
Kifungu 2001 – *Wildlife*............................................Sh.108,849,828,100
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping*................Sh. 13,961,292,404
Kifungu 4001 – *Tourism* ..............................................Sh. 3,332,250,000
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit* .......................................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge baada ya kuwahoji na wote kusema ndio, nitumie nafasi hii kutangaza rasmi kwamba Bunge limepitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, mnafanya kazi nzuri na tunawatakia kila la kheri katika yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza hapa kuhusu wananchi, myachukue kwa uzito ule ule ambao Wabunge wameyasema hapa, kwa sababu nia ni njema uhifadhi tunahitaji hifadhi zetu lakini tuna hifadhi kwa ajili ya binadamu. Kwa hiyo, kama binadamu wanapata madhara Wizara hii ichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa kazi nzuri mnayoifanya. Mmemsikia hapa Mheshimiwa Waziri akieleza namna mnavyoshirikiana vizuri na namna ambavyo amesikia maoni ya Kamati pamoja na ya Wabunge. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia niwatakie kila la kheri Wizara katika utekelezaji wa bajeti hii ambayo imepitishwa na Bunge na tunaamini mtaitendea haki kama mlivyoaahidi. Niwashukuru nanyi kwa utulivu maana muda umeenda sana, lakini mmekaa mpaka muda huu ni uzalendo wa hali ya juu sana kwa hiyo nawashukuru sana na tunaelekea mwisho mwisho hivi, lakini

tuvumiliane kwa sababu Wabunge wengi wanavyotaka kusema hoja zinazowahusu wananchi wao kuwazuia kidogo inakuwa mtihani. Kwa hiyo turidhie pale ambapo inabidi Wabunge wawasemee wananchi na Serikali isikie, basi tuendelee kuvumiliana kwa namna ambavyo leo tumevumiliana, kwa sababu la sivyo ilikuwa Wabunge wengi wasizungumze na wananchi kule wanasubiri Wabunge wao waseme kuhusu athari wanazozipata. Kwa hiyo, tutajitajitahidi wakati mwingine kufuata muda lakini pale ambapo kuna mambo ya msingi itabidi tuvumiliane na tusubiriane kama leo, kwa hiyo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Waziri ulisema jambo moja tu hapa kuhusu hii *Royal Tour* umeita *Royal Tour* ya Yanga, sawa *whatever the name*, jina lolote watakaloitwa, lakini natamani ninyi kama Wizara kwa sababu ndio Wizara inayohusika hasa, mkae mtazame kama itakuwa ni sahihi, kwa sababu nimeshazikia hizo maeneo mengi, kama ni sahihi kutumia neno *Royal* kwenye hizo *tour* nyingine. Kwa sababu neno *Royal* wote tunafahamu linamaanisha nini na linavyopewa hiyo hadhi ni kwa sababu yule anyekwenda kule ni mtu wa hadhi hiyo, ya ufalme au umalkia.

Kwa hivyo, ninyi mtazame kama ni sahihi kuendelea kulitumia hilo neno *royal* ama mtumie neno lingine. Hii maana yake kama ninyi ndio mnaenda kufuatilia maeneo mengine wanafanyaje, kwa sababu kote zinapoitwa Royal Tour wanaohusika ni *Heads of State,* Wakuu wa Nchi zinazohusika. *(Makofi)*

Sasa hizi *tour* zetu, namwona Mbunge wa Iramba pale ananiangalia na yeye ana *tour* yake kule anataka kuita *Royal*. Kidogo tuangalie yale matumizi ili Serikali mtoe mwongozo mzuri kwa sababu kwa kweli mmehamasisha sana wananchi kwenda huko kutalii kujiunga kwenye makundi na nini. Sasa kama na wao watatumia hilo jina au hapana maana Tanzania tuna utaratibu hata watoto tunawaita *Prince* tunawaitwa *Princess* na hatujui atakapokuja hapa *Prince William* tutamwita nani, lakini ndio mambo kama hayo. Nawatakia kila la kheri ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naaharisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.18 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 6 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*